

Kwa nini na kwa namna gani Afrika inapaswa kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi

Dokezo la sera tetezi iliyojikita katika ushahidi na utendaji



Kwa nini na kwa namna gani Afrika inapaswa kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi

Dokezo la sera tetezi iliyojikita katika ushahidi na utendaji



maneno



safari



jifunze kutokana
na yaliyopita

© 2010 UNESCO Institute for Lifelong Learning
(Taasisi ya Elimu kwa Maisha Yote ya UNESCO)
Haki zote zimehifadhiwa

na Adama Ouane na Christine Glanz
Imeandaliwa kwa kushirikiana na Association for the Development of Education in Africa
(ADEA)

UNESCO Institute for Lifelong Learning
Feldbrunnenstraße 58
20148 Hamburg, Germany
Simu: +49(0)40. 44 80 41-0
Faksi: +49(0)40. 410 77 23,
uil@unesco.org, www.unesco.org/uil

Tafsiri ya Kiswahili ya: Why and how Africa should invest in African languages and
multilingual education. An evidence- and practice-based policy advocacy brief
Hamburg: UIL

ISBN 978-92-820-7001-7

Kwa ufadhili wa:

The Danish International Development Agency (DANIDA)
The Government of Norway
The Swedish International Development Cooperation Agency (SIDA)
The Swiss Agency for Development and Cooperation (SDC)

Usanifu wa michoro na maandishi:

Christiane Marwecki

Matumizi ya taipografia na hati za Kiafrika yamechochewa na Saki Mafundikwa (2007),
Afrikan Alphabets: The Story of Writing in Afrika. Mark Batty Publisher, New York

Picha kwa hisani ya:

Afar Pastoralist Development Association and Kinder in Not, Hassana Alidou,
Associates in Research & Education for Development (ARED), Alexander Cobbinah,
Ado Ahmad Gidan Dabino, Christine Glanz, Magueye Kassé,
Kha Ri Gude Literacy Campaign South Africa, Literacy and Adult Basic Education (LABE),
Operation Upgrade Adult Basic Education,
Œuvre suisse d'entraide ouvrière (OSEO), UNESCO/Sergio Santimano

Yaliyomo

Utangulizi: Elimu kwa wote kwa maisha yote katika Afrika yenye lugha nyingi tofauti	4
Kuwepo kwa lugha nyingi ni ukweli uliojipambanua Afrika	8
Mapendekezo ya kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi	10
Maswali ya msingi kuhusu elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi Afrika kusini mwa Sahara	12
1. Athari za elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi	15
2. Uwezekano wa kutumia lugha za Kiafrika katika elimu	21
3. Jinsi ya kusimamia kwa ufanisi hali halisi ya lugha nyingi katika elimu kwa wote kwa maisha yote	24
4. Kwa nini kufundisha kwa lugha-mama hunufaisha utendaji wa wanafunzi	27
5. Aina gani za modeli za lugha zina mafanikio makubwa Afrika?	31
6. Je, elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi inawezekana kugharamiwa?	39
7. Je, ni katika mazingira gani wazazi na waalimu huunga mkono elimu kwa lugha-mama?	45
Kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi ni uamuzi wa kiseru	48
Viambatisho	50
Kiambatisho 1: Mwongozo wa kiseru wa kuunganisha lugha na tamaduni za Kiafrika katika mifumo ya elimu (ADEA na UIL, 2010)	50
Kiambatisho 2: Nyaraka za sera za Afrika	58
Kiambatisho 3: Taasisi za Afrika	59
Kiambatisho 4: Programu za lugha nyingi/mbili Afrika	61
Kiambatisho 5: Fahaarasa ya msamiati wa kitaalamu	64
Marejeo	68

Elimu kwa wote kwa maisha yote katika Afrika iliyo na lugha nyingi tofauti

Katika karne ya 21, ujifunzaji ni kitovu cha jitihada za dunia ya kisasa za kutaka shughuli za kiuchumi zitumie maarifa. Ujifunzaji ni nyenzo muhimu zinazowawezesha watu binafsi kuwa wazalishaji na watumiaji wa maarifa ya dunia ya leo. Ujifunzaji ni kitu cha msingi kinachowawezesha watu kuwa raia makini na kutimiza matamano yao wenyewe. Ni nyenzo za ushindani wa kiuchumi na za maendeleo ya kijamii. Ujifunzaji bora haulengi tu kumfanya mtu kuwa mahiri zaidi, kuwa na ujuzi anuwai zaidi na kuwa mzalishaji zaidi, bali hulenga pia kumfanya mtu kulea hali tofautitofauti zilizopo miongoni mwa watu na kuelewa kinagaubaga utamaduni wake na desturi zake, huku akijizoeza kukabiliana na yale asiyoajua na kuweza kuishi na wengine. Aina hii ya ujifunzaji huhitaji kukuza udadisi na kuthubutu kuwajibika kufanya mambo yanayoweza kuwa ya hatari.


Dokezo hili la utetezi linalenga kuonyesha dhima ya msingi ya lugha katika kufanikisha ujifunzaji wa aina hii. Unalenga hasa kufutulia mbali fikra potofu na mkanganyiko uliopo kuhusu lugha za Kiafrika, na unafichua jaribio linalofanywa mara kwa mara la kuzitweza lugha hizi kwa kudai kuwa ni kikwazo katika ujifunzaji. Dokezo hili linatumia matokeo ya utafiti na utendaji kujadili aina ya sera ya lugha katika elimu inayofaa zaidi kwa bara la Afrika.

Mada ya lugha katika elimu ni suala ambalo limekuwa likizua mjadala tangu pale nchi zilizotawaliwa na wakoloni barani Afrika, Asia na Amerika Kusini zilipojipatia uhuru kisiasa. Katika chapisho muhimu la mwaka 1953, UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi, na Utamaduni) ilisitiza umuhimu wa kuelimisha watoto katika lugha zao za kwanza (UNESCO, 1953). Lugha na mawasiliano, pasi na shaka, ndiyo mambo mawili muhimu zaidi katika mchakato wa kujifunza. Taarifa ya *The Global Monitoring Report* mwaka 2005 (UNESCO, 2004) ilisitiza ukweli kwamba duniani, uchaguzi wa lugha ya kufundishia na sera ya lugha shuleni ni suala nyeti katika kujifunza kikamilifu. Katika utafiti muhimu kuhusu ubora wa elimu barani Afrika, uliofanywa na *Association for the Development of Education in Africa* (Shirika la Maendeleo ya Elimu Afrika) (ADEA, 2004), lugha ilijitokeza sana kama mojawapo ya kiamuzi kikuu cha ubora wa elimu. Hata hivyo, miaka zaidi ya 50 tangu kutolewa kwa tamko hilo la kwanza la UNESCO, na licha ya kuwepo kwa utitiri wa vitabu, makala, mapatano, maazimio na mapendekezo mengi kuhusu suala hili, ikiwa ni pamoja na mlolongo wa majaribio kadhaa ya uthibitisho yaliyotumia lugha enyeji katika shughuli za elimu na serikali, nchi nyingi za Kiafrika bado zinaendelea kutumia lugha za wakoloni kama lugha kuu za kufundishia na kuendesha shughuli za utawala.

Afrika ndilo bara pekee ambamo watoto walio wengi huanza shule kwa kutumia lugha ya kigeni. Kote barani Afrika, baadhi ya watu wanaendelea kushikilia dhana kwamba lugha za kimataifa zenye wigo mpana wa mawasiliano (Kiarabu, Kifaransa, Kiingereza,



Serikali inajenga mazingira ya lugha nyingi, Mali



Kihispania, na Kireno) ndizo njia pekee ya kuleta maendeleo ya kiuchumi. Kuna sababu za kiuadilifu, kihistoria, kisiasa, kisaikolojia na kijamii, na zile za kimkakati zinazoeleza kuwepo kwa hali hii katika nchi za Kiafrika, ikiwa ni pamoja na nchi hizi kutawaliwa na wakoloni na changamoto ya utandawazi iliyopo leo hii. Kuna mambo mengi ya kukanganya ambayo ni vigumu kuepukika, hasa pale yanapotumiwa kama kisingizio cha kuficha dhamiri za kisiasa za dola moja kutawala dola nyingine.

Matokeo ya tafiti mpya yanazidi kuonyesha matokeo hasi ya sera hizi: zinasababisha elimu duni na kutwezwa kwa bara la Afrika, hali inayosababisha »kuingia polepole kwa usahaulifu katika fikra za pamoja» (Prah, 2003). Mafanikio na mafunzo yaliyopatikana kutokana na hatua ndogo zilizochukuliwa na pia tafiti kubwa zilizofanywa kote barani humu na kwingineko yametoa ushahidi maridhawa unaohoji taratibu zilizopo na kupendekeza haja ya kutumia njia mpya za matumizi ya lugha katika elimu¹.

Kutwezwa kwa Afrika kunazidishwa na hali ya bara hili kukaribia kabisa kujitenga na mchakato wa kubuni na kuzalisha maarifa duniani kote. Afrika hutumia, wakati mwingine pasipo kuhakiki, taarifa na maarifa yaliyozalishwa kwingineko kwa kutumia lugha zisizojulikana kwa watu wake walio wengi. Uduni wa sekta ya uchapishaji barani Afrika ni mfano mmoja tu. Asilimia tisini na tano ya vitabu vyote vinavyochapishwa barani Afrika ni vitabu vya kiada na si vya habari za kubuni au vya ushairi vyenye kukuza uwezo wa kufikiri na wa kubuni wa wasomaji. Licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa tamaduni, Afrika ndiyo yenye idadi ndogo zaidi ya machapisho ya kitaaluma, kama inayodhihirishwa na International Social Science Citation Index (Kielezo Mtajo cha kimataifa cha Sayansi za Jamii), ambacho hujumuisha majarida ya kitaalamu ya kisayansi na kiufundi yanayoongoza duniani katika nyanja zaidi ya 100 za kitaaluma. Asilimia moja tu ya mitajo katika kielezo hiki ndiyo hutoka barani Afrika. Uzalishaji wa maarifa unaofanywa na wasomi Waafrika na kutumiwa na umma hufanyika nje ya Afrika. *UNESCO Science Report* ya mwaka 2005 ilionyesha kwamba Afrika huchangia asilimia 0.4 tu ya gharama za jumla za utafiti na maendeleo kimataifa, na katika kiasi hicho, Afrika Kusini huchangia asilimia 90.

Hata hivyo, ikumbukwe kwamba kuna tabaka adhimu la Waafrika walio weledi wa hali ya juu ambao wameweza »kuzitawala« kwa umahiri mkubwa lugha za wakoloni na kuzifahamu na huchangia kwa ustadi na kwa ubunifu katika kuendeleza maarifa mapya, wakati mwingine wakiunganisha hali halisi ya Afrika au wakiusoma ulimwengu kwa mitazamo ya Kiafrika. Hata hivyo, Mwamko wa Kiafrika unatoa wito kwa watu kuelewa kwa undani zaidi na kutegemea zaidi maarifa, maadili, na hekima za Kiafrika, na kuusoma ulimwengu kwa jicho jipya na kushiriki katika kupeana maarifa na kutumia tekinolojia mbalimbali kufungua njia na namna mpya za kuishi.

Hati ya lugha za Kibete hujumuisha pichataarifa za kifonetiki zaidi ya 400. Pichataarifa zilizotumiwa hapa zilichorwa na msanii Frédéric Bruly Bouabré kutoka Kodivaa (Mafundikwa, 2007)

1 Orodha ya tafiti na taasisi za aina hiyo zimetajwa katika Kiambatisho 3 na Kiambatisho 4.

**Matangazo ya vituo
vya redio huakisi
kuwepokwa lugha na
utamaduni anuwai
barani Afrika
Mtangazaji wa redio,
Msumbiji**



Matumizi ya lugha nyingi barani Afrika na kuwepo kwa tamaduni tofautitofauti ni raslimali ambayo, hatimaye, ni lazima itumiwe. Matumizi ya lugha nyingi ni jambo la kawaida barani Afrika. Ama kusema kweli, matumizi ya lugha nyingi ndiyo kanuni hasa inayotawala kila mahali. Matumizi hayo siyo tishio wala mzigo. Siyo tatizo linaloweza kulitenga bara hili na maarifa na ujio wa shughuli za kiuchumi zinazotolewa kupitia lugha za kimataifa zenye wigo mpana wa mawasiliano.

Kwa hiyo, uchaguzi wa lugha nyingi, kutambuliwa kwa lugha hizo na mwandamano wao katika mfumo wa elimu, kuendeleza uwezo wa lugha hizo wa kuwezesha kuwasiliana, na kupatikana kwazo kwa hadhira kubwa zaidi havipaswi kufuata kanuni ya ama lugha hii au lugha ile, bali vinapaswa kufuata utaratibu wa hatua kwa hatua, wenye kitovu kimoja kinachoshirikisha lugha zote.

Tunapendekeza kwamba sera na utendaji katika Afrika vilee matumizi ya lugha nyingi; hasa yale ya lugha-mama huku kukiwa na nafasi inayofaa na inayohitaji uwepo wa lugha za kimataifa zenye wigo mpana wa mawasiliano. Ni jambo la muhimu kuhakikisha kwamba hali hii ya kung'ang'ania lugha moja ya kikoloni haichukuliwi na matumizi ya lugha moja ya Kiafrika. Idadi kubwa ya lugha ni jambo tunaloweza kumudu. Si kweli kwamba muda unaotumiwa kujifunza lugha za Kiafrika au kujifunza kwa lugha za Kiafrika hupotea bure na kwamba, badala yake, ni bora kujifunza na kuwa mjuzi wa lugha zinazodhaniwa kuwa ni zenye manufaa zaidi na ni zenye kutoa matunda zaidi ambazo kwa hali halisi zinafaidika na hadhi kubwa zaidi zilizo nayo. Si kweli kwamba kujifunza lugha hizi au kujifunza kwa lugha hizi huchelewesha upatikanaji au ustadi wa maarifa ya sayansi, tekinolojia, na maarifa mengine ya ulimwengu na ya watu wote. Kwa kusema kweli, hadhi kubwa zaidi ambayo lugha hizi za kimataifa zinaipata inaimarishwa na mipangilio ya mamlaka iliyopo. Haifai kulinganisha lugha enyeji na zile za kimataifa kwa vigezo visivyo na masharti wala mipaka. Lugha za aina tofauti hizi hukamilishana kwa viwango mbalimbali vya manufaa, na ni lugha za lazima kwa maendeleo kamili na linganifu ya mtu mmoja mmoja na ya jamii.

Dokezo hili la sera tetezi ni mkusanyiko mfupi wa kile tunachokijua na kile kinachoelezwa na tafiti kuhusu matumizi ya lugha za Kiafrika katika elimu. Ni mkusanyiko na mapitio ya ushahidi na hoja husika za kuwajulisha wafanya maamuzi barani Afrika katika kufanya uamuzi mgumu wa kisera linapokuja suala la kutumia lugha za Kiafrika katika elimu na utawala. Uamuzi wao huwa mgumu zaidi na zaidi kutokana na ukweli kwamba wadau wawili muhimu sana – yaani wazazi na waalimu – wana uelewa usio sahihi kuhusu suala hili na huelekea kulipinga, kwa madai kwamba kuna haja ya kuhifadhi na kuhami maslahi adhimu ya watoto. Sera ya lugha ni uamuzi wa kisiasa, na wakati wote maamuzi ya kisiasa hayana budi kutumikia maslahi bora



kabisa na ya kiwango cha juu kabisa ya jamii au taifa. Kwa hiyo, muhtasari huu wa sera unashughulika pia na mawakala wa pande mbili au pande nyingi ili kuwapa habari kuhusu maamuzi wanayoyafanya pindi wanapofanya kazi na serikali za Kiafrika na kuwatahadharisha kuhusu matokeo ya matendo yao na ushauri duni.

Mwongozo huu utachunguza ushahidi wa tafiti zinazoeleza kinagaubaga fikra potofu, mikanganyiko, na vitisho vinavyolizunguka suala la lugha. Mwongozo huu unatumaini kuonyesha kwamba kuna manufaa halisi ya asili na yaliyo mazuri ya elimu inayotolewa kwa lugha-mama zaidi ya uambatisho wa kihisia wa mtu na uaminifu wake kwa utambulisho, utamaduni, na maadili.

Mwongozo huu wa sera uliandaliwa kwa ushirikiano na Association for the Development of Education in Africa (ADEA) ambalo kwa miaka mingi limekuwa mmojawapo wa washirika wa karibu zaidi wa UNESCO Institute for Lifelong Learning (UIL). Aidha, tunapenda kuwashukuru Hassana Alidou, Marie Châtry-Komarek, Mamphago Modiba, Norbert Nikiéma, Peter Reiner, Godfrey Sentumbwe, na Utta von Gleich, wataalamu bingwa wa lugha katika elimu na uchapishaji, kwa kupitia waraka huu.

Tunayo matumaini makubwa sana kwamba mwongozo huu utapunguza joto linalozunguka mjadala huu kwa kutoa umaizi na ukweli utakaopasha habari kuhusu maamuzi ya wazi na vitendo vinavyoleta ufanisi.

Adama Ouane
Mkurugenzi, UNESCO Institute for Lifelong Learning



Wanafunzi wakiji-
funza kuandika kwa
lugha mbili, Bukina-
faso

Kuwepo kwa lugha nyingi ni ukweli uliojipambanua Afrika

8

Idadi ya lugha zinazozungumzwa barani Afrika ni kati ya 1,000 na 2,500, kufuatana na makadirio na fasili mbalimbali. Hakuna taifa linalozungumza lugha moja tu, nazo lugha mbalimbali huzungumzwa katika maeneo mbalimbali pasipo kufuata mipaka ya nchi. Wakati nchini Rwanda na Burundi kuna lugha kati ya mbili na tatu, nchini Nijeria kuna lugha zaidi ya 400.

Hali halisi ya kila muktadha wa lugha nyingi ni changamani, ni ya pekee na ni yenye kubadilika (Gadellii, 2004): Karibu nusu (asilimia 48) ya nchi za Kiafrika zilizoko kusini mwa Sahara zinayo lugha ya Kiafrika inayozungumzwa kama lugha-mama na zaidi ya asilimia 50 ya watu wake. Na wakati mwingine kuwepo kwa watu wanaozungumza lugha hiyo kama lugha ya pili lakini kwa umahiri kama wa lugha-mama hufanya idadi ya watu wanaozungumza lugha hiyo kufikia zaidi ya theluthi mbili (asilimia 67). Lugha kumi na sita za Afrika zinazotambuka baina ya nchi na nchi huzungumzwa na watu zaidi ya milioni 150. Ukiacha sekta ya elimu, lugha za Kiafrika zisizopungua 56 hutumiwa katika shughuli za utawala, nazo lugha za Kiafrika zisizopungua 63 hutumiwa katika mfumo wa mahakama (mataifa 26 yaliyoko kusini mwa Sahara huruhusu kutumiwa kwa lugha za Kiafrika katika shughuli za utungaji sheria). Katika mawasiliano ya kibiashara yanayofanywa kwa njia ya maandishi, lugha za Kiafrika zisizopungua 66 hutumiwa, nazo lugha 242 za Kiafrika hutumiwa katika vyombo vya habari.

Kwa ufupi, kuwepo kwa lugha nyingi mno katika nchi moja na haki ya lugha hizi, si tu ya kuendelea kuishi, bali pia ya kupata maendeleo, huonyesha umuhimu mkubwa unaopaswa kuangaliwa kuliko vile zilivyo sasa. Wingi huu wa lugha wenyewe unachukuliwa kuwa ni tatizo asilia katika masuala ya mawasiliano, utawala na elimu.

Kuwepo huku kwa lugha nyingi huchukuliwa kama kikwazo cha mawasiliano na huonekana kama hali inayoleta migogoro na mivutano. Inadhaniwa kuwa kuongoza watu wa jamii-lugha nyingi mno ni tatizo na ni gharama kubwa. Historia ya ukoloni, ujio wa utandawazi, na urafiki na uhusiano wa karibu wa watu na wa jamii mbalimbali umewezesha baadhi ya lugha teule kuonekana kuwa na umuhimu mkubwa, hivyo kuwa na uwezekano zaidi wa kutumiwa kama daraja la kuunganisha wazungumzaji wa lugha nyingi enyeji.

Hii imewezesha lugha kuu za wakoloni kupata hadhi na heshima zaidi – huku lugha za Kiafrika zikikandamizwa, hususani katika elimu – kwani hutumiwa kama mlango wa kupatia elimu zaidi na kushiriki katika kubuni na kuendeleza maarifa. Kwa mujibu wa utafiti wa lugha wa kimataifa uliofanywa kwa agizo la UNESCO (Gadellii, 2004), lugha 176 tu za Kiafrika ndizo zinazotumiwa katika mifumo ya elimu barani Afrika, hasa katika elimu ya msingi: asilimia 87 ya lugha zinazotumiwa kufundishia watu wazima kusoma na



Tangazo kwa lugha tatu (Kiingereza, Kiganda, Kiswahili), Uganda

kuandika na katika programu za elimu isiyo rasmi ni lugha za Kiafrika; kati ya asilimia 70 na 75 ya lugha za kufundishia katika shule za chekechea na madarasa ya awali ya shule za msingi ni lugha za Kiafrika. Baada ya elimu ya msingi, lugha za Kiafrika zinazotumiwa katika elimu ya sekondari ni asilimia 25, na katika elimu ya juu ni asilimia 5 tu. Ingawa mifumo mingi ya elimu barani Afrika hulenga zaidi kutumia lugha za kimataifa, asilimia 10 hadi 15 tu ya watu katika nchi nyingi za Kiafrika ndio wanaokadiriwa kuwa wanaweza kuzungumza lugha hizi kwa ufasaha. Hata hivyo, lugha hizi, licha ya kuwa na nguvu kubwa katika shughuli za utawala, zimekithiri katika mifumo ya elimu, na matokeo yake ni kwamba kuna pengo kubwa mno la mawasiliano kati ya mfumo rasmi wa elimu na mazingira yake katika jamii.



Mapendekezo ya kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi



Matokeo ya tafiti na utendaji yawasilishwayo kwa kina zaidi hapa chini yanatufanya tutoe mapendekezo yafuatayo kuhusu kutunga sera na kuweka mipango ya elimu katika Afrika yenye lugha nyingi na tamaduni nyingi. Mapendekezo haya yanaendana na African Union's Language Plan for Action (Mpango-Kazi wa Lugha wa Umoja wa Afrika) (2006).



- 1.** Kufanya matumizi ya lugha nyingi kuwa ya kawaida ili kuleta mshikamano wa kijamii, maendeleo ya watu binafsi na ya jamii kupitia sera za lugha zinazotumia ustadi wa asili wa lugha mbili au zaidi kama msingi. Sera za aina hii hazina budi kukitwa katika maono ya kijamii ya nchi, kutumiwa katika mfumo wa kutunga sheria, na kujitokeza katika mipango, bajeti, na tafiti zinazogusa sekta zote za jamii.



- 2.** Kuamua kuthamini na kuendeleza lugha za Kiafrika kama njia iliyo kabambe zaidi kwa mawasiliano na chanzo cha utambulisho wa watu walio wengi wa Afrika, na kutunga sera zote za lugha ipasavyo (kama vile kukubali lugha za Kiafrika kuwa lugha rasmi na lugha zinazotumiwa katika mitihani).



- 3.** Kuweka mfumo wa ushirikiano thabiti katika elimu miongoni mwa wadau wote (serikali, watoa huduma ya elimu, wataalamu bingwa wa lugha na wa elimu, soko la kazi, jamii enyeji, na wazazi) ili kuanzisha mazungumzo shirikishi na kuandaa watu wa kuunga mkono kwa kiwango kikubwa elimu anuwai, ya jumla, iliyounganishwa, itolewayo kwa lugha nyingi, itakayosaidia kuleta uwajibikaji na uwazi.

- 4.** Kuweka mpango wa kuwa na elimu ya msingi kwa lugha-mama na lugha mbili au zaidi kama masomo kwa kutumia modeli kawizi au modeli za nyongeza, kuuendeleza kwa ujasiri na kuutekeleza bila kukawia kwa kutumia modeli zilizorekebishwa ili kuendana na maono, hali, na raslimali za pekee za nchi husika. Ili elimu iweze kuendana na mahitaji ya watu, kuanzia mwanzo haina budi kuwaandaa wanafunzi kuwa raia makini na kuwawezesha kuendelea na shughuli za ujifunzaji maishani mwao.

- 5.** Kuongeza upatikanaji wa elimu na taarifa, na kufanya ufundishaji ulete matokeo yanayotakiwa kwa kuondoa kikwazo cha lugha, kutumia lugha ambazo wajifunzaji wanazimudu vizuri, kutumia mitaala inayoendana na mahitaji ya kijamii na kiutamaduni ya watu, kuendeleza zaidi lugha za Kiafrika kwa matumizi ya kitaaluma, kuwapa mafunzo waalimu kuhusu namna ya kushughulikia hali ya kuwepo kwa watu wanaotumia lugha



nyingi na ya kuwepo kwa tofauti za kiutamaduni na vilevile kuendeleza lugha na ujuzi wa kusoma na kuandika, na kutoa vifaa vinavyofaa vya kufundishia na kujifunzia. Kuboresha kabisa matumizi ya lugha pamoja na kutumia mbinu za kufundishia, vifaa vya kufundishia, na mitaala yenye ubora wa hali ya juu na inayoendana na mahitaji ya jamii kutaleta matokeo mazuri zaidi, viwango vya chini zaidi vya wajifunzaji wanaoacha au kurudia masomo kote katika mfumo wa elimu na hivyo kuweka mfumo wa elimu unaotumikia maendeleo ya watu binafsi na ya jamii barani Afrika.

6. Kutambua kwamba uchaguzi wa lugha na jinsi lugha zinavyotumika darasani vinaweza kukwamisha au kuwezesha mawasiliano na ujifunzaji, yaani, kunaweza kuwawezesha au kutowawezesha watu. Mawasiliano ni nyenzo muhimu kwa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kuweza kuleta matokeo yanayotakiwa. Mawasiliano ni kitu cha msingi vilevile katika kutumia na kubuni maarifa. Zaidi ya hayo, uhusiano baina ya matumizi ya lugha darasani na maisha ya wajifunzaji nje ya shule huukilia iwapo kile kinachofundishwa kinaweza kutumiwa na kutekelezwa au la, yaani, iwapo elimu inaendana na mahitaji ya wajifunzaji na ina nguvu ya kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya jamii.
7. Kutumia utaalumu na raslimali zilizopo na kuendelea kujenga uwezo mbalimbali katika sekta ya elimu na habari, na mahali pa kazi vilevile. Kugawana majukumu miongoni mwa vyuo vikuu, taasisi za mafunzo ya ualimu, vyombo vya habari, soko la kazi, shughuli za biashara, na taasisi nyingine zenye utajiri wa raslimali.
8. Kufanya utafiti unaogusa nyanja mbalimbali, kujenga maridhiano na kufanya kampeni za kuwapa watu maarifa mapya zaidi kuhusu umuhimu wa lugha katika elimu na katika kuleta maendeleo.
9. Kushirikiana baina ya nchi na nchi na kutumia raslimali za ukanda husika.
10. Kutumia Mwongozo wa Sera wa Kuunganisha Lugha na Tamaduni za Afrika katika Mfumo wa Elimu (tazama Kiambatisho 1).

Maswali ya msingi kuhusu elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi Afrika kusini mwa Sahara



12

Alama za Adinkra za Waakani (Ghana, Kodivaa) huwakilisha methali, matukio ya kihistoria, mitazamo, vitu, wanyama, na mimea. Awali, zilichapwa kwenye nguo ili zivaliwe na kuonyeshwa kwenye matukio muhimu ya kijamii. Leo hii, huchapwa pia kwenye vyombo vya udongo na vya metali, na hutumiwa katika usanifu majengo na sanaa ya uchongaji (Mafundikwa, 2007).

Msukumo wa waraka huu ni matokeo ya shauku mpya ya kutaka kushughulikia suala la matumizi ya lugha nyingi barani Afrika kwa ubunifu na kwa namna ijengayo, nayo shauku hii inachochewa na mambo makuu mawili. Kwanza, kuna ushahidi wa kutosha (ingawa si kila mtu anakubali hivyo) kwamba lugha nyingi ni raslimali ya maendeleo ya taifa. Pili, Afrika inapaswa kuilea na kuitumia kikamilifu tunu hii ya asili kwa ustawi wa watu wake, kwani wakati wote bara hili litakuwa katika hali ngumu kutokana na kukumbatia lugha za kigeni, bila ya kujali jinsi zilivyojikita katika mandhari ya lugha kitaifa. Suala hili limekuwa likijirudia mara kwa mara katika ajenda ya sera, utamaduni, na elimu ya bara hili.

Mwaka 2003 katika Mkutano wa Kila Baada ya Miaka Miwili wa Association for the Development of Education in Africa (ADEA) ulioitwa »Improving the Quality of Education in sub-Saharan Africa«, mojawapo ya mada kuu zilizojadiliwa ilikuwa ni matumizi ya lugha za Kiafrika kama kigezo cha kuleta elimu bora. Mada hii ilijitokeza tena katika taarifa ya mwaka 2006 ya *Education for All Global Monitoring Report* iliyoitwa *The Quality Imperative*. Uboreshaji wa elimu ni moja kati ya malengo sita ya »Elimu kwa Wote«. Katika mikutano iliyofuatia ya ADEA ya kila baada ya miaka miwili, matokeo ya tafiti yaliyowasilishwa kuhusu elimu ya msingi kwa lugha-mama na lugha ya pili kama somo yameleta msukumo wa kufanywa kwa mijadala mikali na haja ya utafiti zaidi. Kama ilivyonukuliwa katika kumbukumbu za mkutano wa mwaka 2003:

Washiriki walihitimisha kwamba lugha za Kiafrika zilikuwa chaguo la lazima ili kukabiliana na changamoto hizi mpya: »Hebu turudi kwenye utambulisho wetu wa Kiafrika! Tusiendeleo kung'ang'ania mambo ya kikoloni!« alisihi waziri mmoja. Hata hivyo, watunga sera wengi waandamizi wa sekta ya elimu kutoka nchi mbalimbali waliendelea kuonyesha moyo wa kusita. Hawa ni watu ambao walipitia changamoto mbalimbali za mabadiliko ya lugha katika mtaala na waliozoea kukutana na upinzani dhidi ya kuingiza lugha za Kiafrika shuleni. Waziri mmoja alikumbuka tukio moja ambapo mzazi mmoja kijijini alimwambia: »Kujua maarifa fulani kwa lugha-mama hakumfanyi mtoto afanikiwe maishani, bali uwezo wake wa kujua Kiingereza. Je, kutakuwa na shule za matajiri na nyingine za maskini? Mwisho wa yote, tunatarajiwa kufanya mitihani na kufaulu kwa Kiingereza!« (ADEA, 2004: 38).

2 Kwa fasili ya msamiati maalumu kuhusu lugha na modeli za elimu ya lugha, tazama faharasa katika Kiambatisho 5.

Kutafuta ushahidi ili kufanya maamuzi eledi

Ili kueleza bayana masuala yanayoleta ubishi na kuwasaidia watunga sera na waelimishaji kufanya maamuzi eledi, mradi wa utafiti mpana wa tathmini ulichunguza uzoefu wa programu 42 za elimu kwa lugha-mama na kwa lugha nyingi² katika nchi 25 za Afrika zilizoko kusini mwa Sahara kwa kipindi cha miongo minne iliyopita. Utafiti huu ulifanywa kwa agizo la ADEA na kuungwa mkono na Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ) na kufanywa na kikosi cha wanazuoni mahiri sita kutoka UNESCO

Institute for Lifelong Learning (UIL). Matokeo ya mapitio haya ya tathmini yaliwasilishwa kwenye mkutano wa ADEA wa mwaka 2006 mbele ya kundi kubwa la wanazuoni na wataalamu wa mabadiliko katika elimu na vilevile mawaziri wanaoshughulikia masuala ya elimu. Ushahidi muhimu uliotumiwa katika muhtasari huu unatokana na utafiti huo (Alidou na wenzie, 2006).

Tangu kufanywa kwa utafiti huo, nchi kadhaa kama vile Bukinafaso (tazama Alidou na wenzie, 2008), Ethiopia (Heugh na wenzie, 2007), Malawi, Msumbiji, na Nijeri (tazama Alidou na wenzie, 2009) zimeanza kazi ya kutathmini, kuboresha, na kupitia upya mikakati na sera zao kuhusu matumizi ya lugha katika elimu. Data zinazohusiana na hatua hizi mpya za maendeleo zilipatikana na kutumiwa katika waraka huu.

Lengo la UNESCO kuchapisha dokezo hili la sera ni kutoa muhtasari mzito wa utafiti wa kisayansi na uliofanyiwa majaribio kuhusiana na suala la lugha katika elimu barani Afrika, kwa kulenga zaidi matumizi ya lugha na jinsi yanavyoathiri ubora wa elimu na wa ujifunzaji. Maswali makuu katika mijadala inayohusu utekelezaji wa elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi yanashughulikiwa hapa kwa utaratibu maalumu. Utafiti wa tathmini uliotajwa hapo awali ni raslimali muhimu, lakini kwa vyovyote vile si raslimali pekee.

Wakati umefika kutangamanisha nyanja mbalimbali

Waandishi wa taarifa ya mapitio ya tathmini wanaona kwamba (a) kwa kiasi kikubwa, uhusiano uliopo baina ya maendeleo na matumizi ya lugha hupuuzwa; (b) mbali ya wataalamu, kuna watu wachache tu wanaofahamu uhusiano uliopo baina ya lugha na elimu; na (c) watu wengi wanakubali kwamba kuna uhusiano baina ya maendeleo na elimu kutokana na uelewa wa juujuu tu, kwani wanaelewa kidogo sana maana halisi ya uhusiano huo. Kwa hiyo, kwa siku zijazo, kunapendekezwa kuwepo na ushirikiano wa karibu zaidi baina ya wataalamu wa lugha, wataalamu wa elimu, wataalamu wa uchumi, wataalamu wa masuala yahasuyo asili ya binadamu na maendeleo yake ya awali, na wataalamu wa elimu-jamii. Sekta ya mawasiliano kwa maendeleo na ile ya vyombo vya habari hazina budi kushirikishwa kwani nyanja hizi hutoa mchango muhimu sana katika elimu na ujifunzaji. Kila tabaka lina kundi la wataalamu makini ambao kwa kawaida hujenga hoja kulingana na mitazamo yao. Hadi sasa, wamefanya mawasiliano baina yao kwa nadra. Hata hivyo, kila mmoja wao analiona suala hili kuwa ni changamani mno kutafutiwa ufumbuzi kwa kutumia mtazamo mmoja tu. Wakati umefika sasa kutangamanisha nyanja mbalimbali.

Kusisitiza uzoefu barani Afrika

Kwa kuwa msisitizo hapa umewekwa kwenye uzoefu mbalimbali wa elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi barani Afrika, kwa kiasi kikubwa data hizi zinatoka barani Afrika. Hata hivyo, kuchagua data hizi haina maana kuwa ujifunzaji katika miktadha isiyokuwa ya Kiafrika umepuuzwa. Mara nyingi huko nyuma kosa lililokuwa likifanywa ni kuhamisha matokeo ya tafiti za masuala ya lugha katika elimu kutoka nchi zilizoendelea kiviwanda na kuyatumia vile yalivyo katika muktadha wa Kiafrika ingawa miktadha ya lugha ni tofauti sana. Barani Afrika, wanafunzi wengi huikuta lugha rasmi ya nchi yao – ambayo ni lugha ya kigeni – kama lugha ya kufundishia shuleni, lakini haipo katika maisha yao ya kila siku. Mara nyingi wanafunzi wa Kiafrika hujishughulisha na lugha kadhaa katika mawasiliano yao ya kila siku, lakini hawajishughulishi na lugha rasmi. Katika nchi zilizoendelea kiviwanda, wahamiaji na jamii zenye watu wachache huishi katika mazingira ambamo kuna lugha rasmi siku hadi siku.

Maana ya »lugha-mama« barani Afrika

Ili kuweka msingi thabiti wa fasili yake katika hali halisi ya lugha barani Afrika, tunafasili lugha-mama kwa mtazamo mpana kama lugha ambayo au ambazo huzungumzwa katika



Sankofa

»Rudi uipate«
Jifunze kutokana na
yaliyopita

mazingira ya karibu na hutumiwa kwa mawasiliano ya kila siku na ambayo au ambazo »humlea« mtoto katika miaka minne ya kwanza ya maisha yake. Hivyo basi, lugha-mama ni lugha ambayo au ambazo mtoto hukua nazo na ambayo au ambazo mtoto hujifunza miundo yake kabla ya kuanza shule. Katika miktadha ya lugha nyingi kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto hukua na kujikuta wakizungumza lugha zaidi ya moja kama lugha-mama kwani kuna lugha nyingi zinazozungumzwa kwenye familia ya mtoto au kwenye mazingira yanayomzunguka.

Je, masuala yapi huleta ubishi kuhusu elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi barani Afrika?

Hoja kuu zinazojirudiarudia na zinazoendelea kuwepo dhidi ya elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi zinaelezwa kwa muhtasari hapa chini.

- Kwanza, kutumiwa kwa lugha-mama kadhaa katika elimu kunachukuliwa kuwa ni kikwazo kwa umoja wa kitaifa. Kwa maneno mengine, inadaiwa, umoja wa kitaifa huhitaji kuwepo na lugha rasmi moja, kwani matumizi ya lugha-mama kadhaa hudhaniwa kushadidia migogoro baina ya jamii na jamii. Kwa hiyo, hoja inatolewa kwamba, ili kuzuia au kukomesha migogoro ya aina hiyo, ni lazima watu wa jamii na wa makabila mbalimbali watumie lugha moja, na mara nyingi lugha hiyo iwe ni lugha ya kigeni.
- Pili, lugha za Kiafrika zinadhaniwa haziwezi kujifanya kuwa za kisasa au kuendelea au kuendelezwa, na kwa vyovyote vile ni duni zikilinganishwa na lugha zilizotumiwa na wakoloni ambazo sasa zinatumiwa kama lugha rasmi. Hivyo basi, lugha za Kiafrika hazina uwezo wa kutumiwa kama lugha za kufundishia elimu ya juu na kama chombo cha kuelezea masuala ya sayansi na teknolojia. Kwa sababu hiyo, hazina budi kuachwa na kuhamia kwenye lugha zinazotumiwa kimataifa.
- Tatu, matumizi yenye nguvu na ya watu wote ya lugha-mama huleta hatari ya kujitenga. Huchukuliwa kuwa ni kuingilia kati ukuzaji wa lugha ya kimataifa, hivyo kusababisha kuwepo kwa maarifa pungufu na ufujaji wa lugha kwani muda wowote ule unaotumiwa kujifunza lugha-mama huleta madhara kwa lugha 'zinazozungumzwa na wengi', hususani zile za kimataifa. Hata matumizi ya lugha mbili kama kiungo wakati mwingine huonekana kama kikwazo na mzigo.
- Nne, faida za kisaikolojia, kiisimu, na kiutamuzi zinazotajwa kutokana na kujifunza kwa lugha-mama zinachukuliwa kuwa zinatokana na zinatolewa na vikundi shawishi vya watu wachache wa tamaduni mbalimbali na wala kwa hakika hazihusiani na ukweli wa uchunguzi uliofanywa.
- Tano, inadaiwa kwamba, kwa mtazamo wa kiuchumi, kuwa na uwezo usiobadilika wa kujua kusoma na kuandika kwa lugha-mama tu ni kosa. Hoja zinazojengwa kuunga mkono jambo hili ni kwamba kuongezeka kwa idadi ya lugha zinazotumiwa katika elimu husababisha ongezeko la gharama kwa takriban namba kipeo; kuna uhaba sugu wa vitabu na vifaa vya kufundishia na matatizo yanayohusiana na kazi za ubunifu, utafsiri, uchapishaji, na usambazaji katika lugha hizi. Kuna upungufu mkubwa wa waalimu wenye maarifa ya lugha-mama hizi na kutoa mafunzo ili kuwapata kutaleta gharama kubwa za ziada.
- Mwisho, wazazi na waalimu hukataa elimu kwa lugha-mama, hivyo watagomea mabadiliko ya kisiasa yanayotaka elimu itolewe kwa lugha-mama.

Kwa kuzingatia ushahidi unaotokana na utafiti na mazoezi barani Afrika, na mifano kadha wa kadha kutoka maeneo mengine ya dunia, matatizo haya makuu yanajadiliwa katika sehemu 7 zifuatazo kwa kulenga mifano thabiti na kutoa mapendekezo thabiti.

1. Athari za elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi

Tatizo

Elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi ni kikwazo kwa maendeleo na kwa umoja wa kitaifa

Kwa muda mrefu duniani kote, hali ya kuwepo kwa lugha nyingi imekuwa ikionekana kuwa ni tishio kwa mshikamano wa kitaifa na kwa maendeleo ya kiuchumi. Mtazamo huu ni sehemu ya dhana kuu ya watu wa Ulaya ya kutaka kujenga taifa lenye »nchi moja, utamaduni mmoja, lugha moja«. Ili kufikia lengo hilo, siasa za mabavu za kulazimisha watu wafuate tamaduni na lugha za watu wengine na siasa za »kuwagawa watu ili kuwatawala« zimepitiwa na watu duniani kote. Hivyo basi, nchi nyingi zenye wingi wa lugha na tamaduni zilijikuta zikishughulikia kizungumkuti cha kuwepo kwa lugha mbalimbali kwa kujaribu kurahisisha matumizi ya lugha ili kuwa na lugha rasmi moja na wakati huohuo kuzipa hadhi ya chini lugha nyingine zinazozungumzwa katika nchi hiyo. Historia inatufundisha kwamba mitazamo inayotumia sera ya aina hii haileti manufaa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi wala amani kama inavyoonyeshwa na Human Development Report mwaka 2004 ambayo imerejelewa hapa chini.



15

Nsa

»Mwavuli wa Katamanso
– kulifunika taifa«
Ulinzi

Majibu

Kutatua migogoro kwa kutambua kuwa watu wana lugha na tamaduni mbalimbali

Katika karne ya 20, mataifa zaidi na zaidi yalizidi kutumia sera na kufanya kazi kubwa ya kusimamia tofauti zilizopo miongoni mwa watu kwa namna ya kujenga na kuheshimu utambulisho wa kiutamaduni. Katika muktadha huu, utafiti uliweza kuvunjilia mbali imani potofu mbalimbali zilizohusiana na tofauti zilizopo miongoni mwa watu na hali ya taifa husika (Human Development Report 2004):

1. Kutambua utambulisho wa kiutamaduni wa watu mbalimbali kumetatusa migogoro badala ya kuianzisha kwa sababu utambulisho wa kiutamaduni haukuwa chanzo cha migogoro hii. Utambulisho wa kiutamaduni ulitumiwa kuchochea migogoro hiyo; kwa kawaida, migogoro hii huletwa na kutokuwepo kwa usawa kiuchumi na kugombea madaraka.
2. Matumizi ya lugha nyingi ni kiini cha utambulisho wa watu mbalimbali. Siku zote wanadamu wana mambo mbalimbali yanayowatambulisha (jinsia, dini, utaifa, taaluma, kabila, na marafiki). Wao ni sehemu ya makundi mbalimbali katika jamii na hushiriki maadili ya makundi hayo. Hivyo basi, kutambua kuwepo kwa tofauti mbalimbali miongoni mwa watu hakupingani na juhudi za kuleta umoja wa kitaifa kwa sababu siku zote utambulisho wa kitaifa utaendelea kuwa mojawapo ya mambo yanayomtambulisha mtu mmoja mmoja.
3. Hakuna uthibitisho kwamba maendeleo duni ya kiuchumi ni matokeo ya kuwepo kwa tofauti za lugha na utamaduni miongoni mwa watu. Badala yake, kuna viashiria vinavyoonyesha kwamba maendeleo ya kiuchumi hutarajiwa kuwepo kwa sababu watu wengi zaidi wenye uwezo na wabunifu huweza kutoa mchango wao (tazama pia Djité, 2008; Stroud, 2002).

Kwa kuzingatia matokeo haya, inapendekezwa kwamba sera fanisi ya lugha haina budi kuakisi hali halisi ya lugha katika nchi husika. Kukubali matumizi ya lugha nyingi ndiyo njia ya kistaarabu zaidi ya kushughulikia lugha zinazozungumzwa na watu wanaoingiliana, kwani humwezesha mtu kumudu lugha kadhaa. Kwa jumla, matumizi ya lugha nyingi

hayaashirii faida au hasara anayoweza kuipata mtu au jamii; bali huonyesha jinsi watu hawa na jamii hizi zilivyo, na tabia wanazozindeleza. Si jambo linalowezekana kuchagua lugha »isiyopendelea upande wowote« kwani hakuna lugha yoyote inayoweza kujitenga na wazungumzaji wake. Wakati ikionekana kuwa daraja la kuunganisha wazungumzaji wa lugha mbalimbali enyeji, lugha ya kigeni inayotumiwa kama lugha rasmi huleta utegemezi na uhusiano duni na hivyo kimsingi huwanyima watu uwezo.

Maendeleo ya jamii kwa kuhamasisha watu wote

Kwa kiasi kikubwa, maisha ya kijamii barani Afrika huendeshwa kwa kutumia lugha za Kiafrika; hivyo basi, elimu kwa lugha-mama hugusa mazingira waliyomo wajifunzaji. Wajifunzaji wanaweza kutumia moja kwa moja katika mazingira yao kile walichojifunza. Tathmini za programu za elimu isiyo rasmi (tazama, mathalani, Fagerberg-Diallo, 2006) zinaonyesha kwamba kujifunza kusoma na kuandika kwa lugha ambayo au ambazo hutumiwa katika jamii fulani huwahamasisha wajifunzaji. Wajifunzaji hushiriki na kuwa viongozi katika asasi na vyama vilivyoko katika maeneo yao. Uwezo wao wa kujiamini huwa mkubwa sana. Huanzisha shughuli mbalimbali za biashara, kuongoza jumuiya na vikundi vya watu vilivyoko katika maeneo yao, na kushiriki katika asasi mbalimbali za



Kampeni ya Kusoma na Kuandika ya Kha Ri Gude, Afrika Kusini

Juu kushoto: Mvulana akijifunza
Juu kulia: Watu wenye matatizo ya kuona wakijifunza hati ya Braille

Kulia: Watu wakijifunza katika kikundi



kisiasa katika maeneo yao. Na kama wazazi, hutoa msaada bora kwa watoto wao wenye umri wa kwenda shule.

Umuhimu wa kuendeleza na kufundisha lugha za jamii barani Afrika umejidhihirisha pia kupitia jambo lingine. Wahitimu wengi wa vyuo vikuu wenye sifa za hali ya juu hushindwa kupata kazi katika sekta rasmi ya uchumi, ambayo huajiri asilimia 10 tu ya nguvukazi (ILO, 2007). Ujuzi wao wa lugha na maarifa waliyoyapata katika mfumo rasmi wa elimu haviendani na ujuzi wa lugha na uwezo unaohitajika katika miktadha mingine. Hii ni sababu mojawapo kwa nini vijana wengi wa Kiafrika wenye elimu kubwa hukimbilia maeneo ya mjini au ng'ambo.

Uwezo thabiti wa lugha nyingi huendeleza shughuli za kijamii na kiuchumi za kikanda

Uzoefu wa programu za nyongeza za elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi umedhihirisha kwa vitendo kuwa kupata maarifa thabiti kwa lugha ya Kiafrika na kwa lugha rasmi kunaweza kuwa na manufaa sana, kama ilivyo katika programu ya lugha mbili nchini Bukinafaso (Alidou na wenzie, 2008; Ilboudo, 2003). Wajifunzaji katika programu hii wamepata ujuzi thabiti kwa lugha nyingi unaofaa kwa mazingira mbalimbali. Programu hii, kwa makusudi, huunga mkono kuendeleza wajifunzaji kitaaluma. Huitikia shughuli za kijamii na kiuchumi katika eneo hili, hujumuisha mafunzo ya kitaaluma, na huwapa wajifunzaji fursa ya kazi za ufundi, za utaalumu, au za elimu ya juu.

Elimu fanisi kwa lugha-mama na lugha nyingi hufunza ustadi wa lugha na mawasiliano unaoendana na shughuli za kiuchumi barani Afrika zinazofanywa kwa kutumia lugha nyingi, ambazo zina sifa ya kuwa na sekta rasmi ya kiuchumi ndogo na sekta isiyo rasmi kubwa. Sekta isiyo rasmi »hutoa 75% ya kazi zilizopo, 80% ya kazi mpya, na karibu 50% ya pato la taifa« (Walther, 2007: 30). Mawasiliano yaliyo mengi katika sekta hii hufanywa kwa lugha za Kiafrika (Djité, 2008). Sekta hii ina kiwango cha juu cha uvumbuzi na ubunifu, hutoa fursa kwa wenye kiwango kidogo cha elimu, hutoa mafunzo kwa vijana walio wengi kwa msaada kidogo sana kutoka katika serikali za kitaifa, na ina mahitaji makubwa sana ya mafunzo ya ufundi na utaalumu (OECD, African Development Bank, 2008; Walther, 2007). Walther alibaini kwamba »inaelekea kama vile hakuna ufahamu kabisa kuhusu aina na viwango vya maarifa vinavyotolewa huko au kazi na biashara mahususi zilizomo katika muundo wake« (2007: 190). Anataja haja ya kuchambua vizuri stadi na taaluma hizi. Ili kuendeleza programu za mafunzo zinazoendana na miktadha ya lugha nyingi, uchambuzi wa aina hiyo huhitaji kutoa mwanga kuhusu uwezo wa lugha na wa mawasiliano uliopo tayari.



Nkonsonkonson

*Pete za mnyororo,
kama alama ya
umoja na mahusiano
ya watu*

**Kushoto: Elimu ya
utaalamu kwa lugha
mbili, Bukinafaso**

**Kulia: Shughuli za
maendeleo vijijini
zilizotanganishwa,
Afrika Kusini**



Matumizi ya lugha nyingi na mawasiliano kama sehemu muhimu ya maendeleo ya kiuchumi

Katika zama hizi ambazo shughuli za kiuchumi hutumia maarifa, upatikanaji wa habari, maarifa na tekinolojia kwa umma wa watu ni jambo muhimu kwa ustawi wa jumla na una matokeo ya wazi katika kukuza demokrasia. Lugha za Kiafrika ndizo lugha zinazotumiwa zaidi katika mipaka ya nchi na nchi na ndani ya nchi mbalimbali. Hata hivyo, katika nchi nyingi, lugha hizi kwa sasa hupuuzwa na mfumo rasmi wa elimu na magazeti, vyombo viwili ambavyo ni muhimu katika kubuni shughuli za uchumi zinazotumia maarifa, na vinavyoweza upatikanaji wa taarifa, maarifa, na tekinolojia. Elimu itolewayo kwa lugha nyingi huleta mahitaji, mathalani, ya upatikanaji wa taarifa katika lugha husika (Okech, 2002) na hivyo basi huweka msingi wa ushiriki wenye nguvu.

Moyo wa kupenda lugha za Kiafrika umechukua sura mpya, mathalani, katika sekta ya tekinolojia ya habari. Makampuni ya kimataifa kama vile Microsoft yamebaini kwamba kuwekeza katika lugha za Kiafrika ni jambo lenye manufaa kwani yanataka kuwafikia watu milioni 100 wanaozungumza Kiswahili waishio katika nchi sita barani Afrika. Suala hili kuhusu lugha ya Kiswahili linaonyesha kuwa sekta ya biashara huunda istilahi kwa njia isiyo rasmi pindi zinapohitajika. Makampuni yanayochapisha magazeti na yale ya simu za mkononi huwasiliana na wateja wao kuhusu tekinolojia ya kompyuta na mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili na programu za kompyuta hutengenezwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Zaidi ya hayo, wateja hupeva taarifa mbalimbali kwa lugha mbili.

Ensaiklopedia ya Wikipedia iliyoko katika mtandao wa intaneti, ambayo watumiaji wake wanaweza kuichangia maarifa, itatengenezwa kwa kutumia lugha 200, zikiwemo lugha za Kiafrika. Toleo la lugha ya Kiswahili tayari limo mtandaoni (sw.wikipedia.org/). Aidha, UNESCO ina programu maalumu inayoweza matumizi ya lugha nyingi katika njia ya kielektroniki ya mitandao ya kompyuta kuwa jambo linaloweza (www.unesco.org/webworld/multilingualism, Diki-Kidiri, 2007).

Dondoo kutoka *Microsoft, Global Strategic Alliance,* »Unlimited Potential Engagement in Africa« 2007: Local Language Programme

Mojawapo ya vipengele muhimu katika kutumia tekinolojia ya habari na mawasiliano na kukuza maarifa ni kuwa na tekinolojia inayopatikana katika lugha enyeji. Tumetengeneza kifurushi cha lugha kinachobadili programu za Windows na Office kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha enyeji. Kwa sasa kifurushi hicho kinajumuisha lugha ya Kiswahili, Kiafrikana, Kizulu, Kisotho, na Kitswana na huduma hiyo itawafikia watu milioni 150. Watu zaidi ya milioni 100 huzungumza Kiswahili. Kupitia katika Programu ya Lugha Enyeji, zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wa Afrika Mashariki watapata fursa ya kutumia kompyuta kwa Kiswahili.

Aidha, tunashughulikia lugha kwa ajili ya watu wa nchini Ethiopia (Kiamhariki), Rwanda (Kinyarwanda), Nijeria (Kihausa, Kiigbo, na Kiyoruba), na Senegali (Kiwolofu). Pindi programu ya Windows Vista na ile ya Office 2007 zitakapozinduliwa, zitatumia pia lugha za Kiafrika kama Kiswahili, Kiamhariki, Kinyarwanda, Kiyoruba, Kiigbo, Kihausa, Kiwolofu, Kimalagasi, Kizulu, Kiafrikana, Kixhosa, Kisotho, Kileboa, na Kitswana.



Kituo cha mafunzo ya kompyuta, Msumbiji

Lugha na mawasiliano ndio msingi wa uchumi: mfano wa tasnia ya lugha na sekta ya ubunifu

Sifa kuu ya tasnia ya lugha na sekta ya ubunifu ni kwamba huduma zake humhitaji mtu kuwa na maarifa changamani ya lugha na ya mawasiliano. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa kwamba tasnia ya ubunifu na tasnia ya lugha hunufaika na elimu ya msingi kwa lugha-mama na lugha mbili au zaidi kama masomo ambayo hulenga kumpa mtu ujuzi wa hali ya juu wa lugha zinazoendana na miktadha anuwai ya kijamii. Sekta ya ubunifu imefungamana sana na masoko ya eneo na ya ukanda husika na vilevile huzalisha kwa ajili ya kuuza nchi za nje. Masoko haya yana sifa ya kuendeshwa kwa lugha tofautitofauti ambapo lugha za Kiafrika huendana sana na mazingira waliyomo wazalishaji na watumiaji wa Kiafrika. Hivyo basi, inawezekana kwamba kuimarisha stadi za lugha nyingi za watu barani Afrika na kuikubali hali halisi ya kuwepo lugha tofautitofauti miongoni mwa watu barani Afrika kutaeneza na kuongeza ubora wa tasnia hizi mbili (Busch, 2004).

Tasnia ya lugha na sekta ya ubunifu ni masoko ya kazi yenye faida na umuhimu. Kwa bahati mbaya, hakuna tafiti pana zinazofahamika za tasnia ya lugha na tasnia ya ubunifu katika nchi za Afrika. Hili si jambo la ajabu, hata nje ya Afrika. Duniani, utafiti wa kiuchumi katika tasnia ya lugha na tasnia ya ubunifu ni suala geni kiasi. Mnamo mwaka 2005, Kanada, nchi iliyoendelea kiviwanda na yenye lugha rasmi mbili, ilifanya utafiti wa kwanza katika tasnia ya lugha ikianza na shughuli za makampuni ya kiwango kidogo na cha kati katika sekta ya utafsiri, ukalimani, na mafunzo ya lugha (Industry Canada, 2006). Tasnia ya lugha nchini Kanada hutoa huduma kama vile mafunzo ya lugha, mitihani ya kupima ustadi wa lugha, utafsiri, ukalimani, uwekaji sauti za lugha nyingine katika filamu, uhariri na uandishi, usahihishaji profu, uendelezaji wa teknolojia ya lugha, na uendelezaji wa istilahi. Kwa jumla, makampuni haya yalifanya mauzo yaliyofikia dola milioni 404.1 za Kanada ikiwa ni pamoja na riba na gawio la karibu dola milioni 410 za Kanada. Mauzo ya nje ya nchi yalizalisha karibu asilimia 25 ya mapato yote. Baada ya kupata matokeo haya ya utafiti, idara ya Industry Canada ilihitimisha kwa kusema: »Leo hii, kuliko ilivyopata kutokea huko nyuma, kufanya biashara ya kimataifa kunahitaji kuwasiliana na kufanya makubaliano kwa lugha nyingi« (<http://strategis.ic.gc.ca>). Tasnia ya lugha huweka »madaraja« yanayohakikisha kwamba watu wa jamii-lugha mbalimbali wanaweza kuwasiliana.

Utafiti katika tasnia za ubunifu barani Ulaya (Wiesand, 2005) unaonyesha kuwa makampuni binafsi ya ubunifu yanaonyesha kupiga hatua za kushangaza za maendeleo ya kiuchumi kulinganisha na sekta nyingine (jumla ya thamani ya soko katika nchi 31 za Ulaya ilikadiriwa kuwa zaidi ya bilioni 380, na inaongezeka). Sekta ya ubunifu ni soko muhimu la kazi ambamo watu zaidi ya milioni 4.7 wameajiriwa kwa manufaa katika nchi 31 za Ulaya. Mtaji mkuu wa watu wanaofanya kazi katika sekta hii ni ubunifu wao na maarifa waliyo nayo. Sekta hii ina sifa za kuwa na nguvu ndogo ya mtaji ikilinganishwa na sekta nyingine; makampuni yaliyo mengi hufanya biashara za kiwango kiduchu hadi kidogo.



Msusyidie

»Kiondoacho uovu«
Utakatifu, bahati njema

Utafiti wa hivi karibuni kuhusu filamu duniani (UIS, 2009) unaonyesha kuwa Nijeria ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na tasnia kubwa zaidi ya filamu. Kigezo muhimu cha mafanikio yake hayo ni matumizi ya lugha nyingi. Karibu 56% ya filamu zake hutolewa kwa lugha za Kiafrika. Mwaka 2006, lugha kuu nne katika utayarishaji wa filamu nchini Nijeria zilikuwa ni Kiyoruba (31%), Kihausa (24%), Kiigbo (1%), na Kiingereza (44%).

Maono ya jamii na mfumo wa taifa unaoshirikisha raslimali zote

Hali ya kuwepo lugha na tamaduni tofautitofauti miongoni mwa watu siyo tishio halisi na inaweza kusimamiwa ili kuleta manufaa kwa nchi nzima. Djité (2008), mathalani, anazungumzia umuhimu wa hali hiyo kwa maendeleo kwa maeneo ya afya, elimu, utawala, na uchumi. Kila nchi inaweza kujifunza kutoka kwa nchi nyingine lakini haina budi kuweka mikakati yake yenyewe kwa kuzingatia raslimali zake na maono yake.

Kwa msingi huo, mfumo wa elimu itolewayo kwa lugha nyingi utakuwa sehemu ya maono mapana zaidi ya kijamii inayolenga, miongoni mwa mambo mengine, kujenga mfumo madhubuti wa kiuchumi ili kuhakikisha kuwa nchi za Kiafrika zinakuwa na uwezo wa kushindana. Je, kwa nini lugha na elimu zisioongoze katika kuwaandaa wananchi kwa ajili hiyo? Hata hivyo, »ikiwa tatizo la kubainisha hadhi ya lugha za Kiafrika halitashughulikiwa kikamilifu, matumizi ya lugha hizi katika mifumo ya elimu yatagonga mwamba« (Ouedraogo, 2002: 4). Muundo wenye thawabu utakuwa wa muhimu sana katika kukubalika kwa sera za aina hiyo na utarahisisha ujifunzaji wa lugha wa taifa. Matumizi ya lugha nyingi, mathalani, yanaweza kuwa kigezo kimojawapo cha sifa ya kitaaluma na cha kumpandisha mtu hadhi kitaaluma na vilevile kuwa fahari ya taifa.



Kushoto: Riwaya ambazo zimetumiwa kutayarisha filamu, na filamu zilizozaa riwaya, Nijeria

Ukurasa unaofuata: Waafar wakijifunza darasani, Ethiopia




2. Uwezekano wa kutumia lugha za Kiafrika katika elimu

Tatizo

Lugha za Kiafrika si za kisasa; zinahitaji muda na gharama kubwa mno kuendelezwa

Kwa sasa, karibu lugha 200 za Kiafrika hutumiwa katika shule barani Afrika, kwa kiasi kikubwa katika madarasa ya awali ya shule za msingi. Lugha chache za Kiafrika hufundishwa pia katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Ingawa mifano hii inaonyesha kwamba lugha za Kiafrika zinaweza kutumiwa kama lugha nyingine yoyote katika mfumo rasmi wa elimu katika ngazi zote, bado kuna mashaka kama kweli zinafaa kwa elimu ya mfumo rasmi.

Pamoja na imani hii iliyozeleka, inatarajiwa kwamba hata kama mtu atataka kutangamanisha zaidi lugha za Kiafrika katika mfumo rasmi wa shule, atahitaji muda mwingi mno na raslimali nyingi mno kuendeleza msamiati wa lugha hizi, kufunza waalimu, na vilevile kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.



21

Majibu

Utafiti wa lugha za Kiafrika na uendelezaji wa lugha kwa ajili ya elimu barani Afrika (tazama mifano chini) hata hivyo unaonyesha kwamba mashaka haya hayana sababu za msingi. Badala yake, lugha za Kiafrika ni hazina ambazo bado hazijagunduliwa, kuthaminiwa, na kutumiwa kikamilifu.

Funtunfunefu

Denkyemfunefu

»Mamba wa Kisiam«
Demokrasia, umoja
miongoni mwa watu
wenye tofauti mbalim-
bali



Kanuni kuu ya kuendelea kwa lugha ni kwamba lugha huendelea kwa kutumiwa. Kwa hiyo, kila lugha inaweza kutumiwa kwa kusudi lolote. Kila lugha inaweza kubadilika ili kuendana na mazingira fulani kama walivyo wazungumzaji wake. Hivyo basi, lugha za Kiafrika zinaweza kutumiwa kama lugha za kutolea elimu hadi mwisho wa elimu ya chuo kikuu. Nchini Mali, kwa mfano, profesa mmoja mchapakazi hufundisha fizikia na kemia kwa lugha ya Bamana. Kiufundi, inawezekana kwa lugha zote za Kiafrika kutumiwa kutoa mihadhara ya kitaaluma katika ngazi hii. Mifano ya ufundi wa lugha imejaa tele barani Afrika kama inavyoonyeshwa na historia ya Afrika: kuna mradi wa »Six Year Primary Project« nchini Nijeria, mradi wa »Formation Supérieure des néo-alphabètes« (ulioanzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1980 nchini Mali ili kutoa mafunzo ya kiufundi na kuandaa vitabu katika lugha 12 hivi), na kazi za watafiti, wachapishaji, kamati za lugha na vyama vingine chungu nzima (tazama Kiambatisho 3). Yote haya ni ushahidi unaoonyesha nguvu na uwezo wa lugha enyeji kutumiwa kama lugha ya kufundishia na utafiti katika sayansi, tekinolojia, na kadhalika.

Kustawisha maarifa yaliyopo ya kisayansi ya kimataifa kupitia utafiti wa kiisimu barani Afrika

Vidunda, lugha moja ndogo ya nchini Tanzania, inatoa ushahidi kwamba hatuna budi kuwa waangalifu na madaai kwamba lugha (na tamaduni) za Kiafrika zina thamani ya chini kulinganisha na lugha (na tamaduni) nyingine yoyote. Mradi wa utafiti wa kiisimu kuhusu istilahi za kibiolojia katika lugha ya Vidunda ulibaini kuwepo kwa utajiri wa kuvutia wa majina ya miti pori na maarifa kuhusu matumizi yake, jambo ambalo limestawisha maarifa yaliyopo ya sayansi ya muundo wa mimea (Légère, 2004).



Kushoto: Uuzaji wa bidhaa zinazotengezwa katika eneo husika, Uganda

Chini: Tangazo likielekeza kwa lugha ya Kiganda namna ya kutumia dawa ya malaria, Uganda

OMUSUJJA GW'ENSIRI GUTTA BWEGUBA TEGUJANJABIDWA MANGU ATE MUBUTUUFU

Janjaha omusujja gw'ensiri naga akazesa amakerenda aga kulobokwini (Chloroquine).

Enkazesa eri bweti:

Emyaka	Dunaka Oluseeka	Dunaka Ol'wukulu	Duneta akwawerere	Anakerenda guma namu.
Emyaka ebiri okukula ku Mwaka guma	0	0	0	1%
Emyaka Ebiri okukula ku myaka asatu	1	1	1	2%
Emyaka atia okukula ku myaka asano	1	1	1	3%
Emyaka mubwaga okukula ku myaka mubwaga	1	1	1	4%
Emyaka mubwaga okukula ku myaka kumi	2	2	1	5%
Emyaka kumbwaga okukula ku myaka kumi n'waaani	3	2	1	7%
Emyaka kumi n'waaani okukula wagufo	4	4	2	10%

Jukira nti singa omusujja teguwona mu naku satu genda mu dawatiro eri kuli okumpi.

Bikiywidwa aba Mpiigi Community Based Health Carr. (CBHC) Project, P.O. Box 111 Mpiigi, Esisima

OMUSUJJA GW'ENSIRI

Gutta, naye gwayinza ukuziyalibwa

Okuziyala Omusujja Gw'ensiri:

Okuziyala okuziyala eriri okukubwona naga okula bima

- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo

Ziyala omusujja gw'ensiri naga okula bima

- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo

Okuziyala omusujja gw'ensiri:

- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo
- Okuziyala okuziyala n'wawo n'wawo n'wawo

Jukira: Omusujja gw'ensiri naga okuziyala bima, n'obujajabi okuziyala guma gwa kabi naye.

Bikiywidwa aba Mpiigi Community Based Health Carr.



Vitabu vya habari za kubuniwa na visivyo vya habari za kubuniwa vilivyoandikwa kwa lugha ya Kipulaari, Senegali

Uendelezaji wa lugha kitaifa na baina ya mataifa kupitia sekta ya uchapishaji: mfano kutoka Senegali

Nchini Senegali, kuna mashirika mengi yanayochapisha kazi zenye habari za kubuniwa na zisizo za kubuniwa katika lugha mbalimbali za taifa. Mojawapo ya mashirika hayo, Associates in Research and Education for Development (ARED), huchapisha hususani katika lugha ya Kipulaari (au Kifulfulde), lakini si katika lugha hii pekee, ili kuleta heshima kwa jamii ya wazungumzaji wa Kipulaari na kukidhi mahitaji ya maandiko katika lugha ya Kipulaari. Tangu lilipoanzishwa mwaka 1990, shirika hili limechapisha zaidi ya machapisho 150 kwa lugha za Kiafrika, na kuuza zaidi ya vitabu 800,000, vingi kati ya hivyo vikiwa ni vitabu vya riwaya. Lengo la ARED ni kwenda mbali zaidi ya kutayarisha vifaa vya mafunzo ya msingi ya kusoma na kuandika kwa kuchapisha vifaa changamani sana vinavyohusu masuala muhimu kwa jamii hii. Vifaa huandikwa katika lugha ya Kipulaari kwanza ili kuweza kuamua iwapo vinakidhi mahitaji na viwango vya wasomi wapya au la. Uchapishaji baina ya mataifa hufanywa pindi vifaa vinapokuwa vimeandaliwa tayari kwa lugha ya Kipulaari. Vifaa hivi huwekwa katika lahaja nyingine za Kifulfulde, lugha nyingine za Afrika Magharibi, au kutafsiriwa katika Kifaransa. Vitabu vya ARED hutumiwa katika programu zinazoendeshwa na mashirika ya eneo hilo, mashirika yasiyo ya kiserikali, na miradi ya pande mbili nchini Senegali, Mali, Benini, Bukinafaso, na Nijeri.

Kuendeleza lugha kwa ajili ya elimu shuleni hukutumii muda mwingi tofauti na inavyodaiwa mara kwa mara, kama inavyoonyeshwa nchini Somalia:

Kisomali kama lugha ya kufundishia hadi mwaka wa 12, Somalia

Kwa miaka tisa tu, lugha ya Kisomali ilisanifishwa, ikaundiwa alfabeti rasmi kwa kutumia hati ya Kilatini, istilahi zake zikaongezwa kwa ajili ya elimu rasmi, na ikatumiwa kama lugha ya kufundishia hadi mwaka wa 12 katika mfumo rasmi wa elimu. Masomo ya awali katika ngazi ya elimu ya juu yaliandaliwa kwa Kisomali. Kuzuka kwa vita ya wenyewe kwa wenyewe mwaka 1986 ndicho kitu pekee kilichosimamisha mchakato huu.

Mfano wa lugha ya Kisomali unaonyesha kwamba sera thabiti ya lugha na elimu na imani kwamba ni jambo la kawaida kutumia lugha za Kiafrika katika nyanja zote za maisha ndizo sababu kuu za mafanikio (Griefenow-Mewis, 2004).

Mifano ya uendelezaji lugha iliyotajwa hapo juu inasisitiza ukweli kwamba mawasiliano ya kielimu na kitaaluma huweza kufanywa kwa kutumia lugha maalumu za kiufundi ambazo hubadilika wakati wote. Hivyo basi, uundaji wa tahajia za lugha kwa ajili ya elimu ya msingi na madarasa ya kujifunza kusoma na kuandika ni mwanzo tu na haupaswi kuchanganywa na uendelezaji lugha (Faye, 2006). Zaidi ya hayo, mfano kutoka nchini Somalia unaonyesha kwamba inawezekana kufanya mabadiliko ya lugha katika mfumo rasmi wa elimu kwa muda mfupi tu.



Duafu

*Chanuo la mbao
Uvumilivu, upendo,
uangalifu*

3. Jinsi ya kusimamia kwa ufanisi hali halisi ya lugha nyingi katika elimu kwa wote kwa maisha yote

Tatizo

Barani Afrika kuna lugha nyingi mno; hivyo basi, shule hazina budi kusisitiza lugha rasmi


Watunga sera wengi hukutana na changamoto katika kuchagua lugha ipi itumiwe kufundishia. Mojawapo ya hofu kuu za watunga sera, wazazi, na watu wengine wanaohusika ni kwamba elimu kwa lugha-mama itasababisha lugha rasmi kuondolewa katika mtaala wa shule, jambo ambalo litaathiri kwelikweli ujifunzaji wake na utumiaji wake. Kwa hakika, shule ndipo mahali ambapo wanafunzi walio wengi hujifunzia lugha rasmi. Inakadiriwa, kutegemeana na nchi na ukanda husika, kwamba asilimia 5 hadi 15 tu ya wanafunzi ndio hujua lugha rasmi ya kimataifa kabla ya kuanza shule.

Majibu

Kutafiti na kuelewa hali halisi ya matumizi ya lugha

Hapa duniani hakuna nchi yoyote ambayo watu wake wote hutumia lugha moja tu. Badala yake, kwa kuzingatia hali hii ya kuwepo kwa lugha nyingi, matumizi ya lugha nyingi ndiyo kawaida. Hata katika miktadha ambayo watu huonekana kama wenye kutumia lugha moja, kuna tofauti za kilahaja au za kirejesta. Nchi nyingi haziendelezi uelewa wa matumizi ya lugha nyingi, haziendoi mkanganyiko au wasiwasi au kufanya uchunguzi wa hatua kwa hatua au utafiti unaoweza kuwapa watu taarifa kuhusu hali ya matumizi ya lugha nyingi kwa raia wake, matumizi ya lugha mbalimbali katika nyanja mbalimbali za jamii na mgawanyo wa lugha mbalimbali katika ngazi ya eneo, ukanda, taifa na katika maeneo yanayotambuka mipaka ya nchi na nchi. Utafiti wa aina hiyo utapunguza hisia kwamba matumizi ya lugha nyingi ni vurugu isiyoweza kudhibitiwa.

Uchunguzi wa hazina za lugha za Wabanyuku, Senegali



Georges (miaka 26)

Kibanyuku Gubaheri
Kijoola Bandiali
Kiwolofu
Kifaransa
(Kibayoti)
(Kijoola Kaasa)

Vincent (miaka 3)

(Kibanyuku Gubaheri)
(Kiwolofu)

Edouard (miaka 14)

Kibanyuku Gubaheri
Kijoola Kujirerai
Kiwolofu
Kifaransa

Hortance (miaka 47)

Kibanyuku Gubaheri
Kijoola Kujirerai
Kiwolofu
Kifaransa
Kikirioli
(Kibayoti)
(Kijoola Fonyi)

Kuweka muundo wa matumizi ya lugha barani Afrika

Ujuzi wa lugha nyingi ni sifa waliyo nayo Waafrika wengi na jamii zao vile vile. Katika muktadha wa aina hiyo, watu wanaojua lugha moja tu hawawezi kushiriki wala kuwasiliana kwa ufanisi katika mazingira yote ya jamii. Mawasiliano kwa njia ya mdomo na maandishi katika nchi za Afrika yanaweza kuwekwa katika matabaka msonge yanayofikia matano, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo hapo chini. Hebu chukua mfano wa mawasiliano ya kisiasa. Katika ngazi ya kitaifa na kimataifa, lugha iliyo muhimu sana ni lugha rasmi, lakini katika ngazi ya kanda na chini yake, lugha muhimu ni zile zinazozungumzwa katika ukanda na maeneo husika. Je, mfumo wa elimu unaweza vipi kukidhi mahitaji haya kama hautaki kuweka mipaka ya matumizi ya lugha katika ngazi mbalimbali?

Modeli za lugha tatu zinaweza kuwa chaguo zuri mbadala la kuleta mawasiliano baina ya ngazi mbalimbali katika maeneo mengi. Chaguo hili halina budi kuendelezwa na mtaala wa elimu.



Chanzo: Wolff, 2006; kimerekebishwa kutoka Obanya, 1999

Elimu haina budi kuleta mshikamano katika jamii

Modeli iliyo bora ya lugha za kufundishia haina budi kuakisi hali halisi tofautitofauti za lugha zilizopo katika nchi ili kuhusisha ngazi zote za jamii na kufanikisha mawasiliano, kupeana maarifa, uwezo na utajiri, na kuleta utawala wa kidemokrasia na ulio shirikishi. Kwa sasa, pengo la mawasiliano kati ya wazungumzaji wa lugha enyeji na wale wa lugha rasmi na ya kimataifa ni kubwa mno, jambo linaloongeza mgawanyiko katika jamii, dhana ya umbali na hisia za kunyimwa haki na kutengwa. Badala ya kuleta mshikamano panapo tofauti, mfumo wa elimu shuleni ni taasisi muhimu ya kijamii ambayo huendeleza vikwazo kwa sababu hutegemea mno lugha rasmi, huku ikiing'ang'ania kama kipimo kisichoakisi miundo ya lugha inayotumiwa na watu walio wengi katika maisha yao ya kila siku.



Dwanimen

Pembe za kondoo dume
Nguvu na unyenyekevu

Ujifunzaji wa lugha katika miktadha ya lugha nyingi unaweza kuwa mchakato muhimu uleto mshikamano. Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni zaidi kuhusu ujifunzaji lugha katika miktadha ya lugha nyingi (Ouane, 2009; Cummins, 2008; Jessner, 2008; Bamgbose, 2000), lugha hazipaswi kutenganishwa, bali zinapaswa kukaribiana ili wajifunzaji waweze kukuza utambuzi wao wa lugha, kujifunza lugha kadhaa na tamaduni zake kwa wakati uleule, kuelewa ukamilishani uliopo baina ya lugha na tamaduni zilizo jirani, na kuweza kuwasiliana kwa uhodari katika mazingira ya lugha nyingi.

Uchaguzi wa lugha kupitia makubaliano ya kijamii: mfano kutoka Bukinafaso

Nchini Bukinafaso, ambako kuna lugha zipatazo 59, Wabukinabe walio wengi huzungumza lugha zisizopungua mbili, na asilimia 90 ya watu huzungumza walau lugha moja kati ya lugha kumi na nne zinazozungumzwa zaidi. Katika programu ya lugha mbili (inayoendeshwa na Wizara ya Elimu ya Msingi na Œuvre suisse d'entraide ouvrière (OSEO), jumla ya lugha nane za kitaifa hutumiwa. Kati ya hizo zote, hakuna hata lugha moja ambayo serikali iliamuru itumiwe. Uchaguzi wake ulifanywa kutokana na mchakato wa makubaliano miongoni mwa jamii mbalimbali na vyama vya wazazi ambapo hao ndio waliochagua lugha inayozungumzwa zaidi na kueleweka zaidi kwa watu katika maeneo yao ya vijiji au mijini na kufanywa kuwa lugha ya kufundishia (Alidou na wenzie, 2008). Mchakato wa makubaliano katika jamii unahitaji kuendana na mtazamo walio nao watu wengi ambao wanaweza kuunga mkono kufanywa kwa maamuzi eledi kwa kutumia taarifa zenye ushahidi wa karibuni zaidi kuhusu elimu itolewayo kwa lugha nyingi, mafunzo ya kusoma na kuandika, na ujifunzaji lugha utotoni na katika umri mkubwa.

Kila raia ana haki ya kujifunza lugha rasmi

Mfumo wa elimu shuleni na mifumo rasmi ya utoaji mafunzo inayofuatia huwaandaa wajifunzaji kuingia katika sehemu zenye faida zaidi katika soko la kazi. Huko, huhitajika ujuzi mkubwa wa lugha rasmi, ambayo ni lugha ya kimataifa, lugha inayochukuliwa kuwa »hutoa fursa zaidi«. Hivyo basi, ujifunzaji wa lugha rasmi ni jambo muhimu sana na raia wote wana haki ya kuelewa lugha rasmi, lugha inayotumiwa kwa masuala ya kitaifa. Umuhimu huo huongezeka zaidi ikiwa lugha hii rasmi vilevile ni lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano. Ujifunzaji wa lugha hiyo ya kimataifa hauna budi kufanyika katika misingi sawa na ile ya ujifunzaji wa lugha rasmi isiyokuwa na hadhi ya kimataifa.

Tunasisitiza sana elimu thabiti kwa lugha nyingi itolewayo kwa kutumia modeli kawizi au modeli za nyongeza, inayoshughulikia kikamilifu hali halisi ya matumizi ya lugha nyingi na kumsaidia kila raia aweze kuwasiliana kwa ustadi katika ngazi ya eneo husika, kikanda, kitaifa, na kimataifa kwa kutumia lugha kuu zinazohusika. Hivyo basi, elimu itolewayo kwa lugha mbili au kwa lugha nyingi barani Afrika haiwezi kumaanisha kuwa ni kutumiwa kwa lugha-mama au lugha rasmi (ambayo mara nyingi ni lugha ya kimataifa); ni lazima imaanishe kuwa ni kutumiwa kwa lugha-mama au lugha nyingine yoyote ya kwanza iliyochaguliwa kwa hiari pamoja na lugha rasmi ya kimataifa. Utaratibu wa aina hii, unaozingatia maadili ya lugha nyingi, husimamia hali ya kawaida ya matumizi ya lugha nyingi na unakubaliana na malengo ya »Elimu kwa Wote«.

4. Kwa nini kufundisha kwa lugha-mama hunufaisha utendaji wa wanafunzi

Tatizo

Muda finyu unaotolewa kwa ufundishaji katika lugha za kimataifa zenye wigo mpana wa mawasiliano utasababisha wajifunzaji kuwa na kiwango cha chini cha umilisi na ufanisi katika lugha hizi

Inaelekea kuwa wazi kwamba lugha ambayo haikuzoeleka hujifunzwa vizuri zaidi pindi mjifunzaji anapokutana nayo kwa muda mwingi zaidi. Hivyo basi, watu wengi huunga mkono dhana kwamba mtoto hana budi kujifunza lugha ya pili mapema zaidi na kwa nguvu zaidi kadiri iwezekanavyo. Katika hali ya kufikirika, mtoto hana budi »kuzamishwa« katika lugha hiyo. Kwa mtazamo huu, inaelekea hakuna kipingamizi pindi ufundishaji shuleni unapofanywa mapema iwezekanavyo kwa kutumia lugha ya pili, ambayo kwa kawaida huwa haikuzoeleka. Hata hivyo, dhana iliyopo ni kwamba mtoto huyu huwa tayari amepata au wakati uleule huendelea kupata maarifa ya msingi katika lugha ya (/za) kwanza inayojulikana. Shule nyingi za kimataifa hutumia mkabala wa uzamishaji. Hata hivyo, wanafunzi wanaosoma katika shule hizi hutoka katika familia tajiri na huanza shule huku tayari wakiwa na msingi mzuri kielimu.



27

Obi nka obie

»Msiumane«

Alama ya umoja, amani,
na mapatano

Majibu

»Elimu kwa Wote« ni utekelezaji wa haki za kidemokrasia kwa raia wote na ni msingi wa maendeleo ya kijamii na ushirikishwaji, na ndilo lengo la serikali zote zinazounga mkono vuguvugu la »Elimu kwa Wote«. Kwa hiyo, mkabala maalumu wa uzamishaji, yaani kutumia lugha ya pili, ambayo ni lugha ya kigeni, kama lugha ya kufundishia, hauwezi kuwa mkabala wa kutumiwa katika mfumo wa elimu unaotumiwa na wengi.

Matokeo ya kuridhisha ya tafiti za tathmini: mfano kutoka Ethiopia

Sera ya elimu nchini Ethiopia inatamka kwamba lugha-mama haina budi kutumiwa kama lugha ya kufundishia kwa miaka minane ya kwanza shuleni. Katika mfumo wa elimu ambao umetoa madaraka mikoani nchini Ethiopia, baadhi ya mikoa hutumia kanuni hii na mingine, kama vile mji mkuu, Addis Ababa, huanza kutumia lugha ya kigeni, yaani Kiingereza, kama lugha ya kufundishia katika mwaka wa sita tu. Ulinganishi wa mafanikio ya ujifunzaji katika mwaka wa nane ulionyesha kwamba wanafunzi wenye elimu thabiti kwa lugha-mama walifanya vizuri zaidi katika masomo yote, likiwemo somo la Kiingereza (Heugh na wenzie, 2007). Ili kudhoofisha umuhimu wa matokeo haya, inaweza kudaiwa kwamba kila jaribio ni la pekee na huzingatia mlolongo wa vigezo. Lakini, vyovyote iwavyo, kama matokeo haya hayatoi ushahidi madhubuti unaounga mkono modeli kawizi kwa lugha za kwanza, basi huondoa hofu inayoelezwa na wale wanaodai vinginevyo.

Ustadi wa lugha ya kitaaluma ni maalumu sana na uletao changamoto

Tunapojadili kuhusu matumizi ya lugha shuleni, tunahitaji kutambua aina maalumu sana za matumizi ya lugha ambayo hujifunzwa na huhitajika katika miktadha ya shuleni. Elimu itolewayo shuleni hupatikana kwa kujifunza na kutumia dhana dhahania kupitia katika lugha ya maandishi na ya mazungumzo darasani. Hivyo basi, ujifunzaji lugha hufanyika kupitia katika masomo yote, si kupitia katika masomo ya lugha pekee. Dhana dhahania zaidi ambazo hujifunzwa kwa kujifunza lugha huonyesha jinsi lugha ya kwanza ilivyo ya msingi. Shule hazina budi kuendeleza ujuzi na ubingwa wa lugha ya (/za) kwanza kwa kuwa lugha hujifunzwa kupitia masomo yote, si kupitia masomo ya lugha pekee.

Utafiti wa kimataifa unaonyesha kwamba wanafunzi hujifunza haraka ujuzi wa kufanya mazungumzo mepesi katika lugha ngeni, yaani, ndani ya mwaka mmoja au miwili.

Hata hivyo, hata katika mazingira yenye vifaa kemkem vya kujifunzia, huchukua miaka isiyopungua sita kujifunza maarifa dhahania ya lugha ya kitaaluma ambayo kwa kawaida hutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji (Alidou na wenzie, 2006; Cummins, 2000).

Ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia huleta matatizo ya mawasiliano katika madarasa mengi

Katika nchi nyingi za Kiafrika, waalimu wanatarajiwa kuwafundisha wanafunzi kusoma na kuandika katika lugha ambayo (a) haikuzoeleka kwa wanafunzi na (b) wao wenyewe wana ujuzi mdogo wa kuitumia kufundishia. Hivyo basi, waalimu na wanafunzi katika madarasa ya nchi za Kiafrika hukabiliwa na matatizo makubwa ya mawasiliano na ujifunzaji siku hadi siku.

Mfano ufuatao unaonyesha jinsi elimu inavyoweza kutolewa kwa lugha ambayo waalimu wanaweza kuitumia kwa ustadi kufundishia. Ikiwa waalimu watawafundisha wanafunzi kwa lugha ya kigeni, ni sharti wapate elimu kuhusu namna ya kufundisha na kujifunza katika lugha ya pili. Macdonald (1990) alibaini kwamba kufanya mabadiliko kutoka lugha moja ya kufundishia hadi nyingine katika mwaka wa tano kulisababisha kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaoacha shule au kurudia darasa mwishoni mwa mwaka wa tano. Mbali ya kuwepo matatizo kama vile kukosa ada ya shule, kwa ufupi ni kwamba wanafunzi hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha ya kigeni iliyotumiwa kufundishia. Pindi wanafunzi wa mwaka wa tano walipobadilishiwa lugha ya kufundishia kutoka Kitswana kwenda Kiingereza mwanzoni mwa mwaka wa tano, walikuwa na ufahamu wa maneno 800 tu ya Kiingereza, lakini walihitaji kufahamu maneno 7,000 ili waweze kuelewa mtaala wa mwaka wa tano. Waalimu wanautambua ukweli huu, hivyo mara nyingi hutumia lugha iliyozoeleka. Hata hivyo, mfumo wa elimu hautaki kubadilika ili kuikabili au kuitunuku tabia hii ya kibunifu ili kurekebisha hali hii.



Kibonzo kuhusu matumizi ya lugha darasani, Nijeri

ushirikiano. Mtazamo wa aina hii unaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa wanafunzi na kuwajengea woga wa kujifunza lugha na kujifunza kwa jumla. Ili kuepuka kuaibika mbele ya wenzao, baadhi ya wanafunzi huacha kujitolea kujibu maswali darasani. Tabia hii huonekana zaidi kuwa miongoni mwa wasichana barani Afrika. Wanafunzi wa kike hufanya kila wawezalo kuepuka kudhihakiwa madarasani. Hivyo basi, mara nyingi wasichana huepuka kuzungumza kama lugha ya kufundishia haikuzoeleka kwao« (Alidou na Brock-Utne, 2006: 87).

Wasichana wanaelekea zaidi kushiriki kikamilifu darasani kama lugha ya kufundishia ni lugha enyeji (World Bank, 2000).

Vitendo vya ufundishaji kama vile »mazungumzo salama« huzidisha tatizo la mawasiliano na kutojamini. »Mazungumzo salama« hujionyesha kupitia vitendo kama vile »kuwahimiza wanafunzi kutoa majibu ya kuitikia, kurudia sentensi au maneno ya mwalimu

Ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia una athari hasi kwa ufundishaji na ujifunzaji

Waalimu wengi barani Afrika hawana mafunzo kuhusu namna mtoto mdogo anavyojifunza na kutumia lugha. Ukiongezea ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia wanaokuwa nao, hali hii husababisha matatizo makubwa katika ufundishaji.

»Mara nyingi waalimu huichukulia hali ya wanafunzi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha ya kufundishia kuwa hutokana na tabia ya uvivu, uwezo mdogo kiakili au kutotaka kutoa



Programu ya Elimu
kwa Lugha Mbili,
Bukinafaso

na kunakili notisi kutoka ubaoni» (Rubagumya, 2003: 162). Mazoezi yanayotegemea tu kujifunza kwa kukariri, »mazungumzo salama«, na kurudia kama kasuku maneno ya mwalimu ni mazoezi yasiyoleta ufanisi wa kutosha kwa sababu hayawafundishi wanafunzi jinsi ya kutumia maarifa ya kidhanifu katika taarifa mpya. Mara nyingi mazoezi haya ni ishara ya kuwepo uelewa mdogo au ujuzi mdogo wa lugha miongoni mwa wanafunzi na waalimu. Zaidi ya hayo, mazoezi haya hayaamshi shauku ya wanafunzi ya kutaka kujifunza, tofauti na wanavyokuwa katika michezo, kujumuika pamoja, na shughuli za ufundishaji na ujifunzaji zinazohusisha vitendo.

Mifano inayofuata inaonyesha matokeo chanya katika ujifunzaji na ufundishaji pindi lugha inayotumiwa inapokuwa ni ile iliyozeleka kwa wanafunzi na ambayo waalimu huimudu vyema na hivyo kuwa mfano wa kuigwa katika matumizi ya lugha ya kitaaluma.



Uelewa mzuri wa dhana za kisayansi kwa lugha iliyozeleka

Katika jaribio moja lililofanywa nchini Botswana (Brock-Utne na Alidou, 2006; Prophet na Dow, 1994), seti ya dhana za kisayansi ilifundishwa kwa kikundi cha majaribio cha wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa lugha ya Kitswana na kufundishwa pia kwa kikundi kingine cha kupimia majaribio kwa lugha ya Kiingereza. Kisha wanafunzi walipewa majaribio ili kupima uwezo wao wa kuelewa dhana hizo. Watafiti waligundua kwamba wanafunzi waliofundishwa kwa lugha ya Kitswana walikuwa na uelewa mkubwa zaidi wa dhana hizo kuliko wanafunzi waliofundishwa kwa Kiingereza. Utafiti mwingine unaofanana na huo na uliotoa matokeo sawa na hayo ulifanywa nchini Tanzania. Wanafunzi wa elimu ya sekondari waliofundishwa dhana za kisayansi kwa Kiswahili walifanya vizuri mno kuliko wale waliofundishwa kwa Kiingereza (Mwinsheikhe, 2003).

Matokeo mazuri zaidi katika mitihani na warudaji wachache zaidi

Tabia ya kutathmini maarifa ya wanafunzi katika mitihani kwa kutumia lugha wasiyoimudu ina athari hasi kwenye matokeo ya mitihani na viwango vya kufaulu (Brock-Utne na Alidou, 2006). Katika shule moja ya msingi ya eneo la mjini huko Cape Coast (Afrika Kusini), utafiti ulifanywa ambapo Kiingereza kilitumiwa kama lugha ya kufundishia tangu wanafunzi walipoanza shule (Wilmot, 2003). Lugha ya kufundishia ilipobadilishwa kutoka Kiingereza kwenda lugha-mama ya watoto hawa, utafiti huo ulibaini kwamba wanafunzi hufahamu mambo mengi zaidi na kujifunza vizuri zaidi pindi wanapofundishwa kwa lugha waliyoizea, yaani lugha-mama.

Nchini Ethiopia, uchambuzi wa mafanikio yaliyofikiwa na wanafunzi wa mwaka wa nane kati ya mwaka 2000 na 2004 unaonyesha kwamba »kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika somo la hisabati na masomo ya sayansi ni cha juu mno kwa wale wanaofundishwa kwa lugha-mama kuliko cha wale wanaofundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo haya yanaonyesha kwamba kutumia lugha-mama kama lugha ya kufundishia somo la hisabati na masomo ya sayansi katika madarasa ya juu ya elimu ya msingi (mwaka wa saba na wa nane) kuna athari chanya kwenye viwango vya kufaulu« na »kwamba kuna tofauti ndogo tu ya viwango vya kufaulu katika somo la Kiingereza kati ya wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza na wale wanaojifunza kwa lugha-mama. Hii inaonyesha kwamba kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia hakuleti tofauti kubwa ya alama za wastani za kufaulu katika somo la Kiingereza« (Heugh na wenzie, 2007: 81).

Epa

»U mtumwa wa yule
uliyevaa pingu zake«
Utumwa

Nchini Mali, ambako karibu asilimia 10 ya watoto wa shule ya msingi wako katika madarasa ambayo hutumia lugha ya kwanza kama lugha ya kufundishia; wanafunzi hawa wana uwezekano wa mara tano zaidi wa kutorudia darasa na wana uwezekano wa zaidi ya mara tatu wa kutoacha shule. Matokeo haya ni ya muhimu kwelikweli kwa sababu watoto wanaofundishwa kwa lugha ya kwanza mara nyingi hutoka katika makundi ya watu walio katika mazingira magumu zaidi (World Bank, 2005).

»Programme for International Student Assessment« (PISA) inaonyesha kwamba ujuzi wa lugha ya kufundishia ni kigezo muhimu cha kufanya vizuri shuleni

Programu ya Tathmini ya Wanafunzi wa Kimataifa (PISA, 2006) inathibitisha kwamba ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia, ukiwemo ujuzi mdogo wa kusoma, una athari hasi kwa uwezo wa kufanya vizuri katika masomo yote. Nchini Ujerumani, kwa mfano, wanafunzi dhaifu zaidi hutarajiwa kutoka miongoni mwa wahamiaji ambao nyumbani huzungumza lugha tofauti na ile inayotumiwa shuleni na ambao wazazi wao wana hali ya chini kijamii, kiuchumi, na kitaaluma. Ukilinganisha na wanafunzi walio wengi barani Afrika, wanafunzi wahamiaji nchini Ujerumani hujifunza katika mazingira mazuri zaidi: siku zote huwa katika mazingira ya lugha ya kufundishia wawapo nje ya shule, na hujifunza katika shule zenye vifaa bora na katika mazingira yenye utajiri mwingi zaidi wa watu wenye elimu. Hata hivyo, viwango vyao duni vya kufaulu vinaonyesha kwamba ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia na msaada mdogo wanaoupata nyumbani kwa ajili ya maendeleo yao ya kitaaluma ndizo sababu kuu za kiwango duni cha kufaulu shuleni.

Matumizi ya maarifa katika maisha ya kila siku

Matumizi ya lugha-mama au lugha iliyozoeleka hufanikisha utumiaji wa mazoezi kwa vitendo na ufundishaji unaozingatia mahitaji ya mtoto ambayo huhimiza wajifunzaji kuwa watendaji na kushiriki kikamilifu katika mada za masomo. Programu ya »Ecoles Bilingues« ya nchini Bukinafaso (Alidou na wenzie, 2008; Ilboudo, 2003), »Ecoles de la Pédagogie Convergente« ya nchini Mali (Fomba na wenzie, 2003), na »Zambian Primary Reading Programme« ya nchini Zambia (Sampa, 2005) ni mifano ya programu zenye utaratibu wa aina hiyo (Dembélé na Miaro-II, 2004).

Mifano hii ni ushahidi kwamba shule ni sehemu muafaka kwa jamii yote ikiwa ujifunzaji unafanyika katika lugha iliyozoeleka na inayoendana na mazingira ya kijamii na kiutamaduni, lugha ambayo hutumiwa katika mazingira ya kijamii ya mwanafunzi na ikiwa mtaala ni wenye kujali na kushirikisha (Châtry-Komarek, 2003, 1996). Programu ya »Ecoles Bilingues« nchini Bukinafaso (Ilboudo, 2003) huendesha miradi ya uchumi ambamo wanafunzi hujifunza kuhusu uzalishaji ng'ombe kwa kutangamanisha maarifa ya jadi na njia za kisasa. Mtaala haukugawanywa sana katika sehemu sehemu kwani waalimu huhusisha maudhui yaliyofundishwa katika masomo ya jamii, biolojia, na hisabati katika shughuli hii. Utaratibu huu hufanikiwa kwani ujifunzaji huendana na mazingira ya wanafunzi, nao wazazi hunufaika pia kwani watoto wao huweza hata kujipatia kiasi fulani cha fedha kwa kuuza ng'ombe wanaowazalisha. Mfano huu unaonyesha kwamba kutumia lugha inayofaa, mbinu zinazochangamsha ufundishaji, na mitaala inayoendana na mahitaji halisi ya wanafunzi na jamii yao huboresha ufanisi wa elimu.

Kwa kuhitimisha, njia yenye ufanisi inayoweka misingi imara ya elimu bora barani Afrika ni kutumia, kwa kipindi kisichopungua miaka sita, lugha za kufundishia wanazoelewa waalimu na wanafunzi, kutumia mbinu fanisi za kufundishia katika lugha ya kwanza na ya pili, na kutoa mitaala inayoendana na hali ya kijamii na kiutamaduni ili ujifunzaji shuleni uweze kuhusiana na mahitaji ya wajifunzaji na kuleta manufaa maishani mwao wamalizapo shule.

5. Aina gani za modeli za lugha zina mafanikio makubwa Afrika?

Tatizo

Je, kiasi gani cha lugha-mama huhitajika?

Mwaka 2005, timu ya wataalamu bingwa (Alidou na wenzie, 2006), ikifanya kazi kwa agizo la UNESCO Institute for Education (UIE) – sasa UNESCO Institute for Lifelong Learning (UIL) – na ADEA, ilipitia upya programu za elimu barani Afrika na utangamanishaji wa lugha-mama katika mtaala wa elimu. Mapitio hayo yaliyojumuishia nchi 25 na kutumia matokeo ya tafiti na majaribio yaliyofanywa katika kipindi cha miaka 45 iliyopita yanaonyesha kwamba lugha za Kiafrika katika nchi zilizo nyingi hupewa nafasi ndogo katika mifumo ya elimu inayotumiwa na watu wengi. Programu za majaribio za lugha mbili si miongoni mwa programu hizo, lakini kwa kawaida hufuata modeli ya kuwahi kuacha lugha-mama, na kuanza kutumia lugha rasmi baada ya mwaka mmoja hadi minne ya kupata elimu kwa lugha-mama. Upungufu huu (wa kuacha mapema lugha-mama) unaweza kutokana na sababu za kisiasa, pamoja na dhana kwamba lugha-mama ni ya kujifunzia hatua za awali tu; hata hivyo, hakuna ushahidi wa kisayansi kuhalalisha kuwahi kuacha lugha-mama ingawa hii ni hatua kubwa ya maendeleo ikilinganishwa na wale wanaoanza matumizi ya moja kwa moja ya lugha za kigeni kama lugha za kufundishia.



31

Hye wo nhye

»Geuza shavu la pili«
Alama ya msamaha

Majibu

Lenga kupata viwango vya juu vya ujuzi katika lugha za Kiafrika na lugha rasmi

Kwa kiasi fulani modeli nyingi za elimu barani Afrika hutangamanisha lugha-mama (au lugha iliyozoeleka kwa mjifunzaji) na lugha rasmi. Tofauti baina ya modeli hizi hutokana na kiwango cha uelewa wa lugha kinachokusudiwa kupatikana na idadi ya lugha ambazo kiwango hiki kimelewa kupatikana. Hivyo basi, sehemu hii inalenga modeli ambazo zipo siyo kwa ajili ya kuwepo tu. Kilicho muhimu ni kwa wajifunzaji wanaweza kupata uelewa katika lugha nyingi.

Katika mfumo wa elimu unaotumia lugha mbili, modeli mbalimbali zenye makundi tofauti tofauti ya lugha zimetengenezwa na kujaribiwa barani Afrika. Modeli zilizozoeleka zaidi (modeli hamishi na modeli za mpito)³ hulenga kuleta kiwango cha juu cha uelewa wa lugha katika lugha moja tu, ambayo kwa kawaida huwa hi lugha ya kigeni yenye wigo mpana wa mawasiliano. Wajifunzaji huanza kwa kutumia lugha yao ya kwanza kama lugha ya kufundishia, na baada ya mwaka mmoja hadi miaka minne hubadilishiwa na kutumia lugha ya pili. Modeli za aina hii huchukuliwa kuwa ni modeli dhaifu za lugha mbili kwa kuwa lengo kuu ni kuleta ujuzi wa lugha moja tu.

Modeli kawizi na za nyongeza hulenga kuleta kiwango cha juu cha uelewa wa lugha ya kwanza na lugha ya pili (na pengine wa lugha zaidi), hivyo hujenga uelewa wa hali ya juu wa lugha kadhaa. Modeli hizi huchukuliwa kuwa ni modeli thabiti za lugha mbili (Baker, 2006). Dokezo hili la sera linawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu ufanisi wa modeli hizi, kwa lengo la kupendekeza njia zinazofaa za kuendeleza uelewa wa lugha nyingi na kusaidia kuleta mafanikio katika kujifunza masomo yote.

Miaka mitatu hadi minne ya elimu kwa lugha-mama haitoshi hata kidogo

Programu za modeli wahishi barani Afrika zinastahili kuthaminiwa sana kwa kazi yake ya uasisi. Hata hivyo, katika mazingira yaliyopo ya ujifunzaji, na kwa kuzingatia kile tunachokifahamu sasa kutokana na utafiti na vitendo, programu hizi hazina budi kupanuliwa kwani, katika kipindi cha mwaka mmoja hadi minne, wajifunzaji walio

Mafunzo kwa waku-funzi, Nijeri




3 Kiambatisho 5
katika faharasa kina
fasili za modeli za
lugha.

wengi hawapati maarifa yanayotakiwa katika kuzungumza na kuandika ambayo elimu shuleni inayahitaji.

Mabadiliko ya lugha ya kufundishia katika mwaka wa tatu au wa nne hufanyika wakati hasa mtaala unapohama kutoka katika kusoma simulizi nyepesi kwenda katika kusoma matini ngumu za kitaaluma. Mabadiliko haya huja kabla ya wakati wake kwa sababu katika hatua hii wanafunzi huwa hawana ujuzi wa kutosha wa lugha ya pili ili iweze kutumiwa kama lugha ya kufundishia. Wanafunzi huwa bado hawajajifunza na kuimarisha maarifa muhimu ya lugha ya kwanza ili waweze kuyatumia katika kujifunza lugha ya pili.

»Mtaalamu bingwa yeyote anayetambulika katika masuala ya isimu nafsia na ujifunzaji wa lugha ya pili hawezi kudai kwamba watoto katika nchi zinazoendelea na katika jamii ndogo au maskini wabadilishiwe lugha ya kufundishia mwishoni mwa darasa/mwaka wa tatu kutoka lugha-mama kwenda lugha ya pili nao wakafanya vizuri tu kwenye masomo yote katika miaka inayofuata ya elimu ya msingi au katika elimu ya sekondari« (Heugh, 2006a: 68).



Juu kushoto: Darasa la kujifunza kusoma na kuandika, elimu kwa lugha mbili, Nijeri

Juu kulia: Wazazi wakiwafundisha watoto, Uganda


Kushoto: Darasa la wasichana, Senegali

Matokeo duni ya ujifunzaji katika shule barani Afrika huchochewa na mazingira magumu ya ujifunzaji kitaaluma, ambamo mara nyingi waalimu hukosa mafunzo kuhusu ujuzi wa kusoma na kuandika na maendeleo ya lugha, na wanafunzi walio wengi hutoka katika familia zisizo na msingi wa kitaaluma na hujifunza kwa lugha wasiyojua na ambayo haikuzoeleka kwao katika shule zisizokuwa na vifaa vya kutosha.

Elimu kwa lugha-mama – MUDA MREFU ZAIDI, MATOKEO BORA ZAIDI

Ripoti ya Taifa ya Tathmini ya Elimu kwa Darasa la Sita nchini Afrika Kusini ya mwaka 2005 inaonyesha kwamba wanafunzi wanaojifunza kwa lugha-mama hufaulu masomo ya lugha kwa wastani wa asilimia 69 kitaifa. Wanafunzi wanaojifunza kwa lugha tofauti na lugha-mama hupata asilimia 32 tu.

»Utafiti unaonyesha kwamba watoto walio wengi huhitaji miaka isiyopungua 12 ili waweze kuwa mahiri katika L1 [lugha ya kwanza]. Kuna mahitaji thabiti ya miaka isiyopungua saba ya kupata elimu ya msingi katika L1, lakini mipango ya kuanzisha matumizi ya L2 [lugha ya pili] inaweza kubadilishwa kwa urahisi zaidi. Ubora wa mafunzo ya L2 anayopata mtu, na si wingi wa matukio ya kukutana na L2, ndio unaomwezesha mtu kujifunza kwa mafanikio lugha hii ya ziada. Muda wa kuanza kutumia L2 sio jambo la muhimu sana kama ulivyo utoaji wa lazima wa waalimu wa lugha, vifaa na raslimali zinazofaa, mitazamo yenye kuunga mkono na waalimu na wazazi, na haja ya kuufanya mchakato wa ujifunzaji kuwa ule unawaovutia watoto« (Western Cape Education Department, 2002).



Fofoo se die fofoo pe ne se gyanantwi abo bedie
Wivu

Matokeo mazuri katika lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano kupitia modeli ipi?

Modeli za lugha katika elimu barani Afrika zimetathminiwa ili kubainisha ni jinsi gani zinavyofaa katika kufundisha lugha ya pili, lugha ya kigeni, na vilevile masomo mengine. Tathmini hiyo inaonyesha kwamba kuna mikabala mitatu ya kielimu ambayo huwasaidia wanafunzi barani Afrika kujifunza kwa mafanikio (Heugh, 2006a):

- 1. Modeli ya elimu kwa lugha-mama wakati wote wa elimu ya msingi na sekondari:** Wajifunzaji hufundishwa mtaala wote kwa lugha-mama na kujifunza lugha za ziada kutoka kwa waalimu wa lugha walioboea. (Kwa mfano, wazungumzaji wa Kiafrika nchini Afrika Kusini wanaohudhuria kipindi kimoja tu kwa siku wameweza kuwa na uelewa wa hali ya juu wa lugha ya Kiingereza.)
- 2. Modeli ya nyongeza ya elimu kwa lugha mbili:** Wajifunzaji hufundishwa kwa miaka isiyopungua sita hadi nane kwa lugha-mama. Katika kipindi hicho hufundishwa lugha ya kigeni kama somo na mwalimu aliyeboea. Baadaye, huendelea na elimu itolewayo kwa lugha mbili, ambapo baadhi ya masomo hufundishwa kwa lugha-mama na mengine kwa lugha ya pili.
- 3. Modeli inayokawiza sana mabadiliko kuelekea lugha ya pili:** Wajifunzaji hufundishwa kwa miaka minane kwa lugha-mama na hufundishwa lugha za ziada na waalimu wa lugha walioboea. Katika mwaka wa tisa, hufanyiwa mabadiliko na kutumia lugha ya pili kama lugha ya kufundishia. Hii ndiyo sera inayotumiwa nchini Ethiopia; hata hivyo, haitekelezwi katika mikoa yote. Kuanzia mwaka 1955 hadi 1976, wanafunzi weusi nchini Afrika Kusini waliokuwa katika shule zenye raslimali duni, kupitia programu ya aina hii, walifanya vizuri katika masomo yote, likiwemo somo la lugha ya Kiingereza. Mwaka 1976, kiwango cha kufaulu kilikuwa asilimia 83.7. Baada ya mwaka 1976, muda

wa elimu kwa lugha-mama ulipunguzwa hadi miaka minne, kiwango cha kufaulu nacho kikashuka na kufikia asilimia 44 mwaka 1992. Yawezekana kulikuwa na vigezo vingine vilivyochangia kushuka huku kwa kiwango cha kufaulu, lakini kwa hakika kigezo cha lugha ndicho kikuu.

- Modeli kawizi:** Lugha-mama huendelea kuwa lugha ya kufundishia hadi mwaka wa tano na huendelea kufundishwa kama somo. Utaratibu wa aina hii unaweza kuleta uelewa wa lugha ya pili pasipo kuathiri ule wa lugha ya kwanza ikiwa ufundishaji unaofaa wa lugha ya kwanza na ya pili utatumwa kwa pamoja na maudhui mazuri. Utaratibu wa aina hii, kwa mfano, umeanzishwa nchini Bukinafaso ambako kwa sasa unaingizwa katika mfumo wa elimu unaotumiwa na walio wengi.

Faida za kiutambuzi za elimu kwa lugha-mama baada ya miaka sita hadi minane

Matumizi ya lugha iliyozeleka ni jambo la lazima kwa michakato fanisi ya kujifunza na kufundisha kiutambuzi. Msingi imara wa maendeleo ya kitaaluma na kiutambuzi katika lugha ya kwanza hujengwa baada ya miaka minane katika shule zisizokuwa na vifaa vya kutosha (Heugh, 2006a). Kutumia lugha iliyozeleka kama lugha ya kufundishia kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ya elimu ya msingi hujenga pia msingi imara wa kuweza kuhamisha maarifa magumu kutoka lugha iliyozeleka kwenda lugha nyinginezo.

Jedwali 1

Alama za wastani zinazotarajiwa kwa lugha ya pili (kama somo) kwa wanafunzi wa Darasa la

60%				
50%				
40%				
30%				
20%				
10%				
0				
Modeli	<i>1a</i> <i>Hamishi</i>	<i>1b</i> <i>Hamishi</i>	<i>2a</i> <i>Wahishi ya mpito</i>	<i>2b</i> <i>Wahishi ya mpito</i>
Matumizi ya L2 na L1	L2 = LYK hadi mwisho pamoja na kuondosha L2	L2 = LYK hadi mwisho pamoja na kustawisha L2 ili kufundishia masomo	L1 = LYK kwa miaka 2-3 kisha kuhamia katika L2 kama LYK	L1 = LYK kwa miaka 2-3 kisha kuhamia katika L2 kama LYK na kustawisha L2 ili kufundishia masomo
Mahali inakotumiwa modeli	Nchi nyingi za Afrika: Awali ilitumiwa na nchi zinazozungumza Kifaransa na Kireno tu, kisha ikatumiwa pia na nchi za kusini mwa Afrika zinazozungumza Kiingereza			Nchi za kusini mwa Afrika; Marekani

L1 = Lugha ya kwanza/lugha-mama
L2 = Lugha ya pili
LYK = Lugha ya kufundishia

Kwa maelezo ya istilahi »Kuondosha L2« na »Kustawisha L2« tazama faharasa (Kiambatisho 5)

Ulinganishi wa kimataifa wa ujuzi wa lugha ya pili wa wanafunzi wa mwaka wa 10 hadi wa 12 unaonyesha tofauti zinazotegemea programu ya elimu ya lugha ambamo wanafunzi hushiriki (tazama Jedwali 1). Kwa kadiri lugha-mama ilivyoendelea kutumiwa kwa muda mrefu zaidi katika elimu yao, ndivyo walivyopata alama nzuri zaidi katika tathmini ya ufaulu katika lugha ya pili. Jedwali lililopo hapa chini linaonyesha tofauti baina ya modeli tisa za lugha na kuzihusisha na alama za ufaulu wa lugha ya pili zinazoweza kutarajiwa. Alama zinazoweza kutarajiwa zinatokana na matokeo yaliyopo ya utafiti kutoka barani Afrika na kwingineko duniani kwa mwaka 2005 na 2006, na yanahusiana na shule zenye raslimali za kutosha. Ikumbukwe kwamba mikakati na sera hubadilika wakati wote, na tayari zimebadilika kwa wakati huu.

Modeli nyingi zinazotumiwa barani Afrika ni zile za modeli 1a na 2b. Alama zinazoweza kutarajiwa katika lugha ya pili katika mwaka wa 12 ni kati ya asilimia 20 na 40. Modeli 3, kwa mfano, inatumiwa nchini Ethiopia kwa lugha ya Kiamhariki na hadi hata miaka minane kwa wanafunzi wanaozungumza lugha ya Kitigrinya, Kioromifa, na Kisomali; nchini Tanzania (kwa lugha ya Kiswahili); na nchini Nijeria (Six Year Primary Project). Modeli kawizi inayotumiwa na shule zinazotoa elimu kwa lugha mbili zilizojumuishwa katika mradi unaoendeshwa kwa pamoja baina ya Wizara ya Elimu ya Msingi na Kusoma na *Œuvre suisse d'entraide ouvrière* nchini Bukinafaso itadumu kwa miaka mitano



Nsirewa

»Hebu tuishi pamoja«
Umoja, mapatano

10-12 katika shule zenye vifaa vya kutosha kulingana na chaguo za awali za lugha ya kufundishia

<i>2c</i> Wahishi-kati ya mpito	<i>3a</i> Kawizi ya mpito	<i>3b</i> Kawizi sana ya mpito	<i>4a</i> ya Nyongeza	<i>4b</i> ya Nyongeza
L1 = LYK kwa miaka 4 kisha kuhamia kwenye L2 kama LYK, L1 kama LYK	L1 = LYK kwa miaka 6/7 kisha L2 kama LYK	L1 = LYK kwa miaka 8 kisha L2 kama LYK	Lugha mbili za kufundishia: L1 = LYK kwa miaka 5-6, L1 + L2 kama LYK kuanzia mwaka wa 7	L1 = LYK hadi mwisho na ufundishaji thabiti wa L2 kama somo
Bukinafaso; mikoa miwili nchini Ethiopia; Namibia (1976-1990); Afrika Kusini (1976-1995); hadi hivi karibuni kwa lugha moja (Chichewa) nchini Malawi	Six Year Primary Project, Nijeria; baadhi ya mikoa nchini Ethiopia; Tanzania (Kiswahili)	Mikoa mitatu nchini Ethiopia (Somali, Oromifa, Tigrinya); Afrika Kusini na Namibia (1955-1975); Gine (Konakiri) (1966-1984)	Afrika Kusini mwanzoni mwa karne ya 20. Tafiti kutoka Afrika, Ulaya, na Marekani zinadai hii inaweza kufanya kazi vizuri katika Afrika ya sasa	Afrika Kusini, kwa wazungumzaji wa Kiingereza na wa Kiafrika – na kuleta ujuzi wa hali ya juu wa lugha mbili

na imepanuliwa hadi kwa elimu ya sekondari katika »*Collège Multilingue Spécifique*« ambako lugha ya kitaifa iliyokuwa ikitumiwa kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi inafundishwa kama somo na lugha rasmi ambayo ni Kifaransa inakuwa lugha ya kufundishia. Zaidi ya hayo, wanafunzi wanajifunza lugha ya pili ya kitaifa pamoja na Kiingereza.

Modeli 4b imetumiwa nchini Somalia kwa wazungumzaji wa Kisomali na nchini Afrika Kusini kwa wazungumzaji wa Kiafrikana. Wazungumzaji wa Kiafrikana nchini Afrika Kusini walinufaika sana na utaratibu huu; wako miongoni mwa wanafunzi wanaofaulu vizuri zaidi mwishoni mwa elimu ya sekondari. Kwa mantiki hii, uchaguzi wa modeli ya lugha kwa shule za msingi una matokeo yanayodumu kwa muda mrefu. Maisha ya kitaaluma ya wanafunzi hutegemea uchaguzi huu. Heugh anaeleza kwamba »ukweli huo hujitokeza waziwazi kwa namna inayoumiza sana nchini Afrika Kusini kwani wanafunzi pungufu ya asilimia 1 wanaozungumza lugha za Kiafrika kama lugha-mama ndio tu huweza kupata alama nzuri katika somo la Hisabati na Sayansi zinazowawezesha kuingia chuo kikuu mwishoni mwa elimu ya sekondari« (Heugh, 2006a: 72).

36

L1 = Lugha ya kwanza

L2 = Lugha ya pili

L3 = Lugha ya tatu

LYK = Lugha ya kufundishia

LKWM = Lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano

Mapendekezo ya kuanzisha mifumo ya elimu kwa lugha nyingi

Kwa kuzingatia utafiti katika lugha na elimu barani Afrika (Alidou na wenzie, 2006; Ouane, 2003), majedwali yafuatayo yanatoa mifano ya njia mbalimbali za kuunda modeli za nyongeza za lugha mbili kwa mwaka, aina ya lugha, na matumizi ya lugha. Modeli hizi ni za kutolea elimu kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa kumi na mbili. Zimejengwa katika msingi wa kupunguza kabisa matumizi ya lugha mbili na kuweka kusudio bora la matumizi ya lugha tatu. Mpangilio wa matukio ya baadaye umeainishwa pia katika hali kuu tatu kwa kujumuisha au bila kujumuisha lugha za

Jedwali 2 Mapendekezo kwa nchi zenye lugha nyingi pasipo lugha dhahiri ya kitaifa yenye wigo mpana wa mawasiliano

Mwaka	Muda wa kufundisha na aina ya kazi kwa kila lugha		
	% ya L1 kama somo na LYK	% ya L2 (LKWM) kama somo na LYK	Chaguo la hiari: % ya L3 kama somo na/au LYK
1-2	90%: kusoma, kuandika, na kuhesabu	10%: kuzungumza zaidi	
3-4	80%: kukuza ujuzi wa kusoma na kuandika	15-20%: kuzungumza, kusoma, na kuandika	5%: kuzungumza
5	70%: hasa kwa hisabati, sayansi, kuimarisha kusoma na kuandika L1, na L1 kama somo	20-30%: kusoma na kuandika, na kama somo; inaweza pia kutumiwa kama LYK kwa michezo/ muziki/ sanaa	10%
6	60%: hisabati na sayansi; na ama jiografia au historia; kuimarisha kusoma na kuandika kitaaluma, na L1 kama somo	30-40%: kusoma na kuandika na kama somo; na inaweza kutumiwa kama LYK katika michezo/ muziki/ sanaa na historia au jiografia	10%
7-12	45-50%: kwa hisabati, sayansi, n.k., kuimarisha kusoma na kuandika kitaaluma, na L1 kama somo	40-50%: kujenga ujuzi wa kusoma na kuandika kitaaluma, na kama somo, na inaweza kutumiwa kama LYK kwa michezo, historia, jiografia, n.k.	10-15%: kama somo, na inaweza ikatumiwa kama LYK katika sanaa au somo lingine

kitaifa, lakini hujumuisha lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano; hivyo basi, katika mifano yote, modeli hizi hujumuisha kikamilifu miktadha iliyoenea pote ya lugha zilizo jirani barani Afrika.

Jedwali 2 linaonyesha chaguo la lugha mbili na vilevile chaguo la hiari la lugha tatu kwa nchi zilizo na lugha nyingi pasipo kuwa na lugha thabiti ya kitaifa yenye wigo mpana wa mawasiliano bali lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano kama lugha rasmi.

Jedwali 3 linaonyesha chaguo la lugha tatu kwa nchi zilizo na lugha moja au zaidi za kitaifa zenye nguvu na wigo mpana wa mawasiliano pamoja na lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano.

Jedwali 3 Mapendekezo kwa nchi zenye lugha nyingi na lugha ya taifa yenye wigo mpana wa mawasiliano

Mwaka	Muda wa kufundisha na aina ya kazi kwa kila lugha		
	% ya L1 kama somo na LYK	% ya L2 (LTWM) kama somo na LYK	Chaguo la hiari: % ya L3 (LKWM) kama somo na/au LYK
1-2	80%: kusoma, kuandika, na kuhesabu	20%: kuzungumza zaidi	
3-4	70%	30%: kuzungumza; kusoma, kuandika, na kuhesabu	
5	50% na kuendeleza kusoma na kuandika	40%	10%
6-7*	40% na kuendeleza kusoma na kuandika	40%	20%
8-12**	± 35%: kuimarisha kusoma na kuandika kitaaluma na L1 kama somo	± 35% na kujenga ujuzi wa kusoma na kuandika kitaaluma	30% na kujenga ujuzi wa kusoma na kuandika kitaaluma



Wawa Aba

Wawa ni aina ya mti mgumu utumiwao katika uchongaji Nguvu

L1 = Lugha ya kwanza
L2 = Lugha ya pili
L3 = Lugha ya tatu
LYK = Lugha ya kufundishia
LTWM = Lugha ya (ki)taifa yenye wigo mpana wa mawasiliano
LKWM = Lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano

* L1 haina budi kubaki kwa asilimia 50 ya muda wa mafundisho kwa siku. Hata hivyo, lugha ya tatu ikiingizwa katika modeli, mabadiliko hayana budi kufanywa. L1 itaendelea kutumiwa angalau kwa nusu ya muda wote uliobaki katika mtaala.

** Mabadiliko muhimu ya kutumia LTWM ni sahihi katika hatua hii kwani ni lugha inayotumiwa sana katika eneo hili na wajifunzaji hukutana nayo sana kuliko »lugha ya kigeni«/ LKWM.

Chanzo: Heugh, 2006a

Jedwali 4 linaonyesha chaguo mbili kwa modeli inayotumia lugha-mama/lugha ya Kiafrika kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mfumo wa elimu na yenye ufundishaji thabiti wa lugha ya pili. Chaguo A ni la mfumo wa lugha mbili na Chaguo B ni la mfumo wa lugha tatu.

Jedwali 4 Elimu kwa lugha ya Kiafrika/lugha-mama mwanzo hadi mwisho pamoja na ufundishaji thabiti wa lugha ya pili kama somo – namna mbili yakini

Mwaka	Muda wa kufundisha kwa kila lugha		
	% ya L1 kama somo na LYK	% ya L2 (LTWM) kama somo na LYK	% ya L3 (LKWM) kama somo na/au LYK
Chaguo A			
1-12	80%	20%	
Chaguo B			
1-4	80%	10%	10%
5-12	65-70%	10-15%	15-20%

Chanzo: Heugh, 2006a

Jedwali 5 linaonyesha jinsi Bukinafaso na Nijeri zinavyofanya mabadiliko sasa katika mifumo yao ya elimu kitaifa.

Jedwali 5 Mikakati ya Bukinafaso na Nijeri ya kubadili mifumo ya elimu kitaifa

Aina ya shule, mwaka	Muda wa kufundisha na kazi kwa kila lugha	
	BUKINAFASO	NIJERI
Chekechea	L1 LYK 100%	L1 LYK 100%
Shule ya msingi:		
1	L1 LYK 90%, LKWM LYK 10%	L1 LYK 100%
2	L1 LYK 80%, LKWM LYK 20%	L1 LYK 100%
3	L1 LYK 50%, LKWM LYK 50%	Ama mwaka wa 3 au wa 4, LKWM LYK 100%
4	L1 LYK 20%, LKWM LYK 80%	L1 kama somo
5	L1 LYK 10%, LKWM LYK 90%	LKWM LYK 100% L1 kama somo
6	LKWM LYK 100%, L1, LTWM na Kiingereza kama masomo	LKWM LYK 100% L1 na L2 kama masomo
Shule ya sekondari:		
7	LKWM LYK 100%, L1, LTWM na Kiingereza kama masomo	
8		
9		
10		

L1 = Lugha ya kwanza
L2 = Lugha ya pili
LYK = Lugha ya ku-fundishia
LTWM = Lugha ya (ki)taifa yenye wigo mpana wa mawasiliano
LKWM = Lugha ya kimataifa yenye wigo mpana wa mawasiliano

Chanzo: Alidou na wenzie, 2008 na 2009

6. Je, elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi inawezekana kugharamiwa?

Tatizo

Kwa mtazamo wa kiuchumi, je, inawezekana kutoa elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi katika mfumo unaotumiwa na walio wengi?

Licha ya matokeo mazuri yaletwayo na programu za lugha mbili, watu wengi wana mashaka iwapo raslimali haba za nchi za Kiafrika zinapaswa kutumiwa kubadili mfumo wa elimu kuwa ule unaotoa elimu kwa kutumia modeli kawizi au za nyongeza za lugha mbili, hususani ukizingatia mazingira ya ujifunzaji na hali ya madarasa kuwa na wanafunzi wanaozungumza lugha tofautitofauti barani kote. Je, ni kweli jambo hili linapaswa kupewa kipaumbele, na kitu gani kitarajiwe kutokana na uwekezaji huu? Je, haitakuwa ghali mno kutengeneza vifaa vya kufundishia, kuwapa mafunzo waalimu, na kuendeleza lugha hizi?

Katika sehemu inayofuata tunajaribu kuchambua maswali haya. Uchumi wa elimu ya lugha nyingi ni uwanja mpya wa taaluma na uhusiano kati ya lugha na ujifunzaji bado haueleweki vizuri kwa wataalamu wa uchumi walio wengi (Gorter na wenzie, hakuna tarehe).



Nkyimkyim

»Mizunguko ya maisha«

Ari, nguvu, uelekevu

39

Majibu

Je, manufaa yapi hupatikana? Faida kubwa zaidi ya kuwekeza kwenye jamii nzima

Kuna kanuni ya uchumi isemayo kwamba gharama hazina budi kulinganishwa na faida itokanayo na gharama hizo. Kwa suala la elimu fanisi kwa lugha-mama na lugha nyingi, matokeo ya tafiti yanaonyesha kuwepo kwa manufaa ya muda wa kati na ya muda mrefu yaliyo makubwa kiasi cha kutosha kuhalalisha kufanywa kwa utafiti kuhusu maswali ya wazi yaliyobaki na kuzikubali gharama zake kubwa.

Tathmini ya programu za elimu iliyowasilishwa katika sehemu zilizotangulia inaonyesha wazi kwamba, ikilinganishwa na programu nyingine, elimu yenye ubora wa hali ya juu kwa lugha mbili itumiayo modeli kawizi na modeli ya nyongeza huleta faida kubwa na usawa zaidi kutokana na uwekezaji uliofanywa. Faida ya elimu fanisi kwa lugha-mama na lugha nyingi huonekana katika ongezeko la alama za kufaulu, na vilevile katika kiwango cha chini cha idadi ya wanafunzi wanaorudia madarasa na wanaoacha shule. Nchini Afrika Kusini, kwa mfano, inaonyesha kwamba wanafunzi wanaofaulu kwa kiwango cha juu katika mitihani yao ya kumaliza shule ni wale tu wanaoweza kujifunza kwa lugha yao ya kwanza. Huku kukiwa na ongezeko la asilimia 5 tu katika bajeti ya elimu, tafiti za sasa (Grin, 2005; Heugh, 2006b) zinadai kwamba sehemu kubwa ya gharama za kufanya mabadiliko ya aina hiyo zitarejeshwa baada ya miaka mitano hadi saba kutokana na kuwepo idadi ndogo ya wanafunzi wanaorudia madarasa na wanaoacha shule.

»Makadirio ya kiuchumi ya mabadiliko ya lugha na ya kiutamaduni huanza na kauli kwamba maadili ya jamii hayana budi kutokana na maadili ya mtu mmoja mmoja...« (Gorter na wenzie, hakuna tarehe: 23). Elimu itolewayo kwa lugha nyingi ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi huleta manufaa ya namna nyingi kwani huamsha watu, huunga mkono uenezaji na utumiaji wa maarifa na uwezo wake kwa kuondoa vikwazo vya lugha, hupanua ujuzi wa lugha na mawasiliano, na husaidia kutatua migogoro (Adegbija, 2003; Bamgbose, 2000). Utafiti na usimamizi wenye mwelekeo wa

kivitendo hauna budi kutafiti kwa kina zaidi ukweli kuhusu matumizi ya lugha nyingi katika suala hili. Ikumbukwe kwamba kwa jumla wataalamu wachache sana wa uchumi katika elimu ndio tu wanaoelewa uhusiano uliopo kati ya lugha na ujifunzaji. Tafiti wiani kuhusu gharama, usimamizi wa fedha, na matokeo ya elimu itolewayo kwa lugha nyingi ni haba (Carr-Hill na Roberts, 2007), hivyo tafiti hizi zinahitaji kufanywa katika maeneo ya taaluma zaidi ya moja.

Programu bora za lugha mbili zinalingana na gharama zake

Ikiwa tunauliza endapo tunaweza kumudu elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi, itolewayo kwa modeli kawizi/modeli ya nyongeza, hatuna budi pia kuuliza endapo modeli za sasa za lugha zilizopo shuleni ni nafuu zaidi kwa kuangalia gharama na faida halisi inayotokana na uwekezaji unaofanywa, achilia mbali suala la mshikamano katika jamii na upatikanaji wa fursa mbalimbali. Kuna kiasi kidogo cha utafiti uliofanywa kuhusu mada hii. Hata hivyo, ulinganishi ulifanywa nchini Mali baina ya »Pédagogie Convergente«, modeli wahishi inayoelekea katika modeli kawizi yenye mkabala wa lugha mbili za kufundishia katika mwaka wa tano na wa sita, na mfumo wa elimu uliozoeleka shuleni (Fomba na wenzie, 2003). Utafiti huo ulifikia hitimisho kwamba faida itokanayo na programu za ujifunzaji zilizoboreshwa inalingana na gharama zake na kwamba gharama za juu kiasi ni jambo linalostahili. World Bank (2005) ililinganisha gharama na faida za programu zinazotumia Kifaransa pekee na zile za lugha-mama nchini Mali na kubaini kwamba jumla ya gharama za mwanafunzi mmoja kwa miaka sita ya kuhudhuria elimu ya msingi katika programu zinazotumia Kifaransa pekee zilikuwa juu kwa asilimia 27. Vipengele vikuu vilivyobainishwa kuwa hupunguza gharama vilikuwa ni kuwepo kwa idadi ndogo ya wanafunzi wanaorudia madarasa au kuacha shule.

Je, kuna gharama zipi kuhamia katika elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi?

Ulinganishi wa gharama za modeli hamishi/wahishi, elimu ya msingi kwa lugha-mama na lugha mbili au zaidi kama masomo itolewayo kwa modeli kawizi/ya nyongeza na mipango ya kimkakati kwa ajili ya mabadiliko ya aina hii ulibainisha shughuli za aina nane ambazo zina gharama kubwa, hususani zile za muda mfupi na wa kati. Shughuli hizo ni kama vile:

1. Kuimarisha mfumo wa kutunga sheria na wa kitaasisi.
2. Kuendeleza lugha kwa ajili ya mtaala mpya: a) kuunda tahajia kwa lugha zisizokuwa nayo bado; b) kuunda istilahi kwa ajili ya mtaala; na c) kutunga vitabu vya sarufi, kamusi, na msamiati vya lugha moja na lugha mbili.
3. Kutengeneza atlas ya jamii-lugha kitaifa.
4. Kutunga na kutoa miongozo ya waalimu, vifaa vya wajifunzaji, na mitihani ya kumaliza shule.
5. Kuendeleza rasimali watu ya kutekeleza mabadiliko haya.
6. Kuchagua shule kwa awamu ya majaribio.
7. Kusimamia na kutathmini awamu za majaribio na utekelezaji.
8. Kuendeleza mazingira yenye elimu kwa lugha nyingi.
9. Kuunda na kutekeleza mkakati wa mawasiliano kwa ajili ya kuendeleza elimu kwa lugha nyingi.

Hivi karibuni nchi ya Nijeri imefanya utafiti ili kuunda mkakati wa kitaifa utakaowezesha kuingiza elimu kwa lugha mbili katika mfumo wa elimu unaotumiwa na walio wengi katika kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2009 hadi 2019 (Alidou na wenzie, 2009). Mtaala huo wa elimu kwa lugha mbili utawezesha kufundishwa kwa lugha kumi za kitaifa tangu kuanza hadi kumaliza shule, na lugha rasmi itafundishwa kuanzia mwaka wa tatu. Lugha tano kati ya kumi za kitaifa hazijawahi kutumiwa katika mfumo rasmi wa elimu. Uchambuzi wa kina wa gharama za mkakati huu unajumuisha vipengele vyote vya gharama vilivyotajwa hapo juu na unatoa taarifa kuhusu uwekezaji unaohitajika ili

kutekeleza mpango huu. Awamu ya majaribio inakadiriwa kugharimu karibu dola milioni 4 za Kimarekani na utekelezaji dola milioni 100 za Kimarekani.

Nchi ya Bukinafaso iliagiza kufanywa kwa tathmini na kuundwa kwa mpango-kazi (2008 – 2010) utakaowezesha elimu ya msingi kwa lugha nyingi itumiayo modeli ya nyongeza iimarishwe na kuingizwa katika mfumo unaotumiwa na watu wengi (Alidou na wenzie, 2008). Kwa sasa, lugha nane za kitaifa pamoja na Kifaransa zinatumiwa katika programu inayoendelea ya elimu ya msingi kwa lugha mbili, kuanzia shule ya chekechea hadi elimu ya sekondari. Gharama za jumla zinazokadiriwa kwa ajili ya kuimarisha na kueneza programu hii kwa shule 70 za chekechea, 150 za msingi, na 45 za sekondari zitakuwa dola milioni 9.5 za Kimarekani.

Gharama za kuimarisha mfumo wa kutunga sheria na wa kitaasisi zinajumuisha kuwepo kwa fasili ya sera kamilifu ya lugha na pia utafiti kuhusu kuingiza mabadiliko katika muundo wa kitaasisi unaotumiwa na walio wengi (awamu ya uchunguzi, uendelezaji, na utumiaji wa sheria husika).

Kiasi kinachotakiwa kuwekezwa katika uendelezaji lugha hutegemea hatua iliyokwisha fikiwa tayari katika uendelezaji na utumiaji lugha katika mada husika katika elimu na kadhalika.

Heugh (2006b) anaeleza kwamba nchini Afrika Kusini, uendelezaji wa lugha tisa za Kiafrika ili ziweze kutumiwa hadi mwisho wa elimu ya sekondari uligharimu karibu dola 550,000 za Kimarekani. Wakati wa mchakato wa uendelezaji, mikakati minne ifuatayo ya kupunguza gharama na kuokoa muda zilionyesha kuwa na ufanisi mkubwa:

1. Kutumia raslimali zilizopo. Asasi nyingi zisizo za kiserikali tayari zimeshatafiti na kuunda msamiati maalumu katika lugha za Kiafrika. Istilahi hizi zinatumiwa tayari.
2. Kushiriki kwa jamii-lugha husika katika kuendeleza lugha ili kuhakikisha kuwa istilahi mpya zinakubaliwa.
3. Kuendeleza kwa wakati mmoja lugha zinazokaribiana sana huziwezesha kusaidiana katika kuunda istilahi.
4. Kushirikiana raslimali baina ya nchi jirani zenye lugha zinazotambuka mpaka wa nchi na nchi.

Uundaji wa tahajia huhitaji gharama za mara moja tu ambazo zitaendelea kuwa za chini, nao unaweza kufanikishwa katika sehemu nyingi na kufanywa na taasisi kadhaa kama vile Summer Institute of Linguistics (SIL). Ushirikiano kati ya nchi na nchi ili kuhakikisha kunakuwa na ulinganifu wa tahajia za lugha zinazofanana utaleta manufaa ya muda mrefu kwa kuongeza idadi ya wasomaji wa maandiko ya lugha hizo. Mradi wa »Mandingue-Peul« (Mandingo-Fulfulde) katika miaka ya katikati ya 1980 ulisababisha kuenea kwa ulinganishaji wa tahajia, sarufi, na istilahi katika lugha hizi mbili zilizoko katika eneo la nchi 15.

Gharama za atlas ya jamii-lugha kitaifa ni halali kwa sababu atlas itasaidia kuchagua lugha zinazoweza kufundishwa katika kila shule. Itabainisha lugha zinazofaa kufundishwa kwa kila mwanafunzi na sifa kuhusu lugha wanazotakiwa kuwa nazo waalimu na watendaji wengine. Hivyo, atlas hii itakuwa ni kifaa cha msingi kwa uongozi wa shule (Alidou na wenzie, 2009) na kwa mazungumzo na watunga sera, wataalamu, na jamii ya kiraia.

Uundaji na utoaji wa miongozo ya waalimu na vifaa vya wajifunzaji haupaswi kufanywa kwa kutafsiri au kurekebisha tu vifaa vinavyotumiwa katika shule zinazotoa elimu kwa lugha moja. Vifaa hivi ni lazima viakisi mkabala wa lugha nyingi na vitengenezwe katika



Ako-Ben

Pembe ya vita

Silaha mkononi

lugha iliyokusudiwa. Kwa kuzingatia maudhui na mbinu ya ufundishaji, baadhi ya miongozo na vifaa vitakuwa kwa lugha moja na vingine vitakuwa kwa lugha mbili. Vifaa vyote na miongozo yote vinahitaji kufanyiwa majaribio.

Uendelezaji wa mazingira ya elimu kwa lugha nyingi utajumuisha kubuni vifaa vya kujifunzia kusoma vilivyosukwa vilivyo ili kukidhi ujuzi wa kusoma, shauku ya kusoma, na uchaguzi wa masomo wa wajifunzaji. Wizara ya Elimu itahitaji kuwa na maandiko ili kueneza na kuingiza katika mfumo unaotumiwa na walio wengi programu ya elimu inayotolewa kwa lugha nyingi na kuhimiza wajifunzaji kufanya mazoezi ya kusoma nje ya shule.

Mikakati fanisi ya wachapishaji ili kutoa vitabu kwa lugha za Kiafrika: mifano kadhaa

Kwa mujibu wa kampuni ya Gamsberg Macmillan Publishers nchini Namibia (Reiner, forthcoming), ni vigumu kupata faida kwa kuchapisha maandiko kwa lugha ya Kiafrika iwapo soko la lugha hiyo bado ni dogo. Katika mazingira hayo, mchapishaji hutumia njia mbadala, kama vile desturi iliyozeleka ya kuongeza bei kwenye maeneo yenye faida na kupunguza bei kwenye maeneo yenye faida kidogo ili kuongeza polepole soko lenye faida kidogo au kulidumisha tu kupitia makundi madogomadogo yaliyokusudiwa. Mikakati ya kupunguza gharama hujumuisha kuongeza idadi ya chapa ili kukidhi mahitaji ya wateja wa ziada na kutunza machapisho boharini hadi yatakapouzwa badala ya kuyatupa. Bei za vitabu zinaweza kupunguzwa pindi machapisho yanaponunuliwa kwa pamoja; zaidi ya hayo, bei ileile inaweza kutumiwa kwa chapisho lililo katika lugha tofauti. Kwa lugha zinazotambuka mpaka wa nchi na nchi kama vile Chinyanja, Silozi, na Chitonga, mipango ya kushirikiana vitabu imewekwa kwa nchi za Zambia, Malawi, Namibia, na Zimbabwe (Muyeeba, 2004). Kusanifisha tahajia za lugha hizi kutawezesha kupatikana kwa manufaa makubwa zaidi na zaidi. Shirika la ARED la nchini Senegali huuza vitabu vilivyoandikwa kwa lugha za Kiafrika kati ya dola moja hadi tatu za Kimarekani. Shirika hili huweza kufanya hivyo kutokana na mkakati wake wa kulipia gharama za uendelezaji kupitia shughuli zake za asasi isiyo ya kiserikali, na kuwaomba wanunuzi wa vitabu wa maeneo husika kulipia gharama zilizobaki za upigaji chapa na usambazaji (Carr-Hill na Roberts, 2007). Gharama za kutafsiri maandiko zinaweza kupunguzwa kupitia tekinolojia za kisasa za habari na kushirikiana pamoja hifadhi za data (*databases*) za istilahi.

Mkakati wa mawasiliano wa lugha nyingi na wenye kujali utamaduni ili kukuza elimu itolewayo kwa lugha nyingi utaleta shauku na kukubalika kwa mkabala huu mpya miongoni mwa makundi yote ya jamii. Vigezo vyake vya gharama za uundaji, utekelezaji, na utathmini hutofautiana kufuatana na mkakati uliotumiwa kwa kila tukio.

Gharama za uendelezaji wa raslimali watu ili kutekeleza mabadiliko katika sekta nzima na sekta mbalimbali

Gharama hizi zitajitokeza katika awamu ya kwanza ya mabadiliko. Makundi matatu yafuatayo yatahitaji mafunzo ya awali na yaliyo endelevu: 1) viongozi waandamizi na wataalamu bingwa ambao wataongoza na kusimamia mchakato wa mabadiliko; 2) maofisa ufundi wa wizara, wakufunzi wa waalimu, wakaguzi, na washauri; na 3) wakurugenzi wa shule na waalimu wa shule. Uendelezaji wa raslimali watu hizi ni uwekezaji chanya wa awali ambao utaleta faida pindi programu itakapoingizwa katika mfumo unaotumiwa na walio wengi. Kwa hiyo, manufaa yatakayopatikana yatazidi gharama zilizotumika.

Gharama za utoaji mafunzo kwa waalimu zinaweza kupunguzwa ikiwa nchi zitakubali kushirikiana raslimali zenye ubora wa hali ya juu zinazoweza kutatua matatizo waliyo nayo kwa pamoja. Programu maalumu za mafunzo kwa waalimu na watunga sera tayari zinapatikana katika elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi.

Modeli zote za elimu ya lugha huhitaji mafunzo kwa waalimu ili kupata elimu bora

Mafunzo kwa waalimu yatakuwa sehemu ya uwekezaji wa awali na endelevu katika raslimali watu. Hata hivyo, katika kutathmini uwekezaji unaohitajika, haina budi kukumbuka kwamba hata pasipo mabadiliko yoyote, mafunzo kwa waalimu yanahitajika haraka ili kuboresha elimu barani Afrika. Kwa sasa, waalimu walio wengi hawana ujuzi wa lugha za kufundisha. Zaidi ya hayo, waalimu wa masomo yote hawana budi kupewa mafunzo ya lugha na mbinu za kufundisha kusoma na kuandika.

Heugh (2006b) alitathmini kiwango cha mafunzo kazini ambayo waalimu wanayahitaji kwa modeli tano tofauti za lugha (tazama Jedwali 6).

L1 = Lugha ya kwanza
LK = Lugha ya kigeni
LA = Lugha ya Kiafrika
L2 = Lugha ya pili
I/F/R/H = Kiingereza, Kifaransa, Kireno, au Kihispania
LYK = Lugha ya ku-fundishia
LM = Lugha-mama
, **, * tazama ukurasa ufuatao*

Jedwali 6 Mafunzo yanayohitajika kwa waalimu kwa kila modeli ya elimu ya lugha

L2/LK tu	L2/LK tu	Modeli kawizi	Modeli thabiti/ya nyongeza ya lugha mbili (LA + L2 kama LYK)	LA/LM kama LYK hadi mwisho + L2 kama somo
Asilimia 100* ya waalimu wa mwaka 1-12 wanahitaji kuboresha ujuzi wao wa I/F/R/H.	Asilimia 75 ya waalimu wote (wanaofundisha darasa la 4-12) wanahitaji kuboresha ujuzi wao wa I/F/R/H.	Asilimia 50 ya waalimu wote (wote wanaofundisha kuanzia darasa la 7-12) wanahitaji kuboresha ujuzi wao wa I/F/R/H.	Asilimia 50 ya waalimu wote (wote wanaofundisha kuanzia darasa la 7-12) wanahitaji kuboresha ujuzi wao wa I/F/R/H.	Asilimia 15 ya waalimu (wale tu waliobeba katika L2 kama somo) wanahitaji kuboresha ujuzi wao wa I/F/R/H.
Asilimia 100 ya waalimu: lugha ya L2 na mbinu za kusoma na kuandika L2 kwa mtaala wote.	Asilimia 100 ya waalimu: asilimia 25 L1, asilimia 75 L2, kwa lugha na mbinu za kusoma na kuandika kwa mtaala wote.	Asilimia 100 ya waalimu: asilimia 50 L1 & asilimia 50 L2, kwa lugha na mbinu za kusoma na kuandika kwa mtaala wote.	Asilimia 100 ya waalimu: asilimia 50 L1 & asilimia 50 L2, kwa lugha na mbinu za kusoma na kuandika kwa mtaala wote.	Asilimia 100 waalimu: asilimia 85 L1 & asilimia 15 L2, kwa lugha na mbinu za kusoma na kuandika kwa mtaala wote.
Waalimu wote wanahitaji mafunzo kuhusu kuboresha maudhui na mtaala – gharama zinafanana kwa modeli zote				
Alama za mwanafunzi zinazotarajiwa: asilimia 20 katika L2**	Alama za mwanafunzi zinazotarajiwa: asilimia 30-35 katika L2	Alama za mwanafunzi zinazotarajiwa: asilimia 50 katika L2	Alama za mwanafunzi zinazotarajiwa: asilimia 60 katika L2	Alama za mwanafunzi zinazotarajiwa: asilimia 60 katika L2
Gharama juu zaidi	Gharama juu	Gharama kati	Gharama kati	Gharama chini zaidi
Thamani*** chini zaidi	Thamani chini	Thamani kati	Thamani juu	Thamani juu

**Tarakimu hizi zinatumiwa kuonyesha uwiano tu. Siku zote katika mfumo wa elimu kuna baadhi ya waalimu walio mahiri na waliopata mafunzo mazuri.*

Hata hivyo, kwa kuwianisha, asilimia 100 ya wale wasiokuwa na ujuzi wa L2 watahitaji kupata mafunzo kazini. Kanuni sawa na hii itumiwe kwa sehemu iliyobaki ya jedwali hii.

***Tazama Jedwali 1*

****Thamani hupatikana kupitia viwango vilivyoongezeka vya mafanikio vinavyoonyeshwa na utafiti uliopo.*

Safu-mlalo ya kwanza katika jedwali hili inaonyesha kwamba waalimu wote wanahitaji mafunzo ikiwa lugha ya kufundishia ni lugha ya kigeni. Katika modeli inayotumia lugha iliyozeleka kama lugha ya kufundishia, asilimia 15 tu ya waalimu wa lugha waliobobea wanaofundisha lugha ya pili au ya kigeni kama somo ndio wanaohitaji mafunzo.

Safu-mlalo tatu za mwisho zinaonyesha mafanikio ya ujifunzaji yanayotarajiwa katika lugha ya pili au lugha ya kigeni na ulinganishi wa gharama na thamani inayoongezeka kwa kila modeli. Modeli yenye gharama za chini zaidi na thamani ya juu zaidi hutumia lugha iliyozeleka (ya Kiafrika, lugha-mama) kuanzia mwanzo hadi mwisho na ina waalimu wa lugha waliobobea katika lugha za kigeni. Kwa jumla, inakadiriwa kwamba pungufu ya asilimia 10 ya bajeti ya vifaa vya kujifunzia na elimu kwa waalimu itatumiwa kutengeneza vifaa kwa lugha za Kiafrika na kutolea mafunzo kwa waalimu. Kwa nchi ya Afrika Kusini, asilimia 10 hii ni pungufu ya asilimia moja ya bajeti nzima ya elimu (Heugh, 2006b).

7. Je, ni katika mazingira gani wazazi na waalimu huunga mkono elimu kwa lugha-mama?

Tatizo

Wazazi na waalimu hukataa elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi

Miradi mingi hukutana na vikwazo kutoka kwa wazazi na waalimu pindi inapopanga kuanza kutoa elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi.

Wazazi wengi wanadai kwamba wanachokitajarajia kutoka shuleni ni watoto wao kufundishwa kwa lugha rasmi ili waweze kuwa na nafasi nzuri zaidi katika soko la kazi. Wana wasiwasi kwamba lugha ya Kiafrika ikitumiwa kama lugha ya kufundishia, watoto wao wataachwa nyuma na watakataa elimu duni. Waalimu wengi walioandaliwa na mfumo unaotumiwa na watu walio wengi, unaotoa elimu kwa lugha ya kigeni, ili waje tena kuutumikia mfumo huo, hawaridhishwi na manufaa ya kutumia lugha za Kiafrika kwa sababu zina thamani ndogo katika mfumo wa elimu unaotumiwa na walio wengi.

Tumeonyesha katika sehemu zilizopita kwamba lugha za Kiafrika ni nyenzo zinazofaa kwa elimu na kwamba elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi huleta athari chanya katika ujifunzaji wa lugha ambayo haikuzoeleka. Hivyo basi, katika sehemu hii tutajikita katika uzoefu walio nao wazazi na waalimu, ambao unaonyesha kwamba upinzani wao halali hutoweka pindi wanapoelimishwa vizuri na kuyaona manufaa ya mkabala huu.



45

Nyame Dua

*Madhabahu ya
mbingu
Mungu
Kuwepo kwa Mungu*

Majibu

Wazazi tegemeo

Ripoti kadhaa za kisayansi kuhusu programu za elimu kwa lugha mbili hukanusha madai kwamba wazazi hupinga elimu kwa lugha-mama na lugha nyingi (kwa mfano nchini Bukinafaso, tazama Alidou na wenzie, 2008). Sababu kuu za ukanushaji huu ni hizi zifuatazo:

- Wazazi si kundi la watu wenye sifa zinazofanana. Maoni yao hutokana na vigezo vingi, na mara nyingi hukosa taarifa kuhusu suala la lugha katika elimu.
- Maswali yanayotumiwa katika utafiti wakati mwingine hupotosha. Pindi wanapoulizwa iwapo hupendelea elimu kwa lugha-mama AU elimu kwa lugha rasmi, mara nyingi wazazi huchagua chaguo la lugha rasmi. Pindi wanapoulizwa iwapo hupendelea (i) elimu kwa lugha-mama NA elimu kwa lugha rasmi, au (ii) elimu kwa lugha moja ambayo ni ya Kiafrika au (iii) elimu kwa lugha moja ambayo ni rasmi, mara nyingi wazazi huchagua chaguo la (i) lugha-mama NA lugha rasmi.
- Shule zitoazo elimu kwa lugha-mama ambazo zimeweza kuwaridhisha wazazi kwamba wamefanya chaguo sahihi, huwachukulia wazazi kwa makini kwa kuwaelimisha vizuri wakati wote.
- Kwa kawaida wazazi huridhika pindi wanapoona watoto katika programu zinazotumia lugha nyingi (lugha-mama/lugha iliyozoeleka + lugha rasmi) wakifanya vizuri kuliko watoto walioko katika shule zinazotumia lugha moja.
- Watoto wanaojifunza kusoma na kuandika kwa lugha-mama huwatia moyo na kuwahimiza wazazi wao pia kujifunza lugha-mama. Mara nyingi wazazi huitikia na kuhudhuria mafunzo ya kusoma na kuandika (hasa kwa lugha mbili) ya watu wazima.

- Shule zinazotambua na kuthamini utamaduni na maarifa ya jamii enyeji zitaweza kuwashirikisha zaidi wazazi na kuondoa kikwazo cha lugha kati ya maisha ya shule na ya nje ya shule.

Waalimu tegemeo

Mara nyingi waalimu huleta upinzani pindi wanapokuwa hawakupata mafunzo au hawana uzoefu na suala la lugha katika elimu na mbinu za ufundishaji zinazowalenga zaidi wajifunzaji (ujifunzaji lugha utotoni, mbinu za kujifunza na kufundisha kusoma na kuandika). Kwa Shule za Elimu kwa Lugha Mbili nchini Bukinafaso ambako waalimu na wakuu wa shule walipata vizuri mafunzo na wajifunzaji wakafaulu vizuri sana, waalimu na wakuu wa shule wote huisifia programu hii na kutaka iingizwe katika mfumo unaotumiwa na walio wengi (Alidou na wenzie, 2008). Zaidi ya hayo, kwa mfano, uzoefu nchini Malawi unaonyesha kwamba waalimu huhitaji vitabu vya kiada vilivyoandikwa kwa lugha ya kufundishia somo husika ili waweze kuandaa lugha kienzo inayohitajika kwa ufundishaji. Waalimu huhitaji vilevile miongozo ya waalimu kwa lugha hiyo ya kufundishia. Mathalani, Wizara za Elimu ya Msingi nchini Bukinafaso, Mali, na Nijeri kwa kushirikiana na mashirika ya INWENT na GTZ zimeandaa mwongozo wa waalimu kwa lugha zote za kitaifa (Galdames na wenzie, 2004). Barani Afrika, modeli nzuri za mafunzo kwa waalimu zipo; mojawapo ya modeli nzuri zaidi iliundwa kwa ajili ya mradi wa lugha ya Kiife nchini Nijeria (Fafunwa na wenzie, 1989).



te



su



ha



ta/o

Katika madarasa mengi barani Afrika, tayari waalimu kwa namna fulani hutoa elimu kwa kutumia lugha mbili: kwa kawaida wanapofundisha kwa lugha rasmi ya kufundishia, hubadilisha na kutumia lugha iliyozoeleka zaidi kwa wajifunzaji. Waalimu huishia kubadilisha lugha ili kuwasaidia wanafunzi wao kuelewa kile kinachofundishwa. Katika baadhi ya nchi, waalimu hutoa hata wito wa kuangaliwa upya kwa sera ya lugha katika elimu ili kuifanyia marekebisho iendane na hali halisi ilivyo darasani (Buchan, Hicks, Read, 2005; International Reading Association, 2005).

Katika utafiti mmoja nchini Uganda, waalimu na wanafunzi walitakiwa kuchagua wapendavyo lugha ya kutumia katika jaribio la kusoma, kuandika, na kuhesabu katika darasa la nne la shule ya msingi. Katika wilaya zote nane ambako utafiti ulifanywa, waalimu na wanafunzi katika maeneo ya vijijini na mijini pia walichagua lugha enyeji kwa sababu walihisi kwamba walikuwa wanaweza kuitumia kwa urahisi zaidi (Okech, 2002).

Shule za binafsi tegemeo na zenye uvumbuzi

Shule binafsi, ingawa hazilengwi hapa, zinaweza pia kutoa msukumo mkubwa wa kuleta mabadiliko. Nchini Bukinafaso, mathalani, shule binafsi, pamoja na misheni ya Kikatoliki, zilikuwa chanzo muhimu na tegemeo pindi zilipoamua kufanya mabadiliko na kutumia mfumo wa lugha mbili.

Hati hii ya Kiethiopia ilitumiwa kwa lugha ya kiliturujia ya Ge'ez na imekuwepo tangu angalau karne ya nne baada ya Kristo. Leo hii, inatumiwa kuandikia lugha ya Kiamhariki, Kitigrinya, Kioromo, na lugha nyingine za nchini Ethiopia na Eritrea.

⋮⋮ |⋮⋮ ⊖:⊖⋮⋮ ⓪⋮⋮ |⋮⋮ |⋮⋮ <|⋮⋮
⋮⋮>⓪:⋮⋮ | ⋮⋮⓪<⊚: ⋮⋮⊚<⓪
+>⊚<||⋮+ γ +⋮:⓪< γ

Chini: Hati ya lugha ya Kivai ndiyo orodha ya zamani kuliko orodha zote za viwakilishi vya silabi za Kimande. Wavai wa nchini Liberia na Siera Leoni wanaendelea kutumia hati hii hadi leo hii (Mafundikwa, 2007).

Juu: Alfabeti ya Tifnaghi ya watu wa jamii ya Waberiberi imekuwa ikitumiwa kwa miaka 2000 iliyopita. Bado inatumiwa na Watuaregi nchini Libya, Algeria, Moroko, Nijeri, Mali, na Bukinafaso, na katika shule za msingi nchini Moroko kufundishia lugha ya Kitamazighi (Mafundikwa, 2007).



Kode Emower Ewa
»Makucha ya tai«
Uaminifu, moyo wa kupenda kutumikia



gi



ga



hi



ha



wi




wa




i



a



Kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi ni uamuzi wa kisera



48 *Alama hizi zilichongwa kwenye vibuyu na wanawake wa Ibibio, Nijeria (Mafundikwa, 2007).*

Kushoto: Nyayo njiani kama kwenye njia ya upendo

Kulia: Msogeo au mwondoko kama katika kucheza ngoma

Haja ya kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi ni uamuzi nyeti wa kisera na ajenda ya kisiasa. Haja hii ipo katika mkingamano wa mageuzi makuu ya kijamii yaletwayo na mpango wa kisiasa, kiutamaduni, na kimaendeleo pamoja na ajenda ya mabadiliko katika elimu. Hii si jitihada fulani tu kuhusu elimu au lugha. Kila mmojawapo wa mipango hii huitikia ujumbe wa wazi kwa kazi maalumu na hulenga kutimiza malengo maalumu ya kuleta mabadiliko.

1. Ajenda ya sera imeegemea katika kigezo cha heshima na ukuzaji wa haki za binadamu, maadili ya kidemokrasia, kuwepo kwa tofauti mbalimbali miongoni mwa watu, tofauti ya mitazamo, na kulinda utambulisho na utamaduni wa watu. Jitihada za kuleta usawa na ushirikishwaji ndiyo mambo yanayochochea kuchagua sera ya aina hii. Hii huunga mkono machaguo na maamuzi mengine yote endelevu na yanayowezekana yaliyofanywa. Chaguo la kupatiwa elimu kwa lugha ajiuayo mtu, ambayo huheshimu na kuakisi utamaduni na maadili ya mtu, ni sehemu ya utoaji wa haki ya elimu katika jamii shirikishi.
2. Ajenda ya utamaduni ni kipengele muhimu cha mpango wa sera. Lugha kama kipengele cha utamaduni na chombo cha kuelezea utamaduni, alama ya utambulisho na chombo cha mtu kujitambua, ni njia muhimu sana katika kukuza na kuleta mabadiliko ya kiutamaduni. Kuheshimu na kukuza lugha zilizopo ni njia ya kujenga mpango wa kiutamaduni na kufikia malengo yake. Kuwekeza katika lugha za Kiafrika na matumizi ya lugha nyingi ni sehemu ya lazima ya ujenzi huu na kipengele cha uwezesaji.
3. Kuwekeza katika lugha za Kiafrika na elimu kwa lugha nyingi ni sehemu ya harakati kubwa za kuleta mabadiliko katika elimu. Kuna ushahidi wa wazi kwamba utamaduni wa elimu bora inayokidhi vigezo vya uhusiano (wa elimu na mahitaji halisi ya wajifunzaji), ushirikishwaji, jinsia, haki, na mafanikio ya juu zaidi ya ujifunzaji unaweza kufikiwa vizuri zaidi na kwa urahisi zaidi kupitia katika lugha-mama ya mjifunzaji. Elimu itolewayo kwa lugha nyingi hujengwa katika msingi wa kuheshimu lugha-mama au lugha za kwanza za watu, na hulea utamaduni, maarifa, na hekima za wenyeji. Lugha-mama zimejitokeza kama kigezo thabiti cha ubora katika tafiti nyingi ambazo awali hazikulenga kushughulikia kipengele hiki. Mpango wowote wa aina hiyo hauna budi kufanywa kwa kutambua kwamba kipengele cha ufundishaji, kipimo cha jumla cha mtaala, mazingira ya ujifunzaji, kiwango cha ubora wa vifaa vya kujifunzia, sifa walizo nazo wafundishaji, na uongozi kwa jumla ni vipengele muhimu sana vinavyohitaji kushughulikiwa kwa ukamilifu na ulinganifu.




4. Ajenda ya maendeleo endelevu hulenga nguzo nne zinazotegemeana za sera. Hizo ni maendeleo ya kijamii, maendeleo ya kiuchumi, utunzaji wa mazingira, na kuheshimu kuwepo kwa tofauti mbalimbali za kiutamaduni miongoni mwa watu (United Nations, 2002 ;UNESCO, 2001). Malengo yake ya msingi ni kujenga mfumo unaogusa sekta mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa watu, usawa katika jamii, ubora wa mazingira, na ustawi wa kiuchumi. Chaguo la lugha na matumizi ya lugha vina nguvu kubwa katika kuleta mawasiliano thabiti, maingiliano ya watu, ushiriki, na ujifunzaji, na ni vya muhimu sana katika kufikia malengo haya.
5. Kutegemeana kwa maeneo haya manne ya sera kunahitaji msukumo thabiti ili kuleta mfungamano mkubwa zaidi miongoni mwayo. Hii inaweza kufikiwa, mathalani, ikiwa sekta rasmi ya elimu itashughulikia ruwaza za mawasiliano na mahitaji ya kielimu ya watu wengi wanaofanya kazi katika sekta ya uchumi isiyo rasmi itoayo »75% ya kazi zilizopo, 80% ya kazi mpya, na karibu 50% ya pato la taifa« (Walther, 2007: 30).



**Papani amma yenju
Kramo**
*»Lila na fila huta-
ngamana«
Unafiki, uzandiki*

Ajenda ya kisiasa hujumuisha vipimo vyote hivi na hujitokeza kama ajenda iliyo na nguvu zaidi na uwezo zaidi wa kuamua.



Kiambatisho 1:

Mwongozo wa kisera wa kuunganisha lugha na tamaduni za Kiafrika katika mifumo ya elimu (ADEA na UIL, 2010)

50 *1 Mwongozo huu ulikubaliwa na Mawaziri wa Elimu kutoka nchi zifuatazo, ambazo zilihudhuria Mkutano wa Afrika kuhusu Kutangamanisha Lugha na Tamaduni katika Elimu, uliofanyika tarehe 20-22 Januari 2010 mjini Wagadugu, Bukinafaso: Benini, Bukinafaso, Chadi, Ethiopia, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Kongo, Kameruni, Kenya, Kodivaa, Libya, Malawi, (Visiwa vya Morisi, Nijeri, Rwanda, Senegali, Uganda, na Zambia. Mkutano huu uliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Association for the Development of Education in Africa (ADEA), UNESCO Institute for Lifelong Learning (UIL), na Wizara ya Elimu ya Msingi na Mafunzo ya Kusoma na Kuandika nchini Bukinafaso, na kupata msaada wa kifedha kutoka*

ulisahihishwa na kukubaliwa na Mawaziri wa Elimu waliohudhuria African Conference on the Integration of African Languages and Cultures in Education (Mkutano wa Afrika kuhusu Kutangamanisha Lugha na Tamaduni za Kiafrika katika Elimu), Wagadugu, Bukinafaso, tarehe 20-22 Januari 2010¹

Utangulizi

Kwa kipindi cha miaka ipatayo sitini sasa, imekuwa ikifahamika kwamba kutumia lugha-mama za wajifunzaji kama lugha za kufundishia katika mfumo wa elimu huongeza kiwango cha ubora wa elimu. Hivyo basi, wataalamu bingwa wote huuchukulia ufundishaji unaofanywa kwa lugha-mama kuwa ni jambo la lazima na mara kwa mara wamekuwa wakiupendekeza katika vikao vingi vya mabaraza ya kitaifa na kimataifa, kama inavyoonyeshwa katika hati rasmi zifuatazo:

- Katiba na sheria za nchi husika;
- Sheria za msingi za elimu za nchi husika;
- Maamuzi ya Mkutano wa kwanza wa Mataifa ya Afrika kuhusu Maendeleo ya Elimu Barani Afrika, uliofanyika mjini Addis Ababa mwaka 1961, na kupendekeza elimu itolewe kwa lugha-mama;
- Mapendekezo ya Mkutano wa nane wa Mawaziri wa Elimu wa Nchi Wanachama za Kiafrika za UNESCO (MINEDAF VIII) kuhusu kubadilisha na kuimarisha hadhi ya lugha-mama, uliofanyika mjini Dar es Salaam (Tanzania) mwaka 2002;
- Mapatano ya Kikanda kuhusu Kutambua Mitaala, Vyeti, Stashahada, Shahada, na Sifa Nyingine za Kitaaluma katika Elimu ya Juu katika nchi za Kiafrika, yaliyofikiwa mwaka 1981 na kupitiwa tena mwaka 2002;
- Mapatano ya Kimataifa kuhusu Kuhifadhi Urithi Usioshikika wa Kiutamaduni, yaliyofikiwa mwaka 2003 katika kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO mjini Paris (Ufaransa);
- Mkataba wa Mwamko wa Kiutamaduni Barani Afrika, uliofikiwa mjini Khartoum mwaka 2006;
- Mpango-Kazi wa Lugha kwa Afrika, uliokubaliwa mjini Khartoum mwaka 2006;
- Mpango-Kazi wa Muongo wa Pili wa Elimu kwa Afrika, uliokubaliwa na Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa mwaka 2006.

Kusudi la mwongozo huu ni kuthibitisha msimamo wa sera isemayo kwamba elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi haina budi kuchaguliwa kuwa mfumo mkuu wa elimu katika nchi za Kiafrika, kwa lengo la kuleta mabadiliko katika jamii za Kiafrika. Lengo la mabadiliko haya, hatimaye, ni kupunguza umaskini kupitia maendeleo endelevu yaliyojengwa katika msingi wa lugha na tamaduni za Kiafrika. Kwa sababu hii, elimu hii haina budi kusakwa kupitia programu za asasi zilizopo, ambazo uwezo wake hauna budi kuimarishwa vilivyo. Mfumo wa elimu wa aina hii siyo tu kwamba huleta usawa katika kupata fursa na mafanikio kwa watoto wote, bali pia huinua kiwango cha ubora wa elimu inayotolewa kwa kuwa lugha ya mjifunzaji mwenyewe hutumiwa kama lugha ya kufundishia, huku kukiwa na fursa ya kujifunza lugha nyingine za kitaifa na za kigeni. Aidha, hufungulia uwezo wa ubunifu walio nao watu na kuimarisha mshikamano wa jamii. Kwa kutumia lugha za Kiafrika, mfumo wa elimu husaidia kuimarisha sera za kutoa madaraka mikoani zinazotumiwa na baadhi ya nchi.

Sera ya kutoa elimu kwa lugha na tamaduni nyingi huhitaji:

1. **Kuwekwa kwa mifumo ya sera na ya kutunga sheria;**
2. **Kutoa elimu ya jumla ya utambuzi na utetezi katika ngazi ya kitaifa na kuendelezwa kwa mitandao ya kimkoa;**
3. **Kuziimarisha na kuzijengea uwezo taasisi;**
4. **Kuendeleza mikakati ya kusimamia na kutathmini ukadiriaji wa matokeo ya ujifunzaji na ufuatiliaji;**
5. **Kuendeleza mtaala na kutoa mafunzo kwa waelimishaji;**
6. **Kuchapisha kwa lugha za kitaifa na kwa kuzingatia sera za vitabu;**
7. **Kutafiti na kufundisha uvumbuzi;**
8. **Kuandaa raslimali za kifedha.**

Education Program Development Fund (EPDF) na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (BMZ/ GTZ). Toleo la awali la mwongozo huu wa sera – liliowasilishwa mbele ya mawaziri hawa na kuhaririwa ili kuzingatia mapendekezo yao – liliandikwa na wataalamu wafuatao: Bw. Camille Roger Abolou, Bw. Sammy Beban Chumbow, Bw. Abou Diarra, Bw. Issa Djarangar, Bw. Marcel Diki-Kidiri, Bw. Maman Mallam Garba, Bw. Abou Napon, na Bw. Norbert Nikièma, na msaada kutoka kwa Bw. Adama Ouane, Bi. Hassana Alidou na Bi. Christine Glanz kutoka UNESCO Institute for Lifelong Learning (UIL). Kikundi kilichopewa jukumu la kuandika mwongozo huu wa sera kilitumia muhtasari wa kutetea sera wenye kuzingatia ushahidi na mazoezi uliobuniwa na UIL na ADEA.

1. Sera na kutunga sheria

Sera ya kutoa elimu kwa lugha na tamaduni nyingi huhitaji hatua zifuatazo zichukuliwe:

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kuunda sera ya lugha na elimu kwa kupendelea lugha za Kiafrika kwa uwazi, kupitia mashauriano ya kitaifa kama vile vikao vya mabaraza, »mabunge ya makabwela«, na mikutano ya kitaifa;
- Kujumuisha kipengele cha lugha katika hati rasmi zote za kisheria (katiba, sheria za msingi, sheria zinazojenga lugha, maagizo, amri za Rais, maamuzi, n.k.);
- Kutunga kanuni zinazolingiza matumizi ya lugha za Kiafrika katika mitihani na mashindano rasmi;
- Kuanzisha ushirikiano na vyama vya jamii ya kiraia, kama vile vyama vya wazazi na vyama vya waalimu, na kuwashirikisha katika utekelezaji wa sera ya kutumia lugha za kufundishia za Kiafrika katika mitihani na mashindano rasmi.

ii. Katika kipindi cha muda mfupi au wa kati (kutegemeana na hali ya nchi ilivyo):

- Kutumia lugha za Kiafrika katika shughuli zinazoboresha taswira yake;
- Kutumia lugha za Kiafrika katika shughuli za serikali na utawala, mfumo wa mahakama, vyombo vya habari, na elimu – shughuli ambazo katika nchi nyingine kwa sasa zinafanywa kwa lugha rasmi za kigeni pekee;
- Kujenga utashi wa kisiasa unaohitajika katika kuendeleza sera ya kutoa elimu kwa lugha na tamaduni nyingi.

iii. Katika kipindi cha muda wa kati au muda mrefu (kutegemeana na hali ya nchi ilivyo):

- Kutoa madaraka mikoani kwa utekelezaji wa sera hii kwa kushirikisha, katika ngazi ya taifa, vitengo mbalimbali vya usimamizi (majimbo, mkoa, wilaya, n.k.);
- Kuweka uwezekano wa kutafsiri sera zilizoandikwa katika lugha rasmi za kigeni kwenda katika lugha enyeji, ili kutimiza haki ya kila mtu kupata taarifa kwa lugha yake mwenyewe;
- Kuupa kila mkoa (katika nchi) uwezekano wa kuwa na sera ya lugha inayokidhi mahitaji yake husika.

2. Kutoa elimu ya utambuzi katika ngazi ya taifa na mitandao ya mikoani

2.1 Kuhusu kutoa elimu ya utambuzi na utetezi, hatua zifuatazo hazina budi kuchukuliwa:

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kubainisha matarajio ya jamii enyeji;
- Kutekeleza mpango wa mawasiliano kuhusu kuendeleza elimu itolewayo kwa lugha a tamaduni nyingi, kwa kushirikisha asasi za jamii ya kiraia (vyama vya wafanyakazi, vyama vya wazazi, n.k.);
- Kuarifu watu wa kada zote za jamii (viongozi wa kisiasa, raia, viongozi wakuu wa kidini, watoa maoni, n.k.) kuhusu sera ya kutoa elimu kwa lugha na tamaduni nyingi;
- Kutoa elimu ya utambuzi miongoni mwa viongozi waandamizi wa wizara (makatibu wakuu, wakurugenzi wakuu, wakurugenzi katika ngazi ya taifa na mkoa) kwa kufanya kampeni za mara kwa mara za kutetea sera ya lugha na mikakati ya utekelezaji wake vikubalike vizuri zaidi;

- Kutoa nyaraka zifaazo kwa kazi hii ya kutoa elimu ya utambuzi, kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano na vyombo mbalimbali vya mawasiliano.
- ii. Katika kipindi cha muda wa kati:**
- Kuanzisha ushirikiano kati ya serikali na jamii ya kiraia ili kuhakikisha elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi inakuwa bora kwa kuanzisha au kuimarisha mfumo wa udhibiti;
 - Kuanzisha ushirikiano wa sekta nyingi.

2.2 Mitandao ya kimkoa

Sera ya kutoa elimu kwa lugha na tamaduni nyingi itatekelezwa katika ngazi ya taifa, ngazi ndogo kimkoa, na ngazi ya mkoa. Kwa ngazi ya mkoa, itakuwa lazima kuanzisha mitandao midogo kimkoa na mitandao ya kimkoa na mpango wa kimkakati unaohusisha hatua za kuchukuliwa katika kipindi cha muda mfupi na cha muda wa kati katika ngazi zote.

- i. Katika kipindi cha muda mfupi au wa kati (kutegemeana na hali ya nchi ilivyo):**
- Kupandisha hadhi ya lugha zinazozungumzwa na watu wengi katika maeneo yanayotambuka mpaka wa nchi na nchi ili zitumiwe katika elimu na kwa mawasiliano miongoni mwa makundi makuu ya ngazi ya kimkoa na ya chini ya kimkoa.
- ii. Katika kipindi cha muda wa kati:**
- Kuleta ulinganifu wa mifumo na sera za elimu katika nchi mbalimbali, hususani kuhusu modeli za ufundishaji, mafunzo ya stahhada na vyeti, na ufundishaji wa lugha zinazozungumzwa na watu wengi katika maeneo yanayotambuka mipaka ya nchi na nchi.

3. Kuziimarisha na kuzijengea uwezo taasisi

Upungufu wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kutekeleza sera ya kutangamanisha lugha na tamaduni za kitaifa katika elimu ni changamoto kuu kwa nchi za Kiafrika. Hivyo basi, tunapendekeza kuchukuliwa kwa hatua zifuatazo ili kukabiliana na changamoto hii kwa kupitia mikakati ya kutoa mafunzo kwa wakufunzi na kusambaza waalimu.

- i. Katika kipindi cha muda mfupi:**
- Kuimarisha na kuhamasisha watu kuimarisha ujuzi mbalimbali kitaasisi kuhusu mfumo wa elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi;
 - Kuunda chombo cha uongozi katika wizara ya elimu ili kutoa mafunzo kwa kushirikisha idara zote katika ngazi zote;
 - Kuweka mpango wa mafunzo na mikakati ya kusambaza waalimu katika muktadha wa lugha nyingi;
 - Kuhakikisha kwamba maofisa waandamizi wa elimu hujifunza sera hii na mikakati ya kutekeleza;
 - Kujenga utambuzi miongoni mwa maofisa waandamizi wa wizara (makatibu wakuu, wakurugenzi wakuu, wakurugenzi katika ngazi ya taifa na mkoa) kwa kufanya kampeni za mara kwa mara za utetezi ili sera ya lugha na mikakati ya utekelezaji wake viweze kukubaliwa vizuri zaidi;
 - Kutoa mafunzo kwa maofisa kuhusu kuandika lugha za Kiafrika.
- ii. Katika kipindi cha muda wa kati au muda mrefu (kutegemeana na hali ya nchi ilivyo):**
- Kutayarisha mpango-mama kwa pamoja na wadau wote wanaohusika na ratiba ya kuchukua hatua zifuatazo:
- Kuweka katika mpango ulio wazi na kuimarisha polepole lugha zote enyeji, zikiwemo lugha zinazozungumzwa na watu wachache, ili kuzifanya ziwe nyenzo zifaazo kwa elimu na maendeleo ya taifa;

- Kuweka malengo ya muda mrefu ya kutumia lugha zote zilizopo katika nchi, kwa kuanza na zile zenye vifaa vingi zaidi vya elimu.

4. Tathmini na usimamizi

Sera hii itategemea taasisi zilizopo kutekeleza shughuli za kusimamia na kutathmini. Taasisi hizi zitapigwa jeki na kupewa jukumu la usimamizi, ukaguzi, na kufuatilia na kutoa ushauri kwa shughuli za uvumbuzi, katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kutayarisha mpango-mama pamoja na wadau wote wanaohusika na pia ratiba ya shughuli za tathmini na usimamizi;
- Kutayarisha mfumo wa maarifa wa marejeleo kuhusu mchakato wa kutangamanisha lugha za kitaifa katika mifumo ya elimu (chekechea, sekondari, elimu ya juu);
- Kuweka hati za kuthibitisha, kuhalalisha, na kutambua ujuzi wa kielimu.

5. Mitaala na mafunzo

5.1. Kuendeleza mitaala na kutoa vifaa vya kufundishia

Kuendeleza mitaala:

Mapitio ya programu za elimu yana umuhimu maalumu kwa uratibu wa mafunzo kwa waalimu (kabla na baada ya kuanza kazi) kwa waalimu watakaoshiriki katika shughuli hii. Mapitio hayo huhusu pia wanafunzi, ambao umri na uwezo wao wa kujifunza hauna budi kuzingatiwa ili kuendeleza shughuli za kielimu zenye urari na zifaazo ili ziweze kuleta manufaa makubwa zaidi. Mapitio ya aina hiyo huhitaji hatua za lazima zifuatazo:

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kurasimisha desturi za kiutamaduni za jamii enyeji ili kuimarisha matumizi ya lugha na tamaduni za Kiafrika katika elimu;
- Kutangamanisha tamaduni za kitaifa katika mitaala kwa kutumia msingi wa mfumo wa marejeleo wa maarifa ya kiutamaduni ulioendelezwa kupitia njia shirikishi na kuhusishwa kwa fikra za pamoja za jamii mbalimbali enyeji zinazohusika. Mfumo huu wa maarifa hutumiwa kutayarisha miongozo na moduli kwa matumizi ya waalimu, katika ngazi zote za elimu;
- Kuingiza vipengele vya kiutamaduni vilivyotangamanishwa katika maandalio ya masomo ya ngazi mbalimbali za elimu, kutumia mkabala uliotangamanishwa kwa kubainisha masomo ambayo »yatapokea« vipengele hivi au mkabala unaofuata utaratibu wa kutenga vipindi maalumu vya masomo kwa ajili ya mafundisho haya mapya.

ii. Katika kipindi cha muda wa kati:

- Kuendeleza modeli za elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi kwa kuzingatia malengo ya jumla ya elimu na malengo maalumu yanayosakwa na matumizi ya lugha za Kiafrika katika mifumo ya elimu;
- Kutoa upendeleo kwa modeli zinazofaa zaidi, ambazo ni modeli za nyongeza, ambazo huhitaji matumizi ya lugha enyeji katika ngazi zote za elimu pamoja na ujifunzaji na matumizi halisi ya lugha rasmi, na ambazo zinapaswa kuleta manufaa makubwa zaidi ya ndani na nje;

- Kutegemeana na kiasi kilichofikiwa cha kutangamanisha lugha enyeji, fikiria kutumia modeli ya lugha mbili (lugha ya kwanza na lugha rasmi ya kigeni) au modeli ya lugha nyingi (lugha ya kwanza, lugha ya kitaifa inayozungumzwa na wengi, na lugha rasmi ya kigeni).

Mwongozo kwa waalimu:

- Kuhakikisha kwamba waalimu wanajifunza mkabala unaozingatia ujuzi, ambao unatumia na nchi nyingi za Kiafrika;
- Kutayarisha mbinu za kufundishia zilizo maalumu kwa masomo fulani katika lugha zote zinazofundishwa.

5.2. Kuandaa mpango wa mafunzo kwa waalimu

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kuanzisha mpango mkakati wa mafunzo kwa waalimu mahali pa kazi, kwa kuanza na mafunzo ya kupiga msasa. Utoaji wa mafunzo kwa waalimu na wasimamizi kabla na baada ya kuanza kazi utahitaji kuzijengea uwezo taasisi zinazotoa mafunzo kitaifa (vyuo vikuu, taasisi za mafunzo ya juu ya ualimu, vyuo vya ualimu, na taasisi nyingine za mafunzo);
- Kuanzisha programu ya mafunzo kabla ya kuanza kazi kwa kuzingatia mkabala mpya uliokubaliwa na taifa;
- Kupitia sifa za waalimu ili kuona kama zinakidhi mahitaji mapya;
- Kwa ufupi, vipindi vya muda wa kati na muda mrefu hujenga uwezo wa maofisa na watendaji wanaofanya kazi katika elimu, hususani wasimamizi, wakufunzi wa wakufunzi, waalimu, wataalamu wa mitaala, na wataalamu wa tathmini;
- Kupitia upya programu za mafunzo kwa kutilia maanani sera ya elimu kwa lugha na tamaduni nyingi;
- Kutumia modeli zilizopo za elimu kwa lugha nyingi ambazo zimeonyesha kufaa.

ii. Katika kipindi cha muda wa kati:

- Kutumia kikamilifu ujuzi na maarifa ya wenyeji kuhusu elimu kwa lugha za Kiafrika;
- Kuanzisha vituo vya mafunzo kwa wakufunzi vya ngazi ya kimkoa, kuchangisha raslimali kutoka nchi mbalimbali ili kutoa mafunzo kwa wakaguzi na washauri wa ufundishaji, ambao nao watatoa mafunzo kwa watendaji wengine walio chini yao, hivyo kuhakikisha kuwa idadi inajizidisha;
- Kuimarisha uwezo wa wakufunzi wa wakufunzi kuhusu elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi, kwa kutumia msingi wa utangamano wa ngazi ya kimkoa na ngazi ndogo kimkoa unaozingatia matumizi ya lugha za Kiafrika za maeneo yanayotambuka mipaka ya nchi na nchi katika elimu. Kusudi kuu la mkakati huu ni kuchanga uzoefu na ujuzi na kuwasaidia waalimu na wakufunzi kuweza kutembelea maeneo ya ngazi za chini kimkoa. Hii itasaidia kuzifanya lugha za Kiafrika kuwa na thamani zaidi katika soko la kazi;
- Kuanzisha mfumo wa maarifa wa marejeleo katika elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi ambao unaendana na Mapatano ya Arusha (yaliyopitiwa upya mwaka 2002) na sera ya Umoja wa Afrika kuhusu kutambua stahhada.

iii. Katika kipindi cha muda mrefu:

- Kuanzisha sera ya taifa kuhusu kuandikisha waalimu wapya inayoendana na sera ya elimu kwa lugha na tamaduni nyingi;
- Kuanzisha sera ya uandikishaji kwa vyuo vya ualimu inayotoa upendeleo kwa waombaji wanaozungumza lugha nyingi.

5.3. Mikakati ya kusambaza waalimu katika muktadha wa lugha nyingi

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kugawa madaraka ya kuandikisha waalimu kwa mintarafu ya matumizi ya lugha nyingi.

6. Kuchapisha vitabu kwa lugha za kitaifa na kwa kuzingatia sera za vitabu

Katika mfumo wa elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi, ni jambo la lazima kuchapisha vitabu mbalimbali vya shule kwa lugha nyingi, vilivyotungwa kuendana na hali halisi ya utamaduni kitaifa, kikanda, na kimataifa na kuendana na lugha mbalimbali zinazofundishwa au kutumiwa kama lugha za kufundishia. Hii huzipa nchi fursa ya kifahari ya kuanzisha sera ya vitabu vya shule inayojenga na kuendeleza mazingira yanayohitajika kwa uchapishaji wa vitabu wa ngazi ya taifa kufanywa na wachapishaji binafsi wa kitaifa na kimkoa, kwa matumaini ya kusaidia elimu ya watu inayoendelea kutolewa na kuendeleza mazingira ya elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi. Kwa sababu hii, hatua zifuatazo zinapendekezwa sana kuchukuliwa:

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kuhimiza utoaji wa vitabu katika maeneo husika na kubinafsisha shughuli za utoaji na usambazaji wa vitabu;
- Kutunga sera thabiti inayohakikisha watoto wote wanapata vitabu;
- Kuunga mkono, kama sehemu ya lazima ya sera ya vitabu, ukuaji na uendelezaji wa mifumo ya uchapishaji katika ngazi ya taifa, kusaidia ujifunzaji wa mbinu zinazohitajika katika kutoa vitabu vyenye kiwango kizuri cha ubora.

7. Utafiti

i. Katika kipindi cha muda mfupi:

- Kuanzisha ushirikiano rasmi miongoni mwa taasisi za utafiti, wizara, mamlaka za maeneo husika, watoa huduma mbalimbali, na viwanda;
- Kutunga sera ya utafiti inayokusudia kuanzisha au kuimarisha taasisi za utafiti na mafunzo;
- Kuongeza fedha kwa ajili ya utafiti na kuongeza ushirikiano miongoni mwa mashirika ya kikanda na ya kimataifa;
- Kusaidia uendelezaji wa mazingira ya elimu kwa lugha nyingi ili kuimarisha ujuzi wa lugha wa wajifunzaji, katika mifumo rasmi na isiyo rasmi.

ii. Katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu:

- Kufanya utafiti msingi katika sayansi za jamii kama sharti la kuleta elimu fanisi kwa lugha na tamaduni nyingi, kwa lengo la kuweka msingi wa kuendeleza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya lugha na masomo yanayofundishwa;
- Kuhusisha utafiti wa kiutendaji na utafiti msingi ili kukidhi mahitaji ya watendaji katika uwanja husika; kutoa kipaumbele kwa maelezo ya kilahaja, kiisimu-jamii, na ya kiistilahi, ambayo yanaweza kutumiwa kama mwongozo katika kuchagua lugha za kufundishia/lugha za kufundishwa katika ngazi ya taifa na/au ya kimkoa.

8. Kuchangisha raslimali

- Kuchangisha fedha za kutosha kutoka ndani na nje ili kutekeleza sera ya elimu kwa lugha na tamaduni nyingi;
- Katika bajeti za taifa, panga kutenga fedha za kutosha zinazohitajika katika kutekeleza sera ya elimu kwa lugha na tamaduni nyingi;
- Kujitahidi kutafuta raslimali nyingine kutoka katika makundi makubwa ya kiuchumi katika ngazi ya chini kimkoa na ngazi ya kimkoa; na kutoka katika mashirika ya ushirikiano wa kimaendeleo wa pande mbili au wa pande nyingi;
- Kuvipatia vyombo husika raslimali vinazozihitaji;
- Kuhakikisha kunakuwepo na utoaji fedha ulio endelevu kwa ajili ya elimu isiyo rasmi, ambayo huelekea kupata sehemu ndogo sana ya raslimali zinazotengwa kwa ajili ya elimu.

Hitimisho

Tunarudia kusema kwamba mafanikio ya elimu itolewayo kwa lugha na tamaduni nyingi hutegemea:

- Maamuzi yafanywe kwa njia ya kushauriana, shirikishi, na ya kidemokrasia;
- Kutumia kwa kiwango cha juu kabisa maarifa ya kitaifa na kuiweka sera hii katika matendo kwa kuitangamanisha katika programu za mipango na maendeleo za nchi mbalimbali, hususani kupitia bajeti zao za elimu.

Nyaraka za sera za Afrika

Hapa chini kuna orodha ya baadhi ya mipango-kazi, mapatano, na hati ambazo serikali za nchi za Afrika zimekuwa zikiziunda tangu miaka ya 1970 ili kuzisaidia lugha za Kiafrika ziweze kutumiwa katika elimu, kujenga mazingira yenye elimu na kuimarisha maendeleo ya jamii.

- Cultural Charter for Africa/Hati ya Utamaduni kwa Afrika (1976)
- Lagos Plan of Action/Mpango-Kazi wa Lagos (1980)
- Declaration of the Cultural Aspects of the Lagos Plan of Action/
Azimio la Vipengele vya Kiutamaduni vya Mpango-Kazi wa Lagos (1985)
- Organization of African Unity Language Plan of Action for Africa/
Mpango-Kazi wa Lugha wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika kwa Afrika (1986)
- Draft Charter for the Promotion of African Languages in Education/
Rasimu ya Hati ya Kuhimiza Matumizi ya Lugha za Kiafrika katika Elimu (1996)
- Harare Declaration/Azimio la Harare (1997)
- Nairobi Plan of Action for Cultural Industries in Africa/
Mpango-Kazi wa Nairobi kwa Tasnia za Tamaduni Barani Afrika (2005)
- Charter of the African Cultural Renaissance/
Hati ya Mwamko wa Kiutamaduni wa Kiafrika (2006)
- Language Action Plan for African Development/
Mpango-Kazi wa Lugha kwa Maendeleo ya Afrika (2006)

Tazama pia:

The Bamako Commitment on Universal Multilingualism/Maazimio ya Bamako kuhusu Matumizi ya Lugha Nyingi kwa Wote (2009) na Action Plan of the Bamako Commitment on Universal Multilingualism/Mpango-Kazi wa Maazimio ya Bamako kuhusu Matumizi ya Lugha Nyingi kwa Wote (2009)
(www.acalan.org)

Makubaliano ya kikanda ya hivi karibuni kuhusu matumizi ya lugha katika elimu kwa elimu na ujifunzaji wa vijana na watu wazima (www.unesco.org/uil):

- Bamako Call to Action, African Regional Conference in Support of Global Literacy/
Wito wa Bamako, Mkutano wa Kikanda wa Afrika wa Kuunga Mkono Mafunzo ya Kusoma na Kuandika Duniani (2007)
- African Statement on the Power of Youth and Adult Learning and Education for Africa's Development, CONFINTEA VI Preparatory Conference in Africa/
Kauli ya Afrika kuhusu Nguvu ya Ujifunzaji na Elimu kwa Vijana na Watu Wazima kwa Maendeleo ya Afrika, Mkutano wa Maandalizi wa CONFINTEA VI Barani Afrika (2008)

Kiambatisho 3:

Taasisi za Afrika

Taasisi na mashirika mengi barani Afrika yamekuza utaalamu wa hali ya juu katika uwanja wa lugha katika elimu. Orodha iliyopo hapa chini haijumuishi taasisi na mashirika yote yaliyopo barani, bali imeandaliwa kukuchochea kufanya utafiti wako mwenyewe.

Taasisi na mashirika mbalimbali ya kimataifa:

- Association for the Development of Education in Africa/ Shirika la Maendeleo ya Elimu Afrika (ADEA) (www.adeanet.org)
- African Academy of Languages/Taasisi ya Kupatanisha Lugha za Kiafrika (ACALAN), Mali (www.acalan.org)
- AFRILEX, African Association for Lexicography/Chama cha Leksikografia Afrika (www.afrilex.africanlanguages.com)
- Bisharat! Asasi ya lugha, tekinolojia, na maendeleo (www.bisharat.net)
- Maaya – the World Network for Linguistic Diversity/Mtandao wa Kimataifa wa Uanuwai Lugha, ulianzishwa na African Academy of Languages/Taasisi ya Kupatanisha Lugha za Kiafrika (ACALAN), kwa msaada wa Umoja wa Afrika (www.maayajo.org)

Vyuo vikuu, taasisi za utafiti, na vyama vya lugha

- Idara za Isimu na Elimu za vyuo vikuu barani Afrika kama vile Chuo Kikuu cha Ibadan, Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Wagadugu, Chuo Kikuu cha Yaunde, n.k.
- Centre for Advanced Studies of African Society/Kituo cha Taaluma za Juu za Jamii ya Kiafrika (CASAS), Afrika Kusini
- The Educational Research Network for West and Central Africa/Mtandao wa Utafiti wa Elimu kwa Afrika Magharibi na Kati (ERNWACA)
- Taasisi ya Taifa ya Maendeleo ya Elimu (INDE), Msumbiji
- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (sasa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili), Tanzania
- Project for the Study of Alternative Education in South Africa/Mradi wa Utafiti wa Elimu Mbadala Afrika Kusini (PRAESA)
- Vyama / Kamati za lugha kama vile Chama cha Lugha ya Kiganda (Uganda), Chama cha Lugha ya Kibafuti (Kameruni)
- PROPELCA/Mradi wa utafiti wa njia bora za kufundisha lugha nchini Kameruni

Wizara za Elimu katika nchi zinazotekeleza mpango wa elimu kwa lugha nyingi kisekta (Ethiopia, Malawi, Msumbiji, Afrika Kusini) na nchi zilizo katika mchakato wa kupanua utekelezaji (Bukinafaso, Chadi, Ghana, Mali, Nijeri) na vilevile bodi za lugha kitaifa kama vile Pan South African Language Board/Bodi ya Lugha Zote Afrika Kusini (PANSALB).

Asasi nyingi zisizo za kiserikali zinazoshughulikia masuala ya maendeleo ndani na nje ya sekta ya elimu na vilevile **shughuli za biashara na watoa huduma mbalimbali katika sekta rasmi na isiyo rasmi ya uchumi** hutumia lugha za Kiafrika katika mawasiliano yao kwa njia ya mdomo na maandishi. Ili kukidhi mahitaji yao ya mawasiliano, wametafiti na kuendeleza istilahi mbalimbali.

Vyombo vya habari kama vile vituo vya redio, magazeti, vituo vya televisheni, maandishi, na wachapishaji mbalimbali.

Kiambatisho 4:

Programu za elimu kwa lugha nyingi/mbili Afrika

Programu zifuatazo za elimu kwa lugha-mama au lugha mbili barani Afrika zilipitiwa wakati wa utafiti wa tathmini (Alidou na wenzie, 2006). Programu hizo zimewasilishwa hapa ili kujaribu kumwonyesha msomaji kiwango cha kazi iliyokwishafanywa tayari katika uwanja huu. Ikumbukwe kwamba orodha hii haijumuishi programu zote. Kwa sasa, baadhi ya nchi zimeanzisha programu mpya, kama vile Ghana, ambayo mwaka 2007, ilianzisha »*Ghanaian National Literacy Acceleration Programme (NALAP)*« [Programu ya Taifa ya Kuharakisha Ujuzi wa Kusoma na Kuandika nchini Ghana] ambayo ni programu ya kusoma inayoendeshwa nchini kote katika lugha 11 za Ghana na Kiingereza kama lugha ya pili kwa mwaka wa kwanza na wa pili katika shule ya chekechea na darasa la kwanza hadi la tatu katika shule ya msingi. Mwaka 2008, Afrika Kusini ilizindua »*Kha Ri Gude Mass Literacy Campaign*« [Kampeni ya kitaifa ya Kha Ri Gude ya Mafunzo ya Kusoma na Kuandika katika lugha 11]. Mwaka 2009, shirika lisilo la kiserikali liitwalo Tin Tua nchini Bukinafaso lilishinda Tuzo ya UNESCO ya King Sejong Literacy Prize kwa ajili ya kufanikisha programu yake ya matumizi ya lugha nyingi katika elimu isiyo rasmi kwa vijana na watu wazima.

Ili kuendelea kupeana muhtasari wa jumla wa kazi ya utetezi na kubadilishana maarifa inayoendelea katika uwanja huu, wasomaji wanahimizwa kutuma taarifa na tathmini kuhusu programu zao kwa UNESCO Institute for Lifelong Learning (uil@unesco.org).

Nchi	Programu / inaendeshwa na
Afrika Kusini	Project for the Study of Alternative Education in South Africa (PRAESA) [Mradi wa Utafiti wa Elimu Mbadala Afrika Kusini]: Elimu kwa lugha nyingi, programu za mafunzo kwa waalimu na wakufunzi chini ya Kitivo cha Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Cape Town
Afrika Kusini	Elimu kwa lugha-mama kati ya mwaka 1955 – 2005 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Benini	Programu ya elimu ya awali utotoni kwa lugha-mama kati ya mwaka 1975 – 1989 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Botswana	Programu ya elimu rasmi inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Bukinafaso	<i>Programme d'Education Bilingue</i> inaendeshwa na <i>Ministère de l'Enseignement de Base et de l'Alphabétisation</i> (MEBA) [Wizara ya Elimu ya Msingi na Kusoma]
Bukinafaso	Shule za Pambizoni inaendeshwa na UNICEF, MEBA, na washirika wengine
Bukinafaso	Vituo vya Elimu ya Msingi isiyo rasmi inaendeshwa na MEBA na UNICEF
Chadi	Programu ya ufundishaji kwa lugha ya taifa inaendeshwa na Wizara ya Elimu na GTZ/PEB

Nchi	Programu / inaendeshwa na
Eritirea	Programu ya elimu kwa lugha-mama kuanzia miaka ya katikati ya miaka ya 1990 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Ethiopia	Programu ya elimu kwa lugha-mama tangu uhuru inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Ghana	Shule zitoazo elimu kwa lugha mbili kati ya mwaka 1971 – 2002 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Ghana	Local Languages Initial Literacy pilot project [Mradi wa majaribio wa Mafunzo ya Awali ya Kusoma na Kuandika kwa Lugha Enyeji] inaendeshwa na Government Education Service
Ghana	Assistance to Teacher Education Programme (ASTEP) [Programu ya Kusaidia Mafunzo ya Ualimu] inaendeshwa na GTZ
Ghana	Childscope project in the Afram Plains [Mradi wa Mtoto-Shule-Jamii katika Nyanda za Afram] inaendeshwa na UNICEF
Ghana	Shepherd School Programme (SSP) [Programu ya Elimu ya Msingi kwa Jamii za Wafugaji] inaendeshwa na Shirika la Action Aid
Ghana	Vyuo vya mafunzo ya ualimu inaendeshwa na GTZ
Ghana	Uchapishaji na usambazaji wa kiwango kikubwa wa vitabu vya kiada na miongozo ya waalimu katika lugha kuu mbili inaendeshwa na Benki ya Dunia
Gine (Konakiri)	Programu ya elimu kwa lugha-mama kati ya mwaka 1966 – 1984 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Ginebisau	Shule za majaribio ya elimu kwa lugha mbili kati ya mwaka 1987 – 1997 inaendeshwa na Wizara ya Elimu na msaada kutoka Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) na asasi isiyo ya kiserikali ya Ureno (CIDAC)
Kameruni	<i>Projet de recherche opérationnelle pour l'enseignement de langues au Cameroun</i> (PROPELCA) [Mradi wa utafiti wa njia bora za kufundisha lugha nchini Kameruni] inaendeshwa na Chuo Kikuu cha Yaunde
Kenya	Rehema School [Shule ya Rehema] inaendeshwa na Rehema Daycare, School and Orphan Centre [Shule na Kituo cha Kulelea Watoto na Watoto Yatima cha Rehema]
Liberia	Sera ya lugha na elimu kwa elimu itolewayo kwa lugha nyingi inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Malawi	Sera ya elimu ya lugha na Shule za Jamii inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Mali	<i>Écoles de la Pédagogie Convergente</i> [Shule za Majaribio ya Elimu ya Msingi kwa Lugha za Kitaifa] inaendeshwa na Wizara ya Elimu, <i>Centre international audiovisuel d'études et de recherches</i> (CIAVER) ya Ubelgiji, <i>Agence de coopération culturelle et technique</i> (ACCT, sasa OIF)
Mali	Centres d'éducation pour le développement (CED) [Vituo vya Elimu kwa Maendeleo] inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Mali	Programu ya Mafunzo ya Kusoma na Kuandika inaendeshwa na <i>Direction nationale de l'alphabétisation fonctionnelle et de la linguistique appliquée</i> (DNAFLA) [Kurugenzi ya Taifa ya Mafunzo Maalumu ya Kusoma na Kuandika na Isimu Tumizi]
Mali	Mradi wa elimu isiyo rasmi kwa watoto wasiokuwa shule na wanawake inaendeshwa na Wizara ya Elimu ya Msingi na UNICEF
Msumbiji	<i>Projecto de Escolarização Bilingue em Moçambique</i> (PEBIMO) [Mradi wa Majaribio wa Elimu kwa Lugha Mbili Msumbiji] kati ya mwaka 1993 – 1997 inaendeshwa na Wizara ya Elimu

Nchi	Programu / inaendeshwa na
Namibia	Village School Programme in J/'Hoan [Programu ya Shule ya Kijiji huko J/'Hoan] inaendeshwa na Taasisi ya Nyae Nyae
Namibia	Ondao Mobile School project [Mradi wa Shule Inayohamama ya Ondao] inaendeshwa na Shirika la Misaada ya Kibinadamu la Norwe nchini Namibia (NAMAS)
Nijeri	Shule za majaribio ya elimu kwa lugha mbili inaendeshwa na Wizara ya Elimu ya Msingi na GZT-2PEB
Nijeri	Shule za majaribio ya elimu kwa Lugha mbili (Kifaransa-Kihausa) inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Nijeria	Six-Year Primary Project (Ife Mother-tongue Education Project) [Mradi wa Majaribio ya Elimu ya Msingi kwa Lugha-Mama nchini Nijeria (Mradi wa Elimu kwa Lugha-mama ya Kiife)] inaendeshwa na Chuo Kikuu cha Obafemi Awolowo (kilichokuwa Chuo Kikuu cha Ife)
Nijeria	Rivers Readers' Project [Mradi wa Wasomaji wa Jimbo la Rivers] inaendeshwa na Serikali ya Jimbo la Rivers
Senegali	<i>Ecoles Communautaires de Base</i> (ECB) [Shule za jumuiya za elimu ya msingi] inaendeshwa na ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu, asasi zisizo za kiserikali na jumuiya husika
Senegali	Elimu isiyo rasmi inaendeshwa na Associates in Research and Education for Development (ARED)
Somalia	Elimu kwa lugha-mama kati ya mwaka 1973 – 1986 inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Tanzania	Sera na nyenzo kwa ajili ya Kiswahili katika elimu rasmi, programu za kusoma na kuandika na mikakati ya baada ya mafunzo ya kusoma na kuandika tangu uhuru inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Tanzania na Afrika Kusini	Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA) [Mradi wa Lugha ya Kufundishia Tanzania na Afrika Kusini] inaendeshwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Tanzania), Chuo Kikuu cha Oslo (Norwe), na Chuo Kikuu cha Western Cape (Afrika Kusini)
Togo	<i>Ecole d'Initiative Locale</i> (EDIL) [Shule za Jamii] inaendeshwa na jamii husika
Uganda	Basic Education in Urban Poverty Areas (BEUPA) [Elimu ya Msingi katika Maeneo Maskini ya Mjini] inaendeshwa na GTZ
Uganda	Community Oriented Primary Education (COPE) [Elimu ya Msingi ya Jamii] inaendeshwa na GTZ
Uganda	Sera ya Elimu ya Lugha kwa Programu ya Elimu ya Msingi kwa Wote inaendeshwa na Wizara ya Elimu
Zambia	Primary Reading Programme [Programu ya Kusoma kwa Shule za Msingi] inaendeshwa na Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (DFID)
Zambia, Afrika Kusini, Namibia, Botswana	Breakthrough to Literacy [Mwelekeo Mpya wa Mafunzo ya Kusoma na Kuandika] inaendeshwa na asasi isiyo ya kiserikali ya Molteno Project

Faharasa ya msamiati maalumu

Fasili zilizopo hapa chini zimefanyiwa marekebisho na kutumiwa katika muktadha wa lugha barani Afrika na timu ambayo hivi karibuni ilifanya tathmini kuhusu uzoefu wa elimu kwa lugha-mama na elimu kwa lugha mbili barani Afrika (Alidou na wenzie, 2006).

Tofauti kati ya lugha na lahaja

Kwa mtazamo kwa kiisimu, tofauti kati ya lugha na lahaja husisitiza kueleweka au kutoeleweka kwa lugha. Hivyo, ikiwa watu wanaozungumza lugha tofauti wanaweza kuelewana kwa kiasi cha kuridhisha na wanaweza kuwasiliana pasipo matatizo, basi watu hao huzungumza lahaja za lugha moja. Ikiwa hawawezi kuelewana kwa kiasi cha kuridhisha, basi watu hao huzungumza lugha tofauti.

Ujifunzaji lugha usio rasmi

Ujifunzaji usio rasmi hufanyika nje ya shule au nje ya miktadha ya kielimu. Ujifunzaji wa lugha ya kwanza/lugha-mama kwa kawaida hufanyika katika miktadha isiyo rasmi nyumbani na katika mazingira yanayomzunguka mtoto kabla hajaanza kwenda shule. Kisha, ni kawaida kwamba mtoto huendelea kujifunza lugha ya kwanza kupitia mafunzo rasmi ya lugha-mama kwa makusudi ya kitaaluma.

Ujifunzaji lugha ulio rasmi

Ujifunzaji ulio rasmi hufanyika katika miktadha rasmi ya kielimu. Kunaweza kuwa na ujifunzaji rasmi wa lugha ya kwanza, ya pili, ya tatu (na nyinginezo) shuleni.

Lugha-mama au lugha ya kwanza (L1)

Lugha-mama, kwa maana finyu, hufasiliwa kuwa ni lugha ambayo mtoto hujifunza kwanza kutoka kwa mtu anayemtimizia wajibu wa »mama« au mlezi.

Ili kukita vizuri fasili hii katika mazingira halisi ya lugha barani Afrika, tunafasili lugha-mama kwa mtazamo mpana kuwa ni lugha iliyoko (au zilizoko) katika mazingira yanayomzunguka mtoto na hutumiwa kwa mawasiliano ya kila siku, ambayo (au ambazo) »humlea« mtoto katika kipindi cha miaka minne ya kwanza katika maisha yake. Hivyo, lugha-mama ni lugha ambayo au ambazo mtoto hukua nazo na ambayo au ambazo mtoto hujifunza sarufi yake kabla ya kuanza shule. Katika miktadha ya lugha nyingi, watoto wanaweza kukua na lugha zaidi ya moja. Barani Afrika, mara nyingi watoto wana lugha-mama zaidi ya moja. Mara nyingi, lugha kadhaa huzungumzwa katika familia ya mtoto au katika mazingira yanayomzunguka. Hivyo, elimu inaweza kutolewa kwa kutumia mojawapo ya lugha za kwanza alizozioea mtoto.

Lugha ya kigeni

Lugha ya kigeni ni lugha ambayo mtu hakuizoea na ambayo haimudu vema. Inasisitizwa hapa kwamba kwa kuwaangalia wajifunzaji wengi barani Afrika, mara nyingi lugha rasmi ni lugha za kigeni. Kwa kuiangalia jamii, lugha rasmi (ambazo zilikuwa lugha za wakoloni) si lugha za kigeni tena kwani zimepata hadhi ya kuwa lugha rasmi na zimekuwepo kwa zaidi ya miaka 100 katika nchi za Kiafrika. Katika maeneo ya mjini ya nchi nyingi za Kiafrika, kuna watu ambao kihistoria wangeweza kuzungumza lugha za Kiafrika nyumbani, lakini sasa hujitambulisha kama wazungumzaji wazawa wa Kireno (kwa mfano, mjini Maputo au Luanda), Kifaransa (kwa mfano, mjini Dakar) au Kiingereza (kwa mfano, mjini Johannesburg au Nairobi).

Lugha ya pili (L2)

Katika waraka huu, neno »lugha ya pili« litatumiwa kumaanisha lugha ya pili iliyojifunzwa shuleni kwa madhumuni ya elimu rasmi, na lisichanganywe na lugha ya pili au nyingineyo ambayo mwanafunzi alijifunza katika mazingira yasiyo rasmi nje ya shule. Lugha rasmi barani Afrika ni lugha za kigeni kwa wanafunzi wengi wa Kiafrika na mara nyingi hujifunzwa tu kama lugha ya pili.

- **Kustawisha L2** hapa humaanisha kwamba wanafunzi hupewa L2 kama somo na pia msaada wa ziada wa jinsi ya kutumia L2 kama lugha ya kufundishia (kwa mfano, kufundisha msamiati maalumu kwa masomo mahususi).
- **Kuondosha L2** humaanisha kwamba wanafunzi kwa kawaida huwa katika darasa pamoja na wengine ambao lugha ya kufundishia (LYK) ni lugha yao ya kwanza (L1) na kwamba hutolewa nje ya mtaala mkuu ili kupewa mafunzo shadidi ya lugha ya pili katika nyakati fulanifulani. Kinachotokea ni kwamba wanafunzi wengine huendelea na masomo yao na wanafunzi wa L2 hubaki nyuma.

Lugha yenye wigo mpana wa mawasiliano (LWMM)

Lugha yenye wigo mpana wa mawasiliano ni lugha ambayo wazungumzaji wenye lugha-mama tofauti huitumia kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe. LWMM huitwa pia lugha ya mawasiliano au lugha ya biashara.

Lugha ya kufundishia (LYK)

Lugha ya kufundishia ni lugha ambayo hutumiwa kufundisha au kujifunza maudhui ya mtaala.

Elimu kwa lugha mbili

Elimu kwa lugha mbili hufasiliwa kwa namna tofautitofauti. Awali neno hili lilimaanisha matumizi ya lugha mbili kama lugha za kufundishia. Maana yake ilijumuisha kujifunza lugha mbili kama masomo, lakini haikuishia hapo tu. Hivyo, kwa kawaida humaanisha: lugha ya kwanza pamoja na lugha ya pili kama lugha za kufundishia. Nchini Afrika Kusini, elimu kwa lugha mbili hujulikana kuwa ni elimu itolewayo kwa lugha-mama (lugha ya kwanza) tangu kuanza hadi kumaliza shule pamoja na lugha ya pili inayofundishwa kama somo hadi kufikia kiwango cha juu cha ustadi.

Zaidi na zaidi, na hususani Amerika Kaskazini, neno hili limekuwa likitumika kumaanisha lugha ya kwanza kama lugha ya kufundishia kwa kipindi kifupi (tazama modeli wahishi za mpito) na kufuatiwa na lugha ya pili kama lugha ya kufundishia kwa kiasi kikubwa zaidi cha muda. Kwa maneno mengine, neno hili limekuwa likitumiwa vibaya kumaanisha mfumo wa elimu inayotolewa zaidi kwa lugha ya pili. Matumizi haya mabaya ya neno hili yamehamishiwa katika nchi nyingine nyingi barani Afrika ambako watu huita programu mbalimbali kuwa ni za lugha mbili hata kama lugha ya kwanza hutumiwa kidogo sana kama lugha ya kufundishia. Hapa chini kuna fasili ya modeli mbalimbali zinazotumiwa katika programu za elimu kwa lugha mbili (hamishi, wahishi, kawizi, za nyongeza).

Aina za modeli za elimu kwa lugha mbili:

1. **Modeli hamishi ya elimu:** Wajifunzaji huhamishwa kutoka katika matumizi ya lugha-mama na kutumia lugha rasmi/lugha ya kigeni kama lugha ya kufundishia mapema iwezekanavyo. Wakati mwingine hii hujumuisha kwenda moja kwa moja katika lugha rasmi/lugha ya kigeni kama lugha ya kufundishia katika mwaka wa kwanza shuleni.
2. **Modeli wahishi (au ya mpito):** Lengo la modeli hii linafanana na lile la modeli hamishi, nalo ni kutumia lugha moja tu shuleni, ambayo kwa kawaida ni lugha rasmi/lugha ya kigeni. Wajifunzaji wanaweza kuanza na lugha-mama na polepole kuelekea katika lugha rasmi/lugha ya kigeni kama lugha ya kufundishia. Ikiwa kipindi cha mpito kuelekea katika lugha rasmi/lugha ya kigeni huchukua mwaka mmoja hadi miaka minne, modeli hii hujulikana kama modeli wahishi ya mpito.
3. **Modeli kawizi:** Ikiwa kipindi cha mpito kutoka lugha-mama kama lugha ya kufundishia kuelekea katika lugha tofauti kitakawia hadi mwaka wa 5-6, hujulikana kama modeli kawizi ya mpito. Modeli kawizi yenye ufanisi inayoendelea kutumia lugha-mama kama somo baada ya mwaka 5-6 inaweza kuleta ujuzi wa lugha ya pili pasipo kuathiri ule wa lugha ya kwanza iwapo ufundishaji thabiti wa lugha ya kwanza na lugha ya pili utafanywa darasani pamoja na kuwepo kwa mafundisho yanayofaa ya kusoma na kuandika.
4. **Modeli za nyongeza (za lugha mbili) za elimu:** Katika modeli ya nyongeza ya elimu, lengo ni kutumia lugha-mama kama lugha ya kufundishia kuanzia mwanzo hadi mwisho (huku lugha rasmi au lugha ya kigeni ikifundishwa kama somo) au kutumia lugha-mama pamoja na lugha rasmi au lugha ya kigeni kama lugha mbili za kufundishia hadi kumaliza shule. Katika modeli ya nyongeza ya elimu, kamwe lugha-mama haiachi kutumiwa kama lugha ya kufundishia na kamwe haitumiwi chini ya asilimia 50 ya muda wa siku/somo. Hivyo basi, lengo ni kupata kiwango cha juu cha ustadi katika lugha-mama pamoja na kiwango cha juu cha ustadi katika lugha rasmi/lugha ya kigeni. Barani Afrika, modeli za nyongeza zinazoweza kutumiwa zinaweza kuwa ama:

- Lugha-mama kuanzia mwanzo hadi mwisho huku lugha rasmi/lugha ya kigeni ikifundishwa kama somo na mwalimu aliyebobea;
- Lugha mbili za kufundishia: lugha-mama hadi angalau mwaka wa 4-5 na kufuatiwa na matumizi ya polepole ya lugha rasmi/lugha ya kigeni hadi, lakini si zaidi ya, asilimia 50 ya muda kwa siku/somo hadi kumaliza shule;
- Elimu kwa lugha tatu: linaweza kuwa jambo lenye manufaa kuendeleza modeli ya elimu kwa lugha mbili kuwa modeli ya elimu kwa lugha tatu ambapo, pamoja na lugha-mama na lugha rasmi, pawepo na lugha yenye wigo mpana wa mawasiliano kitaifa (kwa mapendekezo, tazama pia Jedwali 2 na 4, Bodomo, 1996; Tadadjeu, 1996).

Elimu kwa lugha nyingi

Neno »elimu kwa lugha nyingi« lilitumiwa mwaka 1999 katika Azimio la 12 la Mkutano Mkuu wa UNESCO kumaanisha matumizi ya lugha zisizopungua tatu, kwa mfano, lugha-mama, lugha ya kimkoa au ya kitaifa na lugha ya kimataifa katika elimu. Azimio hili liliunga mkono mtazamo kwamba masharti ya kushiriki katika shughuli mbambali kitaifa au kimataifa na mahitaji maalumu ya jamii zenye lugha na tamaduni tofauti yanaweza tu kushughulikiwa na elimu itolewayo kwa lugha nyingi (UNESCO, 2003).

Maadili ya lugha nyingi

»Maadili ya lugha nyingi hutetea kukubaliwa na kutambuliwa kwa tofauti mbalimbali za lugha zilizopo miongoni mwa watu ili kuhakikisha kunakuwepo na mshikamano katika jamii na kuepuka kuparaganyika kwa jamii mbalimbali« (Ouane, 2009: 168). Maadili haya hutilia maanani upatanishi wa lugha mbalimbali miongoni mwa watu binafsi wanaozungumza lugha mbalimbali na katika jamii mbalimbali, katika nyanja zote za jamii na vitendo vya mawasiliano. Maadili ya lugha nyingi hutilia mkazo utumiaji wa lugha wa watu wa kawaida na ukamilishani wa lugha na lugha, na ujuzi anuwai wa lugha katika jamii fulani na vilevile miongoni mwa jamii mbalimbali na katika mazingira fulani. Kwa mtazamo huu, hakuna jamii yoyote inayoweza kudai kuwa inamiliki lugha fulani au kwamba kuna mipaka isiyobadilika ya lugha fulani.

- ADEA Secretariat. 2004. *The Quest for Quality: Learning from the African Experience*. Proceedings of the ADEA Biennial Meeting (Grand Baie, Mauritius, December 3-6, 2003). www.adeanet.org, imepatikana tarehe 15 Novemba 2009.
- ADEA na UIL. 2010. *Policy Guide on the Integration of African Languages and Cultures into Education Systems*. Tunis: ADEA.
- Adegbija, Efurosibina. 2003. Central Language Issues in Literacy and Basic Education: Three Mother Tongue Education Experiments in Nigeria. Ktk.: Adama Ouane (mh.). *Towards a Multilingual Culture of Education*. Hamburg: UNESCO Institute for Education. uk. 299-331.
- Alidou, Hassana, Maman Mallam Garba, Andillo A. Halilou, Laouali M. Maman, Abdoulaye Ibbo Daddy. 2009. Etude d'élaboration du document de stratégie nationale de généralisation de l'enseignement bilingue au Niger. Mars 2009. Ministère de l'éducation nationale de la République du Niger.
- Alidou, Hassana, André Batiana, Aimé Damiba, Afsata Kabore Pare, Emma Clarisse Remain Kinda. 2008. *Le Continuum d'éducation de base multilingue du Burkina Faso: une réponse aux exigences de l'éducation de qualité. Evaluation prospective du programme de consolidation de l'éducation bilingue et plan d'action stratégique opérationnel 2008 – 2010*. Rapport d'étude (version finale) mai 2008.
- Alidou, Hassana na Birgit Brock-Utne. 2006. Experience I – Teaching Practices – Teaching in a Familiar Language. Ktk.: Hassana Alidou, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa (ADEA), UNESCO Institute for Education (UIL), Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ). Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31. uk. 85-100.
- Alidou, Hassana, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. 2006. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa, UNESCO Institute for Education, Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit. Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31.
- Baker, Colin. 2006. *Foundations of Bilingual Education and Bilingualism* (4th ed.). Clevedon: Multilingual Matters.
- Bamgbose, Ayo (hakuna tarehe). *Language of Instruction Policy and Practice in Africa* http://www.unesco.org/education/languages_2004/affichlang_afrique.pdf na ramani ya lugha za Jumuiya ya Afrika Mashariki na matumizi yake katika elimu, imepatikana tarehe 12 Desemba 2009.

- Bamgbose, Ayo. 2000. *Language and Exclusion : the Consequences of Language Policies in Africa*. Hamburg: LIT.
- Bodomo, Adams. 1996. On Language and Development in Africa: The Case of Ghana. *Nordic Journal of African Studies* 5(2): 31-51.
- Brock-Utne, Birgit na Hassana Alidou. 2006. Experience II – Active Students – Learning through a language they master. Ktk.: Hassana Alidou, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa, UNESCO Institute for Education, Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit. Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31. uk. 101-117.
- Buchan, Amanda, Dr Rod Hicks, Tony Read. 2005. *Draft Evaluation Report of Year 1 of the Reading Pilot Project*. Sponsored by DCI and USAID on behalf of the Ministry of Education & Sports, November 2005.
- Busch, Brigitta. 2004. *Sprachen im Disput: Medien und Öffentlichkeit in multilingualen Gesellschaften*. DRAVA: Klagenfurt, Austria.
- Carr-Hill, Roy na Fiona Roberts. 2007. *Approaches to Costing Adult Literacy Programmes, especially in Africa*. Hamburg: UNESCO Institute for Lifelong Learning.
- Châtry-Komarek, Marie. 2003. *Literacy at Stake. Teaching Reading and Writing in African Schools*. Namibia: Gamsberg Macmillan Publishers.
- Châtry-Komarek, Marie. 1996. *Tailor-Made Textbooks. A Practical Guide for the Authors of Textbooks for Primary Schools in Developing Countries*. Oxford: CODE Europe.
- Cummins, Jim. 2008. Teaching for Transfer: Challenging the two Solitudes Assumptions in Bilingual Education. Ktk.: Jim Cummins (mh.). *Encyclopedia of Language and Education*, Volume 5: Bilingual Education. New York: Springer Science + Business Media LLC. uk. 65-75.
- Cummins, Jim. 2000. *Language, Power and Pedagogy: Bilingual Children in the Crossfire*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Cummins, Jim. 1984. *Bilingualism and Special Education: Issues in Assessment and Pedagogy*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Delisle, Jean na Judith Woodsworth. 1995. *Translators through History*. Amsterdam: John Benjamins Publishing and UNESCO Publishing.
- Dembélé, Martial na Bé-Rammaj Miaro-II. 2003. *Pedagogical Renewal and Teacher Development in Sub-Saharan Africa: A Thematic Synthesis*. Working Document for ADEA Biennial 2003, Grand Baie, Mauritius.
- Diki-Kidiri, Marcel. 2008. *Securing a Place for a Language in Cyberspace*. Paris: UNESCO.
- Djité, Paulin G. 2008. *The Sociolinguistics of Development in Africa*. Clevedon, Buffalo, Toronto: Multilingual Matters Ltd.
- Fafunwa, A., J. Macauley, J. Soyinka. 1989. *Education in Mother Tongue. The Ife Primary Education Research Project (1970-1978)*. Ibadan: Ibadan University Press.
- Fagerberg-Diallo, Sonja. 2006. *Learner Centered Processes and Approaches: The Connection between Non-Formal Education and Creating a Literate Environment*. Working Document. Biennale on Education in Africa 2006, Libreville, Gabon, March 27-31.
- Faye, Souleymane. 2006. *The Impact of Linguistic Dominance on Senegalese National Languages*. Paper presented at the conference »The power of language«, 16 April 2006, Dakar, Goethe-Institut.
- Fomba, Check Oumar na wenzie. 2003. *Étude de cas nationale : Mali. La pédagogie convergente comme facteur d'amélioration de la qualité de l'éducation de base au Mali. Analyse du développement de l'innovation et perspectives*. Working Document. Biennale de l'ADEA 2003, Grand Baie, Maurice, 3-6 décembre 2003.

- Gadelii, Karl E. 2004. *Annotated Statistics on Linguistic Policies and Practices in Africa*, www.african.gu.se/downloads/gadeliiireport.pdf, imepatikana tarehe 24 Aprili 2009.
- Galdamès, Viviana, Hassana Alidou, Ingrid Jung na Thomas Büttner (wah.). 2004. *L'Ecole Vivante : enseigner la langue maternelle dans un programme d'éducation bilingue*. Niamey: INWENT-2PEB/GTZ.
- Gorter, Durk na wenzie (hakuna tarehe). *Benefits of Linguistic Diversity and Multilingualism*. Position Paper of Research Task 1.2 on Cultural Diversity as an Asset for Human Welfare and Development. Sus.Div. (Sustainable Development in a Diverse World), EURODIV (Cultural Diversity in Europe), www.susdiv.org/uploadfiles/RT1.2_PP_Durk.pdf, imepatikana tarehe 2 Septemba 2009.
- Griefenow-Mewis, Catherine. 2004. How to Turn Oral African Languages into Written Languages? The Somali and Oromo Experience. Ktk.: Joachim Friedrich Pfaffe (mh.). *Making Multilingual Education a Reality for All. Operationalizing Good Intentions*. Proceedings of the joint Third International Conference of the Association for the Development of African Languages in Education, Science and Technology (ADALEST) and the Fifth Malawian National Language Symposium held at Mangochi, Malawi, 30 August – 3 September 2004. Zomba: Centre for Language Studies, University of Malawi and GTZ. uk. 230-237.
- Grin, Francois. 2005. The Economics of Language Policy Implementation: Identifying and Measuring Costs. Ktk.: Neville Alexander (mh.). *Mother-tongue based Bilingual Education in Southern Africa. The dynamics of implementation. Multilingualism, Subalternity and Hegemony of English*, Volume 4. Frankfurt a.M. and Cape Town: Multilingualism Network and Project for the Study of Alternative Education in South Africa. uk. 11-25.
- Guttman, Cynthia. 2003. *Education in and for the Information Society*. UNESCO Publications for the World Summit on the Information Society. Paris: UNESCO.
- Hartshorne, Ken. 1992. *Crisis and Challenge: Black Education 1910-1990*. Cape Town: OUP.
- Heugh, Kathleen, Carol Benson, Berhanu Bogale, Mekonnen Alemu Gebre Yohannes. 2007. *Final Report Study on Medium of Instruction in Primary Schools in Ethiopia*, 22 January 2007. Commissioned by the Ministry of Education Sept. to Dec. 2006.
- Heugh, Kathleen. 2006a. Theory and Practice – Language Education Models in Africa: Research, Design, Decision-making, and Outcomes. Ktk.: Hassana Alidou, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa, UNESCO Institute for Education, Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit. Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31. uk. 56–84.
- Heugh, Kathleen. 2006b. Cost Implications of the Provision of Mother-tongue and Strong Bilingual Models of Education in Africa. Ktk.: Hassana Alidou, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa, UNESCO Institute for Education, Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit. Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31. uk. 138-156.
- Human Development Report. 2004. *Cultural Liberty in Today's Diverse World*. New York: UNDP.
- Ilboudo, Paul Taryam. 2003. *Etude de Cas National - Burkina Faso. Pertinence de l'Education-Adaptation des Curricula et Utilisation des Langues Africaines: Le Cas de l'Education Bilingue au Burkina Faso*. Working document for the ADEA Biennial 2003, Grand Baie, Mauritius, 3-6 December 2003.
- Industry Canada. 2006. *Survey of Language Industry Companies in Canada. Translation, interpretation and language training*. www.btb.gc.ca/btb.php?lang=eng&cont=1045, imepatikana tarehe 27 Agosti 2009.

- ILO (Governing Body, Committee on Employment and Social Policy). 2007. *GB.298 ESP/4*. www.ilo.org/public/english/employment/policy/events/informal/download/esp-informal.pdf, imepatikana tarehe 27 Agosti 2009.
- International Reading Association. 2005. Draft Report. *Improving the Quality of Literacy Learning in the Content Areas – Situational Analysis of Secondary Level Education in Botswana*. UNESCO Section for General Secondary Education Division of Secondary, Technical and Vocational Education.
- Jessner, Ulrike. 2008. Multicompetence Approaches to Language Proficiency Development in Multilingual Education. Ktk.: Jim Cummins (mh.). *Encyclopedia of Language and Education* Volume 5: Bilingual Education. New York: Springer Science + Business Media LLC. uk. 91-103
- Légère, Karsten. 2004. Against the Myth of African languages Lacking Terminologies. Ktk.: Joachim Friedrich Pfaffe (mh.). *Making Multilingual Education a Reality for All. Operationalizing Good Intentions*. Proceedings of the joint Third International Conference of the Association for the Development of African Languages in Education, Science and Technology (ADALEST) and the Fifth Malawian National Language Symposium held at Mangochi, Malawi, 30 August – 3 September 2004. Zomba: Centre for Language Studies, University of Malawi and GTZ. uk. 37-58.
- Macdonald, Carol. 1990. *Main Report of the Threshold Project*. Pretoria: The Human Sciences Research Council.
- Mafundikwa, Saki. 2007. *Afrikan Alphabets: The Story of Writing in Afrika*. New York: Mark Batty Publisher.
- Muyeeba, Kyangubabi C.-M. 2004. Challenges of Making and Implementing Policy in the Multilingual State of Zambia. Ktk.: Joachim Friedrich Pfaffe (mh.). *Making Multilingual Education a Reality for All. Operationalizing Good Intentions*. Proceedings of the joint Third International Conference of the Association for the Development of African Languages in Education, Science and Technology (ADALEST) and the Fifth Malawian National Language Symposium held at Mangochi, Malawi, 30 August – 3 September 2004. Zomba: Centre for Language Studies, University of Malawi and GTZ. uk. 175-184.
- Mwinsheikhe, Halima Mohammed. 2003. Science and the Language Barrier: Using Kiswahili as a Medium of Instruction in Tanzania Secondary Schools as a Strategy of Improving Student Participation and Performance in Science. Ktk.: Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai na Martha Qorro (wah.). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam. E & D Publishers. uk. 129-149.
- Obanya, Pai. 1999. Education, Equity and Transformation from the Perspectives of Language Education. Ktk.: Leslie Limage (mh.). *Comparative Perspectives on Language and Literacy*. Selected Papers from the work of the 10th World Congress on Comparative Education Societies, Cape Town 1998. Dakar: UNESCO BREDA. uk. 17-30.
- OECD, African Development Bank. 2008. *African Economic Outlook 2008*. Paris, Tunis: OECD Publishing, African Development Bank.
- Okech, Anthony. 2002. Multilingual Literacies as a Resource. *Adult Education and Development* no. 59. www.dvv-international.de/index.php?article_id=398&clang=1, imepatikana tarehe 2 Septemba 2009.
- Ouane, Adama. 2009. My journey to and through a Multilingual Landscape. Ktk.: Birgit Brock-Utne na Gunnar Garbo (wah.). *Language and Power. The Implications of Language for Peace and Development*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota. uk. 164-171.
- Ouane, Adama (mh.). 2003. *Towards a Multilingual Culture of Education*. Hamburg: UNESCO Institute for Education.
- Ouedraogo, Rakissouiligr Mathieu. 2002. The Use of African Languages in Educational Systems in Africa. *Newsletter of UNESCO International Institute for Capacity Building in Africa* 4(4): 1-17, www.unesco-iicba.org/index.php?option=com_content&task=view&id=88&Itemid=88, imepatikana tarehe 2 Septemba 2009.

- Prah, Kwesi. 2005. Language and Instruction for Education, Development and African Emancipation. Ktk.: Birgit Brock-Utne & Rodney Kofi Hopson (wah.). *Languages of Instruction for African Emancipation*. Cape Town: CASAS, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers. uk. 23-50.
- Prah, Kwesi. 2003. Going Native: Language of Instruction for Education, Development and African Emancipation. Ktk.: Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai na Martha Qorro (wah.). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E & D Publishers. uk. 14-35
- Programme for International Student Assessment (PISA) 2006. *Where Immigrant Students Succeed – A Comparative Review of Performance and Engagement in PISA 2003*. Paris: OECD.
- Prophet, Robert na J. Dow. 1994. Mother-tongue Language and Concept Development in Science. A Botswana Case Study. *Language, Culture and Curriculum* 7 (3): 205-217.
- Reiner, Peter (forthcoming). Promise and Pitfalls. A Commercial View of Publishing in African Languages. Windhoek, Namibia. Ktk.: Adama Ouane na Christine Glanz (wah.). *Optimizing Learning and Education in Africa – The Language Factor – A Review and Analysis of Theory and Practice in Mother-Tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Hamburg, Tunis: UIL na ADEA.
- Rubagumya, Casmir. 2003. English Medium Primary Schools in Tanzania: a New Linguistic Market in Education? Ktk.: Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai na Martha Qorro (wah.). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E & D Publishers. uk. 149-170.
- Sampa, Francis K. 2005. Zambia's Primary Reading Program (PRP): Improving Access and Quality Education in Basic Schools. Paris: ADEA. www.adeanet.org imepatikana tarehe 21 Oktoba 2009.
- Stroud, Christopher. 2002. *Towards a Policy for Bilingual Education in Developing Countries*. New Education Division Document No. 10. Stockholm: Sida.
- Tadadjeu, Maurice. 1996. *The Cameroonian Experience of Teaching National Languages in Schools: Prospects for International Cooperation and African Integration*. Paper presented at the Panafrican Seminar on the Problems and Prospects on the Use of African National Languages in Education, Accra, Ghana, 26- 30 August 1996.
- Traoré, Samba. 2001. *La Pédagogie Convergente: Son Expérimentation au Mali et son Impact sur le Système Éducatif*. Genève: UNESCO Bureau International d'Éducation.
- UNESCO Institute for Statistics (UIS). 2009. *Information Sheet No. 1. Analysis of the UIS International Survey on Feature Film Statistics*. Montréal, Québec: UNESCO Institute for Statistics.
- UNESCO. 2005. *Science Report*. Paris: UNESCO.
- UNESCO. 2004. *Global Monitoring Report 2005. Education For All: The Quality Imperative*. Paris: UNESCO.
- UNESCO. 2003. Education Position Paper. *Education in a Multilingual World*. Paris: UNESCO.
- UNESCO. 2002. The Universal Declaration on Cultural Diversity. Adopted by the 31st Session of the General Conference of UNESCO, Paris, 2 November 2001. UNESCO: Paris, <http://unesdoc.unesco.org/images/0012/001271/127160m.pdf> imepatikana tarehe 2 Septemba 2009.
- UNESCO. 1953. *The Use of Vernacular Languages in Education*. Paris: UNESCO, Paris.
- United Nations. 2002. *Report of the World Summit on Sustainable Development*, Johannesburg, South Africa, 26 August-4 September 2002. New York; United Nations.
- Walther, Richard. 2007. *Vocational Training in the Informal Sector or How to Stimulate the Economies of Developing Countries?* Paris: Agence Française de Développement.
- Western Cape Education Department. 2002. *Language Policy in the Primary Schools of the Western Cape*. http://wced.wcape.gov.za/documents/lang_policy/index_exsum.html, imepatikana tarehe 11 Julai 2009.

- Wiesand, Andreas kwa kushirikiana na Michael Soendermann. 2005. The »Creative Sector« – *An Engine for Diversity, Growth and Jobs in Europe. An Overview of Research Findings and Debates*. Amsterdam: European Cultural Foundation.
- Wilmot, Eric Magnus. 2003. *Stepping Outside the Ordinary Expectations of Schooling: Effect of School Language on the Assessment of Educational Achievement in Ghana*. Paper presented at the 47th Annual Meeting of CIES March 12-16 in New Orleans.
- Wolff, Ekkehard. 2006. Background and History – Language Politics and Planning in Africa. Ktk.: Hassana Alidou, Aliou Boly, Birgit Brock-Utne, Yaya Satina Diallo, Kathleen Heugh, Ekkehard Wolff. *Optimizing Learning and Education in Africa – the Language Factor. A Stock-taking Research on Mother-tongue and Bilingual Education in Sub-Saharan Africa*. Association for the Development of Education in Africa, UNESCO Institute for Education, Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit. Working Document for the ADEA Biennial 2006, Libreville, Gabon, March 27-31. uk. 26-55.
- World Bank. 2000. *Female School Participation in West Africa*. Africa Region Findings 164, Washington D.C.
- World Bank. 2005. *In Their Own Language... Education for All*. Education Notes, June 2005.



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization



UNESCO Institute
for Lifelong Learning

Institut de l'unesco
pour l'apprentissage
tout au long de la vie



Association
pour le développement
de l'éducation
en Afrique

